

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TATU

Kikao cha Nne – Tarehe 9 Novemba, 2018

(Bunge Lilianza Saa Tatuhwaliwa)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tukae.

Katibu!

NDG. ASIA MINJA- KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kipindi cha maswali tuaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mbunge wa Nyang'hwale sasa aulize swali lake.

Na. 39

Upatikanaji wa Mikopo kwa Vikundi vya Vijana

MHE. HUSSEIN N. AMAR aliuliza:-

Vijana wengi wamekuwa na mwamko wa kuunda vikundi vya ujasiriamali kwa lengo la kupata mikopo inayotokana na 5% ya fedha inayotengwa na Halmashauri nchini kwa kufuata taratibu zote zilizowekwa.

(a) Je, ni kwa nini vikundi hivyo havipati mikopo hiyo pamoja na kwamba taratibu zote za wanavikundi zimefuatwa kwa mujibu wa sheria?

(b) Je, ni vikundi vingapi katika Jimbo la Nyang'hwale vimepata mikopo nani kiasi gani cha fedha?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu wa Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu

NAIBU WA WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba Ofisi ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mbunge wa Nyang'hwale lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2016/2017 Hallmshauri ya Wilaya ya Nyang'hwale ilitenga kiasi shilingi milioni 100 kwa ajili ya mikopo hiyo ambapo shilingi milioni 15 zilitolewa wa vikundi kumi vya wanawake na shilingi milioni 15 zilikopeshwa kwa vikundi saba vya vijana. Katika mwaka wa fedha 2017/2018 shilingi milioni 124.9 zilitengwa na shilingi milioni 15 zilikopeshwa kwa vikundi 14 vya wanawake na shilingi milioni 15 kwa vikundi kumi vya vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale ilitenga kiasi cha shilingi milioni 140 kwenye bajeti yake kwa ajili ya vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Mategemeo ya Serikali ni kwamba kwa kuwa sheria ya fedha ya Serikali za Mitaa Sura 290 imefanyiwa marekebisho ili kuwajibisha kisheria Maafisa Masuuli kuhusu utengaji wa 10% wa mapato ya ndani na utoaji wa mikopo hiyo kwa makundi ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, uwiano wa kiasi kinachotengwa kwenye bajeti na kinachotelewa sasa utakuwa mzuri zaidi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hussein Nassor Amar swalii la nyongeza

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Halmashauri mwaka 2016/2017 ilitenga milioni 100 na ikaweza kutoa takiribani milioni 30 haikuweza kufikia malengo (milioni 70 hazikutoka) na mwaka 2017/2018 malengo vilevile hayakutimia zaidi ya milioni 90 hazikuweza kutoka, kwa kuwa Serikali imeweka sasa kuwa ni sheria.

(a) Je, ambao hawatafikia malengo kwa mwaka huu ambao tumepitisha sheria watachukuliwa hatua gani?

(b) Je, Serikali ina mpango gani sasa kwa sababu Halmashauri zingi zinakuwa haina uwezo wa kufikia malengo ya kukusanyafedha kwa ajili ya kutenga hizo 10%; je, Serikali kwa mpango huu wa bajeti ijayo inaonaje kama itatenga pesa kuweza kuzisaidia hizi Halmashauri kuweza kutekeleza ahadi hizo za kuweza kutenga hizo 10%?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu wa Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WA WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA): Mheshimiwa Naibu Spika, katika swalii la kwanza nikubaliane naye kwamba katika miaka miwili Halmashauri ya Nyang'hwale haikufikia malengo ambayo walikuwa wamejiwekea na kuanzia tarehe 1 Julai, 2018, kwa kuwa Bunge limepitisha sheria rasmi kuwawajibisha maafisa masuhuri kuhusu kutenga 10% wale ambapo hawatatenga 10% watakuwa wanakiuka sheria na watahusika na hatua za kiutawala na kiutumishi kwa kutoheshimu sheria kama ambavyo zipo Serikalini. Lakini napenda kufanua kwamba ile 10% ya mapato ya ndani ni ile inayokusanya sio ile inayotengwa. Unaweza ukatenga kukusanya bilioni 10 lakini

ukakusanya bilioni sita, kwa hiyo 10% ni ile sio ya bilioni sita siyo ya bilioni 10 ileweke hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu katika zile bilioni sita iliyokusanya tunatoa fedha ambazo zinatakiwa zibaki kwenye vituo vya afya na zahanati na fedha ambazo zinatakiwa zibaki shulenii. Kwa hiyo una *subtract* pale ndio unapata hiyo 10% ya kutoa mikopo ya vijana, wanawake na wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili amesema kwa sababu hazitimizi malengo katika ukusanyaji wa mapato kwamba Serikali itengete fedha, Serikali haina nia ya kutenga fedha kwa ajili hiyo. Kwa sababuhata Waziri Mkuu katika maelekezo yake na maagizo yake kwa Halmashauri, ametoa maelekezokila Halmashauri inatakiwa ikusanye kiwango cha zaidi ya 80% ya makisio yake kwenye bajeti kwa hiyo inatakiwa hawa ndugu zetu Wakurugenzi pamoja Waheshimiwa Madiwani wajitahidi kuhakiksha Halmashauri zao zinafikia malengo ambayo yamewekwa na Serikali.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana pamoja na majibu mazuri yalisema na Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge Serikali yetu licha ya kuwa na mfuko huo ambao ni mfuko unaotumiwa kwa kuzingatia fedha za *own source* kutoka kwenye Halmashauri, lakini bado Serikali ina mifuko mingine ya uwezashaji wananchi kiuchumi. Kwa hiyo pale katika Halmashauri wanapoona kwamba kuna mapungufu ya makusanyo ndani na bado kuna vikundi ambayo vingeweza kupewa mikopo na vikafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, wawe wanawasiliana na ofisi zetu hasa Ofisi ya Waziri ambayo ndio inashughulikia masuala uwezeshaji wa wananchi kuichumi, kwa hiyo Waheshimiwa

Wabunge tunaweza tukajipanga na tukatatua matatizo mengi ya kuwawezesha vijana, akina mama na wananchi kwa ujumla kwenye suala uwezeshaji wa wananchi kiuchumi. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Badwel swali la nyongeza

MHE. OMARY A. BADWEL: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa katika Bunge liliopita la bajeti, Bunge hili lilitidhia uondoaji wa riba ama kuondoa riba asilimia 100 au kubaki 2% katika mikopo ya vijana katika Halmashauri zetu, lakini hadi sasa hakuna maelekezo yoyote yaliyotolewa katika Halmashauri zetu na vikundi vile bado vinaendelea kutozwa riba ile ile ambayo illikuwepo siku za nyuma.

Je, Serikali ni lini sasa itapeleka maelekezo rasmi kwa Halmashauri ili riba hiyo iwaze kuondoka?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu wa Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WA WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA): Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuanza utekelezaji wa sheria iliyopitishwa mwezi wa sita na Bunge lako tukufu, kulikuwa na *arrangement* ya riba na wale waliokopa kipindi kile wanatakiwa waendelee kutekeleza kama walivyokuwa wamekubaliana kipindi kile.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa wale ambao watakakopa tangu sheria hii ilipoanza kutumika wote watahusika na kutolipa riba kama sheria ambavyo inasema katika kifungu cha 35(2) *the fund so set aside under subsection one, shall be appropriated as loans to registered groups of women, youth and peoples with disabilities by 40%; 40% for youth and 20% for peoples with disabilities. Loans issued under this section shall not be subjected to any interest.*

NAIBU SPIKA: Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri hicho kifungu kina *retrospective effect* au hakina? Ndio swalii, wengine wataendelea kulipa riba wengine hawalipi.

NAIBU WA WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA): Mheshimiwa Naibu Spika, *horizon* ya mikopo hii ni ndani ya mwaka husika, kwa hiyo, wale ambaa walikopa mwaka jana walipaswa walipe *with interest* na wale waliokopa mwaka juzi hii sheria haijazungumza kuhusu *retrospective* kwa maana kwamba ifute riba kwa wale waliokopa mwaka jana na wale waliokopa mwaka juzi, hapana inafuta riba kwa mujibu wa sheria hii iliyotungwa. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Sawa na ahsante sana Mheshimiwa Naibu wa Waziri. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

Na. 40

Fedha Iliyotengwa Kupunguza Hewa ya Ukaa

MHE. COSATO D. CHUMI aliuliza:-

Wananchi wa Mafinga, Mufindi, Kilolo na Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini wameitikia wito wa kupanda na kuitunza miti na walitarajia kuwa pamoja na faida nyingine watanufaika na fedha zinazotengwa kwa ajili ya wanaosaidia kupunguza hewa ya ukaa (*carbon emission*).

Je, kama Taifa tumenufaika kwa kiasi gani na biashara hii ya hewa ya ukaa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu wa Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, majibu.

NAIBU WA WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano

na Mazingira, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukuchukua fursa hii kupongeza juhudii za wananchi wa Mafinga, Mufindi, Kilolo na Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na maeneo ya mengine ya nchi walioitikia wito wa kupanda na kutunza miti kwa sababu zozote zile.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kulifahamisha Bunge lako tukufu kuwa katika utaratibu wa biashara ya hewa ya ukaa hakuna fedha zinazotengwa kwa ajili ya kupanda na kutunza miti. Fedha hupatikana kwa kuandika miradi inayokubalika kati ya mkulima wa miti na kampuni za nchi zinazoendelea na zenye nia za kununua hiyo hewa ukaa. Utaratibu huu ulianzishwa wakati wa utekelezaji Itifaki ya Kyoto ambayo awamu yake ya kwanza ilikamilika mwaka 2012. Nchi zilizoendelea zikalazimika kuingia mkataba ya kibashara na nchi zinazoendelea kwa kutekeleza miradi ya upunguzaji wa gesijoto kupitia mapnago uliojulikana kama *Clean Development Mechanism (CDM)*. Hata hivyo, biashara hiyo haikuendelea kushamiri kama ilivyotarajiwa kwani soko la hewa ukaa iliishuka sana kutokana na kudorora kwa uchumi wa duniani katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania pamoja na nchi zingine za Bara la Afrika ilinuifaika kidogo sana na fursa ya biashara ya hewa ukaa ikilinganishwa na nchi kama vile China, Brazil na India. Kutokana na bei ya hewa ukaa kushuka katika kipindi cha miaka michache, Tanzania ilitekeleza miradi miwilli tu ya *CDM* ambayo ni mradi wa Dampo la Mtoni uliopo Temeke, Dar es Salaam na Mradi wa *Mwenga Hydropower* uliopo Iringa. Aidha, baadhi ya wananchi wa Mkoa wa Iringa waliopanda miti walipata fedha za hewa ukaa kupitia soko la biashara hii kupitia Kampuni ya *Green Resource*.

NAIBU SPIKA: Mhe. Cosato Chumi swalii la nyongeza.

MHE.COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napokea hizo pongezi wa niaba ya wananchi wa

Mafinga, Mufindi, Kilolo na Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kwa kuitikia wito wa kupanda miti kwa wingi pamoja na majibu haya ya Serikali nina maswali wawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, Serikali imetueleza jinsi ambavyo wananchi wanapaswa kuandika miradi ili waweze ku-access hizo fedha za *carbon emission*, sasa wananchi hao hawana uwezo huo, lakini wao uwezo walionao wameitikia wito, wamepanda miti kwa wingi, Serikali ipo tayari kuwawekea utaratibu kuititia ama vikundi au vijiji au mtu mmoja mmoja kuweza *ku-access* hizo fedha?

Swali la pili, kwa kuwa wananchi wa mikoa hii wameitikia sana kupanda miti na hawana chuo karibu cha kuweza kuwapa mafunzo na katika kuchangia mpango tumezungumza sana kuhusu elimu ya ufundi.

Je, Serikali haioni sasa ni wakati wa kufungua tawi la Chuo cha Misitu cha Olmotonyi katika Mji wa Mafinga ili kiweze kuhudumiwa maeneo ya Nyanda za Juu Kusini?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, majibu.

**NAIBU WA WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS,
MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tupo tayari kutoa utaratibu huo wa mafunzo kwa ajili ya watu ambao wamejitokeza na kwa nia ya dhati kabisa katika kuweza kutunza mazingira kwa kupanda miti ya kutosha, lakini pia napokea ushauri wake wa kufungua tawi, nakushukuru.

NAIBU SPIKA: Waheshimwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mheshimiwa Boniventura Desdery Kiswaga, Mbunge wa Magu sasa aulize swali lake.

Na. 41

Ujenzi wa Daraja la Sukuma

MHE. BONVENTURA D. KISWAGA aliuliza:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Daraja la Sukuma ambalo upembuzi yakinifu umeshakamilika na zabuni imeshatangazwa na mkandarasi ameshapatikana?

(b) Je, ni lini Serikali itapeleka fedha za kuanza ujenzi huo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
(MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** anajibu:

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Boniventura Desdery Kiswaga, Mbunge wa Magu, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Daraja la Sukuma liliopo katika barabara ya Mangu – Kabilia – Mahaha ni daraja la chuma (*bailey bridge*) na linaunganisha vijiji vya Lumeji na Ngha’aya. Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina pamoja na kuandaa nyaraka za zabuni kwa daraja hilo imekamilika Aprili, 2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2014 Wizara ilitangaza zabuni ya kumpata mkandarasi wa kujenga daraja hilo lakini zabuni zilizowasilishwa zikawa na gharama kubwa na hivyo taratibu za ununuizi hazikuweza kuendelea. Hadi sasa shilingi milioni 883.6 zimetolewa na Serikali na kupelekwa *TANROADS* kwa ajili ya mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, zabuni imetangazwa tena tarehe 12 Oktoba, 2018 na inatarajiwa kufunguliwa tarehe 12 Novemba, 2018 ili kumpata mkandarasi na gharama za ujenzi wa daraja hilo. Aidha, Serikali inaendelea kutenga fedha ambapo katika mwaka wa fedha 2018/2019 jumla ya

shillingi milioni 650 zimeidhinishwa ili kuanza utekelezaji wa mradi huo katika mwaka wa fedha 2018/2019.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kiswaga swal la nyongeza.

MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali lakini ninayo maswali ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa gharama halisi ya mradi ni zaidi ya bilioni tatu na Serikali imekuwa ikitenga fedha kidogo kidogo, je, Serikali ipo tayari kutenga fedha za kutosha kwenye bajeti ya mwaka 2019/2020 ili liweze kutengenezwa daraja hili kikamilifu?

(b) Kwa kuwa sasa dajara hili limeharibiaka kabisa, huduma za wananchi zimesimama hasa Tarafa yote ya Ndagalu hawawezi kupita kwenye daraja hilo iwe pikipiki iwe baiskeli na imefungwa, Serikali inachukua hatua gani za haraka ili kuweza kutatua tatizo hilo la kuwaka mbao haraka ili wananchi waweze kupata huduma?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu wa Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasilianomajibu,

NAIBU WA WAZIRI UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli imekuwa muda mrefu tangu usanifu wa barabara ufanyike ndio maana kwa sasa tulikuwa tumeelekeza mapito ya daraja hii yafanyike ili tuweze kuona kama kuna mabadiliko ya gharama halisi ya ujenzi wa daraja hili.

Kwa hiyo nipende kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba mara baada ya kupata gharama halisi tutazingatia katika bajeti ijayo kwamba tunapata fedha za kutosha kuweza kukamilisha ujenzi wa daraja hilo. Kwa hiyo nikutoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa Magu kwamba tulitazama eneo hili ili tuweze kupafanya maboresho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu (b) amesema kuwa huduma zimesimama kabisa. Nimfahamishe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kuna taratibu za manunuzi kwa matengenezo ya muda mfupi kuweza kuboresha eneo hili liweze kuitikia zilikuwa zinakamilishwa, kwa hiyo, naamini baada ya kikao cha Bunge hili ninaamini Mheshimiwa Mbunge na zoezi la kufanya marekebisho eneo hili ya haraka ili papitike yatakuwa yamefanyika. Kwa hiyo nikutoe wasiwasi na sisi tutaendelea kusimamia kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma wakati tunafanya harakati za kufanya ujenzi wa daraja hili ili liwe la kudumu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ezekiel Maige swalii la nyongeza

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swalii la nyongeza.

MHE: EZEKIEL MAIGE: Mheshimiwa Naibu Spika, katika ilani ya CCM tuliahidi kujenga barabara ya Kahama kwenda Geita kwa kiwango cha lami na mwaka juzi 2017/2018 zilitengwa shilingi bilioni 26 kwa ajili ujenzi wa barabara hiyo na mwaka huu tulionao 2018/2019 zimetengwa pia fedha lakini mchakato wa kuanza ujenzi unaonekana hata wananchi wakaona kwamba kazi inafanyika haujaanza.

Nilitaka tu kumwomba Mheshimiwa Waziri atusaidie kuwafahamisha wananchi wa Msalala na Geita kwamba mchakato wa kupata mkandarasi wa kujenga hiyo barabara umefikia hatua gani?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii Mheshimiwa Mbunge anayoizungumza kutoka Kahama kwenda Geita urefu wake ni kilometra 120 ambapo kilometra 61 ziko upande ambapo Mheshimiwa Mbunge anatoka kwa maana ya kutoka Kahama mjiini mpaka

mpakani mwa Geita ni kilometra 61 na ni kweli, katika mwaka huu wa fedha kuna shilingi bilioni 13 zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hii na nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Kahawa kwa ujumla, wananchi wa Msalala ni kwamba tuko kwenye hatua ya kusubiri fedha hatua za manunuzi za mwisho, na ujenzi utakuwa unaanza.

Kwa hiyo, tuombe Mungu tupate fedha ili ujenzi uweze kuanza, kwa hiyo nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge ni dhamira ya Serikali barabara hii muhimu kwamba itajengwa kiasi cha lami na harakati za ujenzi zimekwishaanza.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, na swalii la Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe, kwa niaba yake Mheshimiwa Joseph Selasini.

Na. 42

Daraja la Njia Moja la Mto Wami

MHE. JOSEPH R. SELASINI (K.n.y. MHE. FREEMAN A. MBOWE) aliuliza:-

Daraja la Njia Moja la Mto Wami liliopo kwenye barabara ya Chalinze – Segera ambalo ni kiungo muhimu kwa Mikoa ya Kaskazini na nchi jirani za Afrika zilizoko Kaskazini mwa Tanzania ni hatari kwa abiria, mizigo na hata vyombo vinavyotumia barabara hiyo.

- (a) Je, daraja hili liliijengwa mwaka gani?
- (b) Je, Serikali haioni kuwa ajali nyingi zinazotokea hapo husababishwa na wembamba wa daraja hilo?
- (c) Je, kuna mpango gani wa kupanua daraja hilo sanjari na eneo lote la barabara la mteremko?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
(MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliiano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe, Mbunge wa Hai lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Daraja la Wami lenye urefu wa mita 88.75 liliopo Mkoa wa Pwani lilijengwa mwaka 1959. Daraja hili ni kiungo muhimu kutoka Chalinze kwenda mikoa ya Ukanda wa Kaskazini mwa nchi yetu na nchi za jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa daraja hili kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya nchi yetu, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) ilitangaza zabuni ya kumpata Mhandisi Mshauri kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na kuandaa nyaraka za zabuni kwa ajili ya ujenzi wa daraja jipya la Wami na kazi hii ilikamilika mwezi Machi, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, Daraja jipya la Wami litakuwa na urefu wa mita 513.5 na upana wa mita 11.85 na litajengwa umbali wa mita 670 pembedi ya daraja la zamani upande wa kulia ukiwa unaelekeea Segera. Upana wa daraja hili umezingatia sehemu ya barabara, waenda kwa miguu pamoja na vizuizi kwa ajili ya usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) na mkandarasi *Power Construction Corporation* kutoka China walisaini mkataba wa ujenzi wa daraja hili tarehe 28 Juni, 2018 kwa gharama ya shilingi 67,779,453,717.00 na muda wa miezi 24.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa mkandarasi yupo kwenye maandalizi ya kuanza ujenzi ambapo baada ya maandalizi hayo kazi ya ujenzi wa daraja utaanza. Ujenzi huu unagharamiwa na Serikali yetu kwa asilimia 100.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Joseph Selasini swali la nyongeza.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Kwanza nichukue fursa hii kwa niaba ya wananchi wa Mikoa ya Kaskazini kuishukuru Serikali kwa kukubali kujenga upya daraja hili, baada ya shukrani hizo sasa niulize maswali mawili ya nyongeza.

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, magari makubwa yanaharibu sana barabara zetu na madaraja yetu sasa ili kulinda daraja la Wami na daraja la Ruvu, je, Serikali iko tayari kusanifu na kujenga barabara kutoka Chalinze kwenda Kisarawe kuungana na barabara ya Pugu ili malori makubwa kutoka bandarini yaweze kutumia barabara hiyo na kupunguza msongamano katika Jiji la Dar es Salaam?

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa ujenzi wa barabara ya Mkuu Tarakea daraja la Ungwasi halikujengwa, sasa kutokana na barabara hiyo kujengwa na kutumika na magari makubwa ya nchi jirani sasa daraja la Ungwasi linaonekana kutohimili uzito wa magari yanayopita pale, je, Serikali iko tayari kutembelea daraja hilo na ikiwezekana kutengeneza mpango mkakati wa namna ya kulijenga upya kukidhi mahitaji ya sasa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Joseph Selasini maarufu kama Paroko kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, hizo shukrani nazipokea kwa niaba ya Serikali na ni uungwana kwa kweli kama mtu ana *appreciate* kazi nzuri Serikali inafanya umedhishisha kwamba kweli wewe ni Paroko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu (a) amezungumza juu ya uharibifu wa barabara lakini pia amezungumza juu ya msongamano niseme tuu kwamba ziko hatua ambazo tunazichukua kuanza kuwa-*control*, kupunguza

msongamano ndio maana tunafanya mapitio ya usanifu wa barabara ukitoka Kibamba kwenda Pugu, ukitoka Kibamba kwenda Bunju lakini maeneo kutoka Mbezi kwenda Bunju pamoja na kutoka Mbezi kwenda Pugu ili kuweza kumudu kupunguza msongamano na ukizingatia kuwa sasa kuna ujenzi wa barabara njia sita kutoka Dar es Salaam kuja mpaka Kibaha ujenzi unaanza kwa ajili kupunguza msongamano katika jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuhusu uharibifu wa barabara ni muhimu kujua kwamba tunazo-*control*/ambazo zinafanya hizi barabara zetu ziweze kutokuharibiwa hii ni zoezi zima la ku-*control* uzito wa magari kwamba kubeba mizigo mikubwa na ndio maana tuna mizani ya kuhamishika, tuna mizani tunaendelea kuboresha na hatua mbalimbali ambazo tunazichukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi kama Serikali tutaendelea kusimamia kuhakikisha kwamba kunakuwa na matumizi sahihi ili barabara zetu ziweze kudumu na kuweza kutusaidia kama nchi kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuhusu eneo hili la ungwasi, mimi nimepita kwenye eneo la Rombo, nikitokea kule Lengai kuja Kamwaga nimepaona hapa lakini niseme tu kwa ujumla wake kwamba madaraja haya yanayotengenezwa kabla ya usanifu na ujenzi wa kiwango cha lami yanazingatia matazamio ya matumizi yake kwa muda mrefu. Kwa hiyo, wakati wa ujenzi wa barabara hii ya lami yale madaraja ambayo yamejengwa kipindi kilichopita yalizingatia kwamba yataendelea kutoa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nikubaliane na wewe kwamba iko haja ya kwenda kuangalia eneo hili kama kutakuwa na mahitaji ya kufanya mapitio daraja hili kwamba magari makubwa yanapita labda saa nyininge linaweza kuwa limepunguza zile sifa, sisi kama Serikali tuko tayari kwenda kuangalia na kuchukua hatua ambazo zinastahili. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kabla sijakaribisha swalii la nyongeza, niwaombe sana kwa sababu ya muda wetu na Wabunge tuko wengi, Mbunge unayepewa fursa ya kuuliza swalii la nyongeza usijenge hoja, nenda kwenye swalii moja kwa moja, ili na Wabunge wengine wapate fursa ya kuuliza swalii.

Mheshimiwa James Mbatia.

MHE. JAMES F. MBATIA: Nashukuru Mheshimiwa Naibu Spika.

Mheshimiwa Naibu Spika, daraja hili la Wami kwa kuwa ajali nyingi sana zinatokea mara kwa mara kwa wakati huu, je, mkandarasi ambaye anajenga daraja hili jipya kwa miaka miwili ijayo atazingatia kigezo cha kuweza kuzuia ajali kwenye daraja ambalo lipo sasa ili kuhakikisha ajali zinapungua kwa kiasi kikubwa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kwamba usanifu uliofanyika umezingatia uliofanyika umezingatia utaalamu na kuzingatia *nature* ya eneo, ndio maana unaona kwenye jibu la msingi kwanza nimeonesha daraja hili lilikuwa la muda mrefu 1959, lakini uone kabisa urefu wa barabara hii kutoka mita 88 hizo kwenda zaidi ya mita 500 tumezingatia kuona kwamba ile miteremko tunaweza kuwa tumei-control vizuri, lakini pia tumeonesha kwamba tutaweka zile kingo za kuzuia usalama lakini pia tumeonesha upana wa barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kwa maana hiyo, tumezingatia vilivyo kuhakikisha kwamba patakuwa salama zaidi kuliko hali ilivyo sasa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Catherine Magige, swalii la nyongeza.

MHE. CATHERINE V. MAGIGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa barabara ya Mto wa Mbu - Loliondo imeanza kwa ujenzi wa kilometra 50 kutoka Loliondo kuja Mto wa Mbu na barabara hii ina zaidi ya kilometra 200, ningependa kufahamu ni nini mkakati wa Serikali kumalizia barabara hii mapema ili kusaidia mradi wa kimkakati wa Magadi wa Engaruka Wilaya ya Monduli kukamilika mapema?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Naibu Spika, ni mkakati wa Serikali kuiunganisha Arusha na Mkoa wa Mara ndio maana kipande hiki cha kilometra 50 tumeanza, lakini pia tumefanya usanifu wa barabara kutoka Loliondo mpaka Mto wa Mbu lakini pia kuna usanifu ulifanyika kutoka Loliondo kwenda kwenye Mkoa wa Mara, na ziko hatua katika maeneo mbalimbali ukiangalia kwa upande wa Mara pia kuna kipande cha barabara kutoka Nata - Sanzate tutaendelea kukijenga kwa maana hiyo mkakati wetu ni kuunganisha Mkoa wa Arusha na Mkoa wa Mara kama ilivyo katika sera ya ujenzi. Ahsante.

MHE. NAIBU SPIKA: Ahsante sana Waheshimiwa tunaendelea na swali la Mheshimiwa Machano Othman Said, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Juma Ali Juma.

Na. 43

Fedha ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Inayoidai ATCL

MHE. ALI JUMA JUMA (K.n.y. MHE. MACHANO OTHMAN SAID) aliuliza:-

Kwa muda mrefu Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuititia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar imekuwa ikilidai

Shirika la Ndege Tanzania (*ATCL*) mamilioni ya shilingi kutokana na huduma mbalimbali ikiwemo *landing fee*.

(a) Je, ni lini *ATCL* itaanza kulipa deni hilo hasa ikizingatiwa kuwa sasa inaimairika kiuchumi?

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha ambacho *ATCL* inadaiwa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege vya Zanzibar hadi mwezi Septemba, 2017?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano napenda kujibu swali la Mheshimiwa Machano Othman Said, Mbunge kutoka Baraza la Wawakilishi lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amekuwa akihakiki hesabu na madeni mbalimbali ya taasisi za Serikali. Hivyo madeni yote ya *ATCL* ambayo inadaiwa na taasisi mbalimbali ikiwemo Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar yatalipwa mara tu uhakiki wa madai hayo unaendelea kufanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG*) utakapokamiliika.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya Ndege Tanzania (*ATCL*) inakiri kudaiwa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar kiasi cha shilingi 241,141,778.00 hadi Septemba, 2017. Deni hilo liliwasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG*) kwa ajili ya uhakiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya uhakiki kiasi cha shilingi 200,248,024.00 zilithibitishwa kama deni halali na kiasi kilichobaki cha shilingi 40,893,754.00 uhakiki wake bado unaendelea.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Juma Ali Juma swali la nyongeza.

MHE. JUMA ALI JUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naishukuru Serikali kwa majibu mazuri, lakini naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekiri kwamba inadaiwa shilingi milioni 248, je, ni lini Serikali italipa deni hili?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii, kumpongeza sana, Mheshimiwa Juma Ali Juma, kwa jinsi ambavyo ameendelea kulifatilia deni hilo kwa maslahi ya Uwanja wa Ndege wa Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoelezwa hapo mwanzo lengo la Serikali kupitia *ATCL* ni kulipa deni lote la shilingi 241,141,778.00 lakini hadi sasa hivi ninapozungumza ni kwamba ddeni lililohakikiwa na kugundulika kwamba liko sahihi ni deni la shilingi 200,248,024; kwa hiyo, tutakapojojridhisha na kiasi kilichobaki cha shilingi 48,893,754 tutapanga muda maalum wa kuweza kulilipa deni hilo badala ya kulipa nusu nusu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Masoud swali la nyongeza,

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi kuuliza suala dogo swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ripoti hizo za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anasema anataka hatua za kinidhamu zichukuliwe kwa wale wote walioliingiza Shirika la Ndege letu la Taifa kwa dola za Kimarekani milioni 41 sawa na bilioni 92 ambao waliingia mikataba mibovu ndege ilifika hapa muda wa miezi sita, ndege baadae ikaondolewa hapa

ikapelekwa Liberia, ikapelekwa Ufaransa, zikapakwa rangi lakini hadi leo hakuna hatua za kinidhamu zilizochukuliwa. Je, Serikali inasema niniju ya maelezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hatua za kuchukuliwa kwa walioliingiza Taifa hasara?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu.

MBUNGE FULANI: Waziri hayupo.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali ilizungumza hayo na sisi kama Serikali tumeunda timu kwa ajili ya kuhakiki ili tuweze kutoa majibu sahihi kwa wananchi kwa ujumla.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Amina Mollel swali la nyongeza.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya vyanzo ambavyo vingeweza kusaidia Shirika letu la Ndege kuongeza mapato na hata kulipa deni ni pamoja na jiko, jiko ambalo linatumika kwenye vyakula kuandaa vyakula na jiko hilo lina-*provide* vyakula hivyo katika ndege zote zinazotua nchini, lakini badala yake jiko hilo limekodishwa kwa wa-South Africa sijui Serikali ina mpango gani wa kulirudisha jiko hili kuwa mikononi mwao ili basi liweze kuongeza mapato kutokana na vyakula vitakavyo andaliwa na kugaiwa katika Mashirika yote ya Ndege yanayotua hapa nchini? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Naibu

Spika, ni kweli kwamba Serikali ina nia na lengo la kuhakikisha Shirika letu la Ndege linaongeza kipato na tumekuwa tukifanya mchakato mbalimbali ya kuhakikisha kwamba kipato cha Shirika letu la Ndege kinaimarika.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la jiko, lilikuwa limekodishwa kwa watu kutoka *South Africa* lakini hivi ninapoongea na wewe kuna baadhi ya maeneo ambapo tayari limekwisha rudishwa kwa umiliki wa Watanzania, na ndio maana hata ukiingia kwenye Shirika letu la Ndege chakula kinachokuwa *supplied* mle kimetengenezwa kutoka hapa hapa Tanzania na kinahudumiwa vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ni lengo la Serikali kuhakikisha kwamba Shirika letu linaendelea kujitegemea zaidi kwa kuhakikisha kwamba Watanzania nao wanakuwa *involved* katika kullimarisha.

NAIBU SPIKA:Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Haji Khatib Kai, Mbunge wa Micheweni sasa aulize swali lake.

Na. 44

Serikali Kuwasaidia Wavuvi Nchini

MHE. HAJI KHATIB KAI aliuliza:-

Tanzania ina mwambao mkubwa wa Bahari ya Hindi na pia ina Watanzania wengi ambao ni wavuvi kwenye ukanda huo.

Je, Serikali inawasaidiaje wavuvi hawa ili waweze kufanya kazi yao bila kubughudhiwa?

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Haji Khatib Kai, Mbunge wa Micheweni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli za uvuvi nchini zinaongozwa na Sera ya Uvuvi ya mwaka 2015 na kusimamiwa na Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya mwaka 2003 na kanuni zake za mwaka 2009; Sheria ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bahari Kuu na Sheria ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Na. 29 ya mwaka 1994.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria na miongozo mbalimbali katika uvuvi nchini inalenga kuhakikisha uvunaji wa raslimali za uvuvi unafanyika kwa misingi inayozingatia haki na usawa kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea kusimamia uvuvi nchini kwa mujibu wa sheria na kuhakikisha hakuna wavuvi au mtu ye yeyote anajishughulisha shughuli za uvuvi anaonewa ama kubughudhiwa ili mradi mtu huyo havunji sheria za nchi zillzopo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Haji Khatib Kai swali la nyongeza.

MHE. HAJI KHATIB KAI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Katika jibu la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri amesema Wizara itaendelea kusimamia uvuvi nchini kwa mujibu wa sheria na kuhakikisha kwamba hakuna mvuvi atakayeonewa wala kubughudhiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mara kadhaa wavuvi wetu wa maeneo ya Jasini, Moa, Tanga na maeneo ya Pemba wamekuwa wakikamatwa na askari wa Kenya (*Navy*) kwa kisingizio cha kuvua katika Bahari ya Kenya hata pale wanapokuwa katika maji ya Tanzania.

Je, Serikali inalijua hilo na imechukua hatua gani ili wavuvi wetu wawe na imani katika shughuli zao za kazi?

Mheshimiwa Naibu Spika, uonevu na bughudha wanazopipata wavuvi wetu wa Tanzania ni muendelezo wa dhuluma wanazofanyiwa na vyombo vyetu vya ulinzi vya

Tanzania kutokana na *operation* ambazo zimekuwa zikiendelea katika maziwa na hata baharini.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kuwa Wizara yako ndiyo inayosimamia *operation* hizo ni kwa nini wizara yako isiandae utaratibu wa kukutana na wavuvi kabla ya *operation* hizo kuanza kwa lengo la kuwaeleza wavuvi madhumuni na lengo halisi la *operation* hizo ili tu wavuvi hao wafahamu kwamba Serikali haina nia ya kuonea wala kuwadhlumu? Ahsante. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza namna ambavyo sisi kama Serikali tunavyowasaidia wavuvi wa Tanzania wanaokamatwa katika maeneo yanayosemwa kuwa sio maji ya Tanzania. Ni mara kadhaa ye ye mwenyewe Mheshimiwa Kai atakuwa shahidi, sisi Serikali tumekuwa tukifanya jitihada kwa kushirikiana na wenzetu wa Wizara ya Mambo ya Nje ya kuhakikisha kwamba watanzania wale wanaokamatwa katika maeneo ambayo yansemwa kuwa sio maji ya nchi yetu wanapata msaada wa kisheria na hatimaye kuweza kutolewa kwenda kufanya shughuli zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, rai yangu kwake ye ye Mheshimiwa Kai yangu kwake ye ye Mheshimiwa Kai na wavuvi wote wanaovua katika maeneo ya Moa, Jasini, Pemba na kule Shimanzi wote amba wapo ndani katika eneo letu la Tanzania wajitahidi sana kuhakikisha yakwamba kweli wanavua ndani ya maji yetu, sisi tuna eneo kubwa sana la uvuvi, watunze rasilimali zetu ili ziweze kuwafaidisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, wavuvi wetu walikuwa hawataki kutunza rasilimali zetu, wale wenzetu wa kule Kenya wametunza rasilimali zao na ndio maana samaki katika eneo la maji ya Kenya wakawa kwa wingi na ndio maana wavuvi wetu wa Tanzania wakatamani kwenda kuvua kule. Sisi kama viongozi wote ni wajibu wetu kuhakikisha kwamba tunawapa

elimu wavuvi wetu watunze mazingira yetu ili mradi wasiweze kwenda katika maji ya nchi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ni kwa nini Wizara ya Mifugo na Uvuvi haitoi elimu ama taarifa kwa wavuvi kabla ya kwenda kufanya *operation*. Sisi katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi tumekuwa tukifanya utaratibu wa kutoa taarifa, elimu na hata kufanya mikutano ya hadhara.

Mheshimiwa Waziri Luhaga Joelson Mpina na mimi mwenyewe Naibu Waziri tumefanya mikutano ya mara kwa mara, hata hapo Moa ataposema Mheshimiwa Kai mimi nimefika mara kadhaa na kuweza kwenda kuzungumza na wavuvi wa pale kuwapa elimu na kuwataadhalisha juu ya uvuvi haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe tena taarifa ya kwamba kwa kuwa tunasimamia sheria ambayo ndio tuliyooapa katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tutaendelea kusimamia sheria hii kwa maslahi mapana ya Taifa letu. Nataka niwaambie tu Waheshimiwa Wabunge wote zoezi la uvuvi haramu limeleta faida kubwa sana katika taifa letu kwa kuongeza moja usimamizi wa sheria na wavuvi wameelewa na mbili upatikanaji wa malighafi kwa ajili ya viwanda vyetu. Ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso swali la nyongeza.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ziwa Tanganyika ni miongoni mwa maeneo ambayo kumetokea oparesheni za uvuvi haramu, jambo ambalo ni sahihi lakini kumekuwa na tatizo la tozo/faini kubwa wanazotozwa wananchi hasa wale wachuuzi wadogo wadogo na wanaosafirisha wale samaki kwa kutozwa tozo kati ya shilingi 1,000,000 mpaka 20,000,000. (*Makof*)

Je, Serikali haioni kwamba inawaonea wale wananchi ambao wanatozwa faini hiyo wakati hawajaenda hata kupeleka elimu kwa wahusika. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvubi majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, nikirejea katika jibu letu la msingi kwamba elimu tunatoa na tumekuwa tukifanya hivyo wakati wote. Tozo hizi zipo kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni zinazoongoza tasnia ya uvubi.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji sasa aulize swali lake.

MHE. OMARY O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Naibu Spika, hakika swali hili limepitwa na wakati kwa kuwa sheria ilishafanyiwa marekebisho, lakini kwa faida ya wengine nimuombe tu Mheshimiwa Waziri aweze kuliweka vizuri.

Na. 45

Kuanzishwa kwa Kada ya Wakili Mkuu wa Serikali

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA aliuliza:-

Mwanasheria Mkuu wa Serikali ndiye Wakili Mkuu na Wakili namba moja kwa mujibu wa Katiba na taratibu za uendeshaji wa kesi mahakamani.

Je, Serikali haioni kuwa Kada ya Wakili Mkuu wa Serikali iliyoanzishwa sasa inakinzana na Sheria ya Uanzishaji wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri kama sheria ilishapita na tatizo limeisha labda ni kueleza kwamba sheria inasemaje kuhusu jambo aliloliuliza.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Mohamed Omar Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji kwa taarifa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Wakili Mkoo wa Serikali (*Office of Solicitor General*) imanzishwa na kupewa majukumu kisheria kuititia Hati Idhini ya Rais kwa Tangazo la Serikali Na. 50 la tarehe 13 Februari, 2018. Aidha, ofisi hiyo imetambuliwa na Sheria ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali (Utekelezaji wa Majukumu) Sura 268 kuititia Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 2 ya mwaka 2018 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendment) No. 2 Act 2018*).

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho yaliyofanyika kwenye muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali yamelenga kuiwezesha Ofisi ya Wakili Mkoo wa Serikali kutekeleza majukumu yake ya usimamizi na uendeshaji wa mashauri ya madai yakiwemo ya kikatiba ambayo Serikali ni mdaawa kwa niaba ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huo, kuanzishwa kwa Ofisi ya Wakili Mkoo wa Serikali hakukinzani na Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania na Sheria ya Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali kama ilivyofanyiwa marekebisho na Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 2 ya mwaka 2018 ambayo tayari Rais ameridhia.

NAIBU SPIKA: Nakushukuru sana.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la nyongeza.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mchengerwa una swalii la nyongeza wakati jambo limeshapitwa na wakati tena.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nyongeza ya hapo hapo marekebisho.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mchengerwa.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na marekebisho Na. 2 ya mwaka 2018 ambayo Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria ameyazungumza yameondoa mamlaka ya *prosecution* ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kesi zote za jinai, lakini katika kesi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) dhidi ya Khamis Ali Machano na wenzake 18 *Criminal Application No. 8* ya mwaka 2000 ambayo iliamuliwa na Jaji Kisanga, Jaji Ramadhan na Jaji Lugakingira, walizungumzia kanuni za msingi kuhusu mambo yale ambayo yanaweza kutokea kuhusu mambo ya uhaini. Na kwa kuwa Katiba sasa imemtaja Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuwa ye ye ndiyo muhusika wa mambo yote ya Muungano hususani ya masuala ya kesi na kwa kuwa marekebisho Na.2...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mchengerwa sasa uliza swali lako kwa sababu kwanza umeanza kwa kusema sheria imeshapitishwa swali lako limekwisha, sasa umeanza na maelezo marefu sana unanipa wasiwasi kidogo. Uliza swali lako.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: ...iwapo masuala ya kiahini yaktoketa kule Zanzibar na marekebisho haya Na. 2 yaliyozungumzwa. Je, Mkurugenzi wa Mashitaka atakuwa na mamlaka yote aliyonayo Mwanasheria Mkuu wa Serikalikama ambavyo yametamkwa katika Katiba.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria nakupa uhuru kwa sababu swali alilouliza sio sehemu ya msingi lakini kama unaona majibu unayo unaweza kuyatoa, kama huna majibu hilo ni swali ambalo lipo tofauti na swali la msingi.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mchengerwa swali hilo la nyongeza lifanye la msingi ili Mheshimiwa Waziri akajiridhishe na hiyo kesi ilichosema na hicho ulichosema wewe kama atawea kutoa hayo majibu hapo baadae.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na swali la Mheshimiwa Kabwe Ruyagwa Zitto, Mbunge wa Kigoma Mjini.

Na. 46

Mashauri Yanayoikabili Tanzania Kwenye Mahakama za Kimataifa

MHE. KABWE Z. R. ZITTO aliuliza:-

Tanzania inakabiliwa na mashauri mbalimbali kwenye Mahakama za Kimataifa kama vile ACSID, ICA London, ICC Paris na kadhalika kuhusiana na masuala ya uwekezaji na mikataba ya kibiashara.

(a) Je, kuanzia Novemba 2015 ni mashauri mangapi kwa idadi yapo kwenye mahakama zipo na jumla ya madai ya mashauri hayo yote ni kiasi gani kwa fedha kwa dola za Kimarekani?

(b) Je, kuanzia mwaka 2000 - 2018 kumekuwa na mashauri mangapi dhidi ya Jamhuri ya Muungano, mangapi yameamuliwa, mangapi bado na mangapi Tanzania ilishinda?

(c) Je, kesi iliyofunguliwa na Kampuni ya *Acacia Mining (LCIA Arbitration No. UN 173686 No. 87)* huko London Uingereza ina madai gani na kwa nini kuwe na kesi mahakamani wakati Serikali ilifanya mazungumzo na *Barrick Gold* ambao ni wamiliki wa Acacia?

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA Alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kabwe Ruyagwa Zitto, Mbunge wa Kigoma Mjini lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mashauri yaliyofunguliwa nje ya nchi dhidi ya Serikali kuanzia Novemba 2015 ni 13. Aidha, mashauri hayo yapo katika mahakama mbalimbali

za usuluhishi ikiwemo *Permanent Commission of Arbitration (PCA), London Court of International Arbitration (LCIA) na International Centre for Settlement of Investment Dispute (ICSID)* na huko Johannesburg – Afrika ya Kusini kupitia Sekretarieti ya *UNCTRAL*. Jumla ya madai katika mashauri hayo ambayo hayajathibitisa ni dola za Kimarekani 185, 580,009.76.

Mheshimiwa Naibu Spika, mashauri yote yaliyopo kwenye Mahakama za Kimataifa bado hayajatolewa uamuvi. Hivyo, takwimu halisi za madai na gharama ambazo Serikali inaweza kuwajibika kulipa itapatikana baada ya mashauri husika kukamilika na uamuvi kutolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa hakuna kesi yoyote katika Mahakama za Usuluhishi ya London iliyofunguliwa dhidi ya Serikali na Kampuni ya *Acacia Mining PLC*. Shauri Na. *LCIA Arbitration UN 173686* lilitotajwa na Shauri Na. *UN 1736867* yamefunguliwa mnamo tarehe 3 Julai, 2017 na makampuni mawili ya madini ya hapa Tanzania ya *Pangea Minerals Limited* na *Bulyanhulu Gold Mining Limited*, mtawalia. Utetezi wa Serikali kwenye kesi hizo umekwishawasilishwa mahakamani. Makampuni hayo yameendelea na mashauri hayo kwa madai ya kulinda maslahi ya wanahisa wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulijulisha Bunge lako tukufu kwamba kwa mujibu wa masharti katika mikataba ya kimataifa, kanuni na desturi zinazisimamia mashauri ya usuluhishi kimataifa inaelekeza masuala ya kesi yaliyopo kwenye vyombo vya usuluhishi ni siri mpaka pale mahakama au baraza husika la usuluhishi itakapoamua kuyaweka wazi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zitto Kabwe swalii la nyongeza.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nataka niweke *attention* kwa Mheshimiwa Waziri kwamba kipengele (b) cha kesi za kuanzia mwaka 2000

mpaka 2018 hakijajibiwa kabisa na naomba sasa niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni za *Pangea Minerals* na Bulyanhulu ni kampuni tanzu za *Acacia Mining*, kama vilevile ambavyo Serikali ilivyozungumza na Barrick kwa ajili ya makosa ya Acacia hapa nchini, ndivyo hivyo hivyo kesi za *Pangea Minerals* na Bulyanhulu huwezi kuzitofautisha na kesi za Acacia. Kwa hiyo, naomba Serikali injibiu kwa nini tushtakiwe wakati tuna mazungumzo na watu hawa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali katika taarifa yake ilioitoa kwa umma mwaka jana ilisema kwamba tumeahidiwa kishika uchumba cha dola milioni 300 takribani shilingi bilioni 700 na mpaka sasa hatujapata.

Sasa swalilangu, sasa hivi Serikali imefungua kesi dhidi ya makampuni ya Barrick na Acacia; hayo *Pangea* na Bulyanhulu kutokana na masuala yanayohusiana na *tax avoidance* jambo ambalo ndilo lilipaswa kufanywa kabla ya kadhia yote ya makinikia. Waziri anataka kuiambia Tanzania sasa Serikali imejifunza kutumia maarifa kwenye kukabiliana na changamoto mbalimbali za nchi badala ya kutumia mabavu ambayo yanatuingiza katika kesi ambazo hazina msingi wowote? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria majibu.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Naibu Spika, masuala yote aliyoyasema yale yaliyo katika mahakama za kimataifa na mahakama ya nchi ni *sub judice*, kwa hiyo, Serikali haitatamka chochote. (*Makofi*)

Nataka niwaambie katika Sheria za Kimataifa tamko lolote ambalo nitalifanya hapa likaingia kwenye *Hansard* litahatarisha hoja za Serikali katika kesi hizo. Mtego huo uwewe bahati mbaya, wa kuadhimia au wa kutumwa sitauingia kamwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mtego uwe wa bahati mbaya au wa kutumwa sitauingia kamwe. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na swali la Mheshimiwa Ussi Salim Pondeza, Mbunge wa Chumbuni.

Na. 47

Tume ya Haki ya Binadamu na Utawala Bora

MHE. USSI SALUM PONDEZA aliuliza:-

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imemaliza muda wake lakini mpaka sasa mchakato wa kupata viongozi wapya bado haujakamiliika.

(a) Je, ni nini kinachelewesha kupatikana kwa Makamishna wa Tume hiyo?

(b) Je, ni kwa nini ripoti za Tume haziwasilishwi kwa wakati katika Bunge la Jamhuri na Baraza la Wawakilishi?

(c) Je, ripoti ya mwisho ya Tume hiyo iliwasilishwa lini katika Bunge la Jamhuri ya Muungano na Baraza la Wawakilishi?

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ridhaa yako naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Chumbuni lenye vipengele (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kuwapata Makamishna unapitia hatua mbalimbali ikiwemo watu kuomba nafasi, usaili pamoja na upekuzi. Mchakato wa uteuzi unaendelea na hivyo nimwombe Mheshimiwa Mbunge avute subira pindi zoezi hilo litakapokamiliika Makamishna wa Tume watateuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua zimechukuliwa ili kuhakikisha kuwa taarifa za Tume zinawasilishwa Bungeni kwa wakati. Aidha, Tume imeshaandaa taarifa zake hadi mwaka 2015/2016 na taarifa ya mwaka 2016/2017 ipo katika hatua za mwisho za maandalizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya mwisho ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora iliwasilishwa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Baraza la Wawakilishi mwaka 2011/2012.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza swalii nyongeza.

MHE. USSI SALUM PONDEZA: Mheshimiwa Naibu Spika, asante. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa amjibu yake mazuri na kuweza kukiri lakini nilikuwa na maswali mawili madogo ya nyongeza ya kumuuliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekiri kuwa zaidi ya miaka sita tangu 2011/2012 haijawasilisha ripoti ya haki za binadamu katika Baraza la Wawakilishi wala Bunge. Je, Serikali haioni kuwa inavunja Katiba na masharti yake? (*Makofii*)

Swali la pili, Tume ya Kurekebisha Sheria ipo kwa mujibu wa sheria, Makamishna hawajateuliwa kwa muda mrefu sasa toka 2011 na 2012. Je, Serikali haioni kama kuna watu ambao wanakosa haki zao? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria majibu.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, Tume inafanya kila jitihada kuhakikisha kwamba taarifa zote zimekamilika na kuwasilishwa na vile vikwazo vyote ambavyo vilikuwa vinafanya taarifa hizo zichelewe kuwasilishwa zimekwishatatuliwa ikiwa ni pamoja na rasilimali fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uteuzi wa Makamishna, pamoja na kwamba Makamishna hawajateuliwa lakini Tume inaendelea kufanya kazi kuitia watendaji wake na kwa hiyo hakuna madhara makubwa yaliyotendeka, lakini hata hivyo hiyo haimaanishi kwamba hatua za kukamilisha mchakato wa uteuzi wa Makamishna zisiendee na zinaendelea. Katika kufanya hivyo, tarehe 21 mwezi wa kenda mwaka huu tumepitisha kanuni kuhusu utaratibu wa uteuzi wa Makamishna ili kanuni hizo zisaidie kuharakisha mchakato huo.

NAIBU SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii Mheshimiwa Mwanne Ismail Mcchemba, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 48

Kuvitangaza Vivutio vya Utalii Vilivyo Katika Mkoa wa Tabora

MHE. MWANNE I. MCHEMBA aliuliza:-

Mkoa wa Tabora una vivutio vingi vya utalii, pia una makumbusho mengi yenye historia mbalimbali.

Je, Serikali ipo tayari sasa kuvitangaza vivutio hivyo?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Mwanne Ismail Mcchemba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inavitambua vivutio na kumbukumbu muhimu za kihistoria zinazopatikana Mkoani Tabora na baadhi yake vimetangazwa katika Gazeti la Serikali. Baadhi ya vivutio viliviyotangazwa na kutambulika kisheria ni Tembe la Kwhihara la Dkt. Livingstone la mwaka 1953, eneo la Hifadhi Kwhihara (1953), Ngome ya Mirambo ya Karne ya 19 (1937) na Makaburi ya Urambo ya mwaka 1937. Aidha,

suala la uhifadhi na uendelezaji wa malikale linahusisha Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Mashirika Yasiyokuwa ya Kiserikali na Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya kutambua na kutangaza vivutio ni endelevu, hivyo, Wizara yangu itaendelea kushirikiana na Halmashauri za Wilaya katika Mkoa wa Tabora kwa lengo la kufanya utafiti, utambuzi na kutangaza maeneo hayo na kumbukumbu muhimu za kihistoria zitakazokidhi vigezo vya kuwa urithi wa utamaduni wa Taifa. Maeneo yatakayotangazwa yataendelezwa na kutumika kama vivutio vya utalii na vyanzo vya mapato kwa Halmashauri husika na Taifa letu kwa ujumla.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwanne Mchemba swalii la nyongeza.

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa vivutio Mkoa wa Tabora ni vingi, na kwa kuwa Serikali imeshavitambua naishukuru sana Serikali yangu. Naomba niviongeze vivutio vifuatavyo; kuna vivutio vya njia ya watumwa kutoka Ujiji, Kigoma kupitia Tabora ambayo ni njia nzuri sana kama kivutio; kuna maboma ya machifu ambao ni wengi sana wa Mkoa wa Tabora, lakini pia kuna jambo ambalo Serikali imelisahau, kuna *zoo* ambayo iko katikati ya Mji wa Tabora ambayo wanyama wale wanashirikiana na wananchi, je, Serikali iko tayari sasa kuitambua *zoo* ya Tabora Manispaa ili iwe mionganoni mwa vivutio vya Mkoa wa Tabora? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, kwa kuwa Serikali imekubali kwamba vivutio vya Mkoa wa Tabora viro, je, Serikali iko tayari kuboresha zile barabara ambazo zinakwenda kwenye vivutio hivyo hatimaye kupata mapato ya kutosha katika Serikali yetu?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii majibu.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa fursa hii ya kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa bibi yangu, mchumba wangu, Mwanne Ismail Mchemba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swalî lake la kwanza, ni kweli Serikali inakiri kwamba Tabora ina vivutio vingi nya kihistoria na hata nya kiasili kama hifadhi mbalimbali kama mbuga zikiwemo Mbuga za Ugala na misitu ikiwemo misitu ya Ipole, misitu ya jirani ya Inyonga na misitu ya Igombe, na vyote hivi vina hadhi ya kitaifa na kimataifa na tunavitambua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ambayo tunakusudia kuifanya katika Awamu ya Tano ni kuhakikisha vivutio hivi kwa ujumla wake vinatumika ipasavyo kiutalii na hili tunalitekeleza katika mkakati wetu wa kufungua *circuit*nyingine mpya zaidi za utalii zilizopo Magharibi na Kaskazini Magharibi mwa Tanzania lakini pia zilizopo kusini mwa Tanzania.

Kwa hiyo, uwekezaji wetu mkubwa kwa sasa utaelezewa huko ikiwemo vivutio vilivyopo katika Kanda ya Magharibi kuanzia Mkoa wa Tabora kwenda mpaka Mkoa wa Kigoma na hapa tunakusudia katika siku za usoni kuanzisha mchakato wa kufanya utafiti lakini pia kufanya *recategorization* ya Pori la Akiba la Ugala kuwa Hifadhi ya Taifa lakini pia Pori la Akiba la Moyowosi kuwa hifadhi ya Taifa na kutengeneza *categories* mpya za maeneo ya uhifadhi ili *circuit* ikamilike vizuri tukiunganisha na Hifadhi za Masito, Tongwe, Gombe pamoja na Mahale kule Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili linahusu miundombinu na hapa tunapokwenda kutekeleza mkakati wetu wa kuifungua upya *circuit* ya magharibi kiutalii maana yake ni lazima tuzungumzie kufungua miundombinu na hivyo Mheshimiwa Mwanne Ismail Mchemba asiwe na shaka kuhusu mikakati yetu, yajayo yanafurahisha.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nitampa nafasi Mbunge mmoja, lakini niwakumbushe swali hili linahusu kutangaza vivutio, maana tusije tukaanza kuuliza maswali ambayo hayana uhusiano na kutangaza.

Mheshimiwa Joseph Mbilinyi.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Naibu Spika, *you are so preemptive. (Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri amezungumzia kuanzisha *circuit* mpya sijui Magharibi na kadhalika na mara nyingi tunasikia kwamba tunataka kuanzisha hifadhi mpya na kuwahamisha wanavijiji, lakini ukweli ni kwamba bado tuna vivutio vingi sana ambavyo hatujavitangaza. Nyanda za Juu Kusini kuna vivutio vingi sana, kuna Katavi, Ruaha, Kitulo, *Lake Ngozi*, kuna Kimondo kule Mbozi na kadhalika, hata tukitaka *hiking* pia kuna *Mount Mbeya* unaweza ukaanza pale Mbeya Mjini katika ardhi ya Mbeya Mjini kufanya *hiking* kwenye *Mount Mbeya* na kuvutia watalii wengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mpango gani sasa, maana yake hiki kitu sisi Wabunge wa Nyanda za Juu Kusini tumeifuatilia muda mrefu sana kuhakikisha inakuja na mpango *credible* wa kutangaza utalii kwenye *Southern Circuit*?

NAIBU SPIKA: Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu kwa swali hilo muhimu.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la ndugu yangu, Mheshimiwa Joseph Mbilinyi *aka Sugu aka Mr. II*, Mbunge wa Mbeya Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na yeze, Ndugu Jongwe kwamba tuna vivutio vingi sana katika nchi yetu, na ninaomba hapa niweke kwenye rekodi kwamba Tanzania ni kati ya nchi chache Barani Afrika ambayo ime-

sacrifice asilimia 32.5 ya ardhi yake na kuifanya kuwa maeneo yaliyohifadhiwa, na katika maeneo hayo asilimia 25 ni hifadhi zenyé hadhi mbalimbali za wanyamapori. Kwa msingi huo nakubaliana na yeye kwamba tuna vivutio vingi sana katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kutangaza ni jambo moja na kutangaza inategemea eneo wakati linatangazwa rasmi na Serikali kama ni kivutio cha utalii na kama ni eneo la hifadhi lilikuwa lina lengo gani, maeneo haya yana malengo mbalimbali, siyo kila maeneo tutayatumia kwa ajili ya utalii. Lakini mikakati ya kutangaza ipo na watalii wanayatumia maeneo haya na yanaingiza kwa kiasi kikubwa sana pato la kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya utalii ndiyo inayoongoza kwa kuingiza fedha za kigeni hapa nchini na hiyo inatosha kuwa ushahidi kwamba kazi ya kutangaza, lakini pia kutumia vivutio vyetu kibashara inafanyika ipasavyo. Na ili kumpa taarifa Mheshimiwa Mbunge, Waheshimiwa Wabunge wenzangu watu wa kusini na Watanzania wote kwa ujumla, napenda niwathibitishie kwamba *corridor* ama *circuit* ya Kusini ni katika *circuit* ambazo zimepewa kipaumbele cha juu sana na Serikali ya Awamu ya Tano kuititia utekelezaji wa Mradi wa ReGROWambao unakusudia kuifungua *circuit* hiyo kiutalii kwa kufanya shughuli za utangazaji kwa kasi kubwa zaidi kwa kujenga miundombinu ya kisasa zaidi, kwa kujenga barabara za hifadhi lakini pia viwanja vya ndege vya kisasa, lakini pia kuunganisha hiyo *circuit* ya Kusini pamoja na *circuit* ya Magharibi na *circuit* ya Kaskazini.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Wabunge wengi wameomba kuzungumza kuhusu kutangaza vivutio vilivyoko kwenye maeneo yao. Kwa sababu hawawezi kupata wote fursa ya kuzungumza hapa, naomba Wizara ule mpango wake wa kutangaza hivi vivutio mbalimbali, hawa Wabunge ama wauone huo mpango au kama siyo mpango basi wayaone matangazo yanayohusu maeneo yao kwa sababu Wabunge wengi wameomba kuchangia hapa. Kwa

hiyo ni vizuri kama Wizara mkatayarisha hayo matangazo ili na yenyewe wawe wanayaona ili wajue maeneo yao yanatangazwa. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji; Mheshimiwa Maria Ndila Kangoye, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 49

Serikali Kuboresha Huduma ya Maji Vijijini na Mijini

MHE. MARIA N. KANGOYE aliuliza:-

Serikali katika Ilani ya Uchaguzi iliahidi kuboresha huduma ya maji kwa vijiji kutoka asilimia 67.7 kwa mwaka 2015 hadi asilimia 85 kwa mwaka 2020 na kwa upande wa mijini asilimia 68 kwa mwaka 2015 hadi asilimia 95 kwa mwaka 2020.

(a) Je, ni nini mkakati wa Serikali katika kutekeleza azma hii ambayo pia itasaidia kumtua mwanamke ndoo kichwani?

(b) Je, ni lini Bwawa la Kidunda litajengwa ili kuboresha huduma ya maji katika Jiji la Dar es Salaam?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maria Ndila Kangoye, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufikia azma ya Serikali ya kupata huduma ya maji safi na salama wananchi wa vijijini kwa asilimia 85 na asilimia 95 kwa wananchi waishio mijini ifikapo 2020, kwa upande wa vijijini Serikali imeendelea na utekelezaji wa Programu Ndogo ya Huduma ya Maji Vijijini na Usafi wa Mazingira ambapo hadi kufikia mwezi Septemba,

2018, jumla ya miradi 1,595 imekamilika. Serikali inaendelea kukamilisha miradi inayoendelea, kupanua miradi iliyopo na kuanzisha miradi mipyä ili kufikia lengo lake la kuwapatia huduma wananchi wa vijijini. Aidha, kwa upande wa mijini Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maji inayohusu ujenzi na ukarabati katika miji mikuu ya mkoa, miji mikuu ya wilaya na miji midogo pamoja na mirdai ya kitaifa ambapo miradi yote ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, maandalizi ya ujenzi wa Bwawa la Kidunda ambalo litasaidia kuboresha huduma ya maji katika Jiji la Dar es Salaam yamekamilika ikiwa ni pamoja na usanifu, nyaraka za zabuni, michoro pamoja na ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaopisha ujenzi wa bwawa hilo. Serikali inaendelea kutafuta fedha kutoka kwa wadau mbalimbali wa maendeleo kwa ajili ya ujenzi wa bwawa hilo linalokadiriba kufikia shilingi bilioni 470.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Maria Kangoye swalii la nyongeza.

MHE. MARIA N. KANGOYE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Katika Wilaya ya Kwimba kuna visima takribani zaidi ya 188 ambavyo ni vibovu na havitoi maji licha ya Mheshimiwa Ndassa kuhangaika kila leo, pia katika Wilaya ya Illemela vipo visima nane, kimoja kimekamilika, vinne vinasuasua, vitatu mkandarasi amesimama kabisa na visima vya namna hii vipo karibu katika kila Wilaya ya Mkoa wa Mwanza, je, ni nini kauli ya Serikali juu ya suala hili la visima hivi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, itakumbukwa kwamba Mheshimiwa Kitwanga aliwahi kusimama ndani ya Bunge hili na kutishia kuzima mitambo ya maji kule lhelele kwenye chanzo cha maji yanayokwenda Shinyanga na Kahama kwa sababu wananchi wa maeneo yale hawakuwa

na maji safi na salama. Je, ni nini mkakati wa Serikali wa kusambaza maji masafi kutoka Ziwa Victoria kwa wananchi wa Vijiji vya Mkoa wa Mwanza? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, ni mionganini mwa Wabunge shupavu na mahiri katika kuhakikisha wanawatetea wananchi wao katika Mkoa wa Mwanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Wizara yetu ya Maji inatambua kabisa eneo la Kwimba pamoja na Sumve ni moja ya maeneo yenye ukame mkubwa sana katika suala zima la maji. Sasa sisi kama Serikali tumekuwa na jitihada ya uchimbaji wa visima lakini visima vile vimekuwa vikikaa kwa muda mfupi kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mkakati wa Wizara yetu ya Maji tunaona namna gani ya kutumia maji ya Ziwa Victoria ambacho ni chanzo cha uhakika katika kuhakikisha tunaondoa tatizo la maji. Nataka nimhakikishie mzee wangu, Mheshimiwa Ndassa, kwa kuwa sisi ni Wizara ya Maji siyo Wizara ya ukame, tutahakikisha tunawapelekea wananchi wake maji katika kuhakikisha tunakamilisha azma ya Mheshimiwa Rais. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili, amezungumzia suala la maji kwa Mheshimiwa Kitwanga, sisi kama Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Uwekezaji ya Ulaya pamoja na Shirika la Maendeleo la Ufaransa tunatekeleza mradi wa *EIRO* milioni 114.5 katika Miji ya Magu, Misungwi pamoja na Lamadi katika kuhakikisha tunatatua tatizo la maji. Na katika Mji wa Misungwi tuna kazi ya kutengeneza mifumo ya kutibu maji kwa maana yawe maji safi na salama lakini pia kutengeneza matenki makubwa kwa ajili ya usambazaji. Nataka kumhakikisha Mheshimiwa Kitwanga, hana sababu ya kuzima mitambo, mradi ule utakapokamilika utawezesha

wananchi zaidi ya 23,000 katika kuhakikisha tunatatua tatizo la maji. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwenda, tunaendelea na Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Flatei Massay.

Na. 50

Ahadi ya Ujenzi wa Bwawa la Maji Dongobesh

MHE. FLATEI G. MASSAY (K.n.y. MHE. MARTHA J. UMBULLA) aliuliza:-

Wakati wa ziara ya kampeni ya Mheshimiwa Rais katika Jimbo la Mbulu Vijijiini aliahidi ujenzi wa Bwawa la Maji la Dongobesh akiingia ikulu.

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Bwawa la Maji la Dongobesh katika Jimbo la Mbulu Vijijiini ili kuondoa adha na kero kubwa ya maji wanayoipata pamoja na mifugo yao?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Awamu ya Kwanza ya utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (*WSDP/I*) Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu ilipanga kutekeleza miradi ya maji 11 ambayo ni Haydom, Singu, Endamasak, Maretadu Chini, Dongobesh, Arri-Harsha-Bashay, Moringa, Masieda, Endanyawish, Eshkesh na Mongahay-Tumati. Kati ya miradi hiyo, miradi ya maji sita imekamilika katika Vijiji vya Singu, Endamasak, Maretadu Chini, Dongobesh, Moringa na Masieda na miradi ya maji mitatu ya Haydom, Arri-Harsha-Bashay na Mongahay-Tumati inaendelea na utekelezaji wa

miradi na miradi miwili ya Endanyawish na Eshkesh imepanga kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa miradi ya Haydom, Arri-Harsha-Bashay na Mongahay-Tumati upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji na inatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2019 ambapo utekelezaji wa Mradi wa Maji wa Haydom umefikia asilimia 97 na unatoa huduma kwa wananchi. Mradi wa Maji Arri-Harsha-Bashay umefikia asilimia 50 na Mongahay-Tumati umefikia asilimia 47 na utekelezaji wa miradi iliyobaki utafanyika katika Awamu ya Pili ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (*WSDP II*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Bwawa la Maji la Dongobesh limekusudiwa kutumika kwa ajili ya mifugo na killimo cha umwagiliaji na linasimamiwa na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Flatei Massay swali la nyongeza.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kama kijana mwenzangu amefika kwenye jimbo langu na kupita vijiji vyote hivi vya Labai lakini sasa kuna miradi hii ambayo ameisema mwenyewe ameiona kwa macho; Mradi wa Mongahay, Mradi wa Tumati, Arri-Harsha, lakini na anajua kwamba tumewapa *DDCA Visima* vya Labai, Endagichang, Gendaa, Maretadu, Ng'orat na ye ye mwenyewe amefika Haydom na ameahidi kisima, je – aji-commit leo miradi hii inaisha lini na kile kisima cha maji anasemaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili...

NAIBU SPIKA: Sasa hapo mbona umeuliza mawili tayari Mheshimiwa? Umechanganya yote mawili katika swali moja, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, napenda kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuwatetea wananchi wake katika Jimbo la Mbulu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikubaliane kabisa na Mheshimiwa Mbunge baada ya ombi lake la kwenda kutembelea katika Jimbo la Mbulu nimefika pale, kiukweli kuna hali ya upatikanaji wa maji kumekuwa na changamoto; moja, kuna miradi ambayo ni kiporo, sasa sisi kama Wizara ya Maji tumeomba wataalam sasa wa Wilaya ya Mbulu kuja katika Wizara yetu ya Maji tuweze kushirikiana na wataalam wetu katika kuhakikisha Wizara tunawapa nguvu ili miradi hiyo iweze kukamilika na wananchi wake waweze kupata maji safi, salama na yenye kuwatoshleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuhusu Mradi wa Haydom, tunaonya Mji wa Haydom, pamoja na utekelezaji wa mradi wa maji, lakini kumekuwa na ongezeko kubwa la watu, sasa kuna haja ya uchimbaji wa kisima. Sasa sisi kama Wizara ya Maji tumeona haja ya kuwapa kiasi cha shilingi milioni 60 katika kuhakikisha kisima kile kinachimbwa kikubwa Kirefu katika kuhakikisha kinaongeza uwezo ili mradi ule uweze kutoa huduma kwa wananchi wa Haydom.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri hebu watazame Wabunge waliosimama, waangalie vizuri umemuona Mama Nagu, akina mama wamesimama wengi kweli hapa na akina baba. Kwa hiyo tafadhalii hii Wizara ambayo..., Mheshimiwa Naibu Waziri naomba uwatazame hao Wabunge waliosimama kwa sababu ya muda wetu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI KILIMO (MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA): Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Lakini na mimi naomba nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji kwa majibu yake mazuri sana, na vilevile swali hili la Manyara ambalo linahusu masuala yote ya mabwawa ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa wiki chache zilizopita Tume ya Umwagiliaji ilihamia Wizara ya Kilimo na sisi kama Serikali tumepanga shilingi milioni 44 katika hili Bwawa la Maji la Dongobesh na hii iko katika mwaka wa fedha ule wa 2018/2019. (*Makofii*)

Kwa hiyo naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge swali lake hili litajibowi na hizi fedha tutaweza kuzipeleka katika Bwawa la Maji la Dongobesh pamoja na Waheshimiwa Wabunge mbalimbali ambao masuala yao yanahuksika katika mabwawa ya maji, ahsante. (*Makofii*)

NAISBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea Mheshimiwa Upendo Furaha Peneza, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Cecilia Paresso.

Na. 51

Matatizo Makubwa ya Maji-Wilaya ya Geita

MHE.CECILIA D. PARESSO (K.n.y. MHE. UPENDO F. PENEZA) aliuliza:-

Wilaya ya Geita inakabiliana na changamoto kubwa ya uhaba wa maji.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha upatikanaji wa maji ya kutosha kwa wananchi?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika,kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji naomba kujibu kujibu swali la Mheshimiwa Upendo Furaha Peneza, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha upatikanaji wa maji ya kutosha kwa wananchi wa Wilaya ya Geita, Serikali inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali katika

Halmashauri ya Wilaya ya Geita ikiwemo ujenzi wa mradi wa maji wa Chankorongo katika vijiji vya Chigunga, Chikobe, Kabugozo na Chankorongo. Mradi huo unatarajia kuhudumia wananchi wapatao 23,000, Pia kukarabati Mradi wa Maji wa Katoro ambapo kazi zitakazofanyika ni pamoja na ukarabati wa mabomba na vituo vya kuchotea maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika kuhakikisha wananchi wa Geita wanapata maji ya kutosha, Serikali kuititia halmashauri ya Geita ina mkakati mbalimbali ikiwemo kujenga miradi ya maji katika vijiji vya Nyamboge na Nyakagwe ambayo inatarajiwani kuhudumiwa wananchi 8,662 na kujenga mradi mkubwa wa maji katika eneo la Mamlaka ya Mji Mdogo wa Katoro ambapo upembuzi yakini na usanifu wa mradi huo umekamilika. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo unaotarajia kuhudumia wananchi wapatao 114,151.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Cecilia Paresto swali la nyongeza.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Tarafa za Kasamwa, Ihanimo na Nyakungu Wilayani Geita hakuna huduma za maji kutokana na mradi uliopo unasuasua na Serikali kutokutoa fedha. Je, ni lini fedha hizo zitatolewa ili wananchi hao waweze kupata maji safi na salama?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili miradi mingi ya maji hapa nchini si endelevu kwa sababu ya wakandarasi wengi kujenga chini ya viwango. Je, Serikali mnalitambua hili na mnachukua hatua gani ili jambo hili lisijirudie na miradi yetu ya maji iwe endelevu?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitumie nafasi hii kushukuru kwa maswali mazuri, lakini kubwa sisi kama Wizara ya Maji katika Bunge la bajeti katika Wilaya ya Geita tulitenga kiasi cha shilingi bilioni 1.261. Sasa hizi ni fedha kwa ajili ya kwenda kutatua tatizo la maji. Nimtaké Mhandisi wa Wilaya ya Geita asilale, atumie fedha hizi katika kukarabati na kujenga miradi mipyä katika kuhakikisha tunatatua tatizo la maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala zima la wakandarasi ambao wanaotekeleza miradi na kuweza kusuasua. Hili ni changamoto kubwa sana na sisi kama viongozi wa Wizara ya Maji tumeona haja sasa ya kutengeneza mfumo wa kuhakikisha kwamba tunawabana wakandarasi hawa tupate wenyewe uwezo ili kuhakikisha kwamba miradi yetu inakuwa na ubora na ndiyo maana sasa tunataka kuanzisha Wakala wa Maji Vijijini. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge litakapokuja hili Bungeni lisikae katika kuhakikisha tunaenda kusimamia miradi na wananchi wawze maji ya uhakika na usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuniomba niangalie Wabunge waliosimama katika Bunge la Jamhuri ya Muungano ni wengi na hii ni kutokana maji ni uhai ningeshangaa kama Wabunge wasingesimama kutetea uhai wa wananchi wao. Na sisi kama viongozi wa Wizara Maji tutahakikisha tunawapelekea maji, ahsanteni sana. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Mary Nagu.

MHE. DKT. MARY M. NAGU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Mheshimiwa Naibu Waziri alitembelea Wilaya ya Hanang nampongeza naaliona tatizo kubwa la maji kwa sababu sehemu kubwa ya Hanang iko kwenye bonde la ufa na mpaka watu wanachota maji kwenye mapango. Je, anasemaje kuhusu visima ambavyo vimechimbwa lakini haviendelezwi, naomba nisikie atakavosema kwa sababu anajua shida ya maji ya watu wa Hanang? Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kiukweli mama yangu mama Mary Nagu anafanya kazi kubwa sana katika Jimbo leke. Lakini kikubwa mimi kama Naibu Waziri nillifanya ziara katika Jimbo lake tumeona hali ya upatikanaji wa maji, lakini changamoto kubwa sana kutokana na wananchi wake wapo katika Bonde la Ufa. Sasa sisi kuangalia namna gani tunaweza tukawasaidia tumeomba watu wale wa rasilimali za maji. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wamekwishafika katika Jimbo lako na wamefanya ni namna gani wanaweza kupata maji na sisi kama Wizara ya Maji kupitia *DDCA* tutaa ngalia namna ya kukuchimbia visima haraka ili wananchi wako waweze kupata maji safi, salama na yenye kuwatoshleza,

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, swali la nyongeza.

MHE. ANNE K. MALECELA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwa kuwa Serikali inajitahidi sana kupeleka miradi ya kupunguza mamatizo ya maji vijijini na hasa kupitia wafadhili. Lakini miradi hii ya Wafadhili ikikamilika kule vijijini wananchi wakiendelea kuitumia baadae miradi ile inakuфа na wananchi wanashindwa kuifufua.

Je, Serikali inaweka utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba ile miradi ya wafadhili inaendelea kuwa endelevu na kusaidia wananchi kama Kata ninayotoka mimi ya Kiurio mradi ule umekufa ni wa pesa nyingi sana?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge. Kiukweli sisi kama Wizara ya Maji tumeiona hiyo changamoto

kwamba tunatekeleza miradi mikubwa ya maji na tunawakabidhi wananchi katika kuisimamia. Lakini wamekuwa hawana taaluma ile na wakati mwingine hata baadhi ya jumuiya zile za watumiaji maji ile fedha ambazo wanazokusanya badala ya kuzipeleka benki wamekuwa wakigawana leo anapewa Mwenyekiti, kesho anapewa Katibu. Na ndiyo maana tumeona haja sasa ya kuunda Wakala wa Maji Vijiji ni huu utakuwa ni mtatuzi na kutakuwa historia kabisa ya matatizo ambayo yanayotokea kutohama na changamoto hizo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Maftaha swali la nyongeza.

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante nilikuwa naomba Naibu Waziri ama Wizara itueleze ina mkakati gani katika miji mingi ya Tanzania ambapo hakuna mfumo wa maji taka ikiwemo Manispaa ya Mtwara Mikindani. Ni lini Serikali italeta mfumo wa maji taka?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na wananchi kuhitaji maji na Serikali imekuwa ikifanya jitihada ya kuwapelekeea maji, Lakini tunatambua kabisa je, matumizi yale ya maji yamekuwa na uchafuzi mkubwa kwa maana ya maji taka. Sasa sisi kama Wizara tunamkakati wa kuunda sera na kuweka uwekezaji mkubwa sana katika kuhakikisha tunaweka katika mifumo ya maji taka na hili litatokana katika utafutaji wa fedha na wadau mbalimba kushirikiana nao katika kuhakikisha tunawekeza mifumo ya maji taka. Nataka nimhakikishie maeneo ambayo tutatekeleza miradi hiyo ya mfumo wa maji taka Wana Mtwara hatutowaacha na wala hatowatosa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Innocent Bashungwa.

MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwanza niishukuru Serikali kwa mkakati wa kuwatua ndoo kichwani akinamama wa Karagwe kuititia Mradi wa Maji wa Rwakajunju. (*Makofii*)

Je Serikali imefikia hatua gani katika utekelezaji wa huu mradi? Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze kaka yangu Bashungwa Serikali imekuwa na kimkakati katika kuhakikisha tunatatua tatizo la maji na tumekuwa na utekelezaji wa miradi mbalimba. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Bunge litakapokuwa linakwisha nafanya ziara ya Kagera na moja ya maeneo ambayo ungependa ningefika katika mradi huo katika kuhakikisha tunausukuma ili uweze kukamilika kwa wakati na wananchi wako waweze kupata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine na la msingi katika kuhakikisha tunataua tatizo la maji katika Jimbo lako. Ni moja ya miji 26 ambao kuititia fedha za India dola zaidi ya milioni 500 tunaenda kuwekeza mradi mkubwa sana katika Jimbo lako katika kuhakikisha tunamtua mwanamama ndoo kichwani.

NAIBU SPIKA: Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi sasa aulize swali lake.

Na. 52

**Malipo ya Mkandarasi Aliyejenga Vituo vya Polisi-
Mkokotoni na Madungu**

MHE. JAKU HASHIM AYOUB aliuliza:-

Tarehe 25/5/2017 Mheshimiwa Mwigulu Nchomba wakati akijibu swali Na. 274 kuhusu malipo ya mkandarasi

alijenga vituo vya polisi Mkokotoni, Unguja na Madungu, Pemba ambaye anaidai Wizara ya Mambo ya Ndani tangu mwaka 2012 alisema kuwa deni hilo limeshahakikika na Mkaguzi Mkuu wa Ndani na litalipwa mara fedha zitakapotolewa na Wizara hii imeshakiri zaidi ya mara tano kuhusu deni hilo na huu ni mwaka wa sita sasa.

(a) Je, wakati Waziri na Naibu Waziri wakijibu swalii hilo tarehe 25/5/2017 na tarehe 8/11/2017 hawakuwa na uhakika na majibu yao?

(b) Je, Waziri anaweza kukubaliana na mimi kuwa Wizara hii haiendi na kasi ya Mheshimiwa Rais ya kutaka wananchi wasionewe na haki itendeke?

(c) Je, ni lini sasa deni hilo litalipwa nani deni la kiasi gani hadi kushindikana kulipwa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, Mbunge kuititia Baraza la Wawakilishi lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua madai ya mkandarasi *M/S ALBATNA Building Contractor* ya shilingi 158,216,496.35 ambayo yanayotokana na ujenzi wa asilimia 60 wa Kituo cha Polisi Mkokotoni, Unguja na madai ya shilingi milioni 14,919,420 kuhusuana na kukamilisha kwa kazi ya ujenzi wa nyumba ya makazi ya askari Madungu, Chakechake Pemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inakiri pia kuwepo kwa madai ya shilingi 24,000,000 ya Mshauri Elekezi *M/S SAMKAY Consult Co.Ltd.* kuhusiana na ujenzi wa majengo hayo. Aidha, katika nyakati tofauti ikiwemo mwaka 2017/2018

madai haya yamekuwa katika mchakato wa ukaguzi wa ndani na nje wa madeni (*Internal and External Auditor*) pamoja na madai ya wazabuni wengine, lengo likiwa ni kujiridhisha kabla ya kufanya malipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Malipo kwa madai haya na wazabu ni wengine wote waliohusika katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya ujenzi wa Ofisi, Vituo vya Polisi na nyumba za makazi ya askari nakadhalika, katika Jeshi la Polisi yanaendelea kufanyika mara taratibu za malipo zitakapokamilika madeni haya yatamalizika kulipwa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub swalil ya nyongeza.

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kanuni za Balaza tulizopewa na tunazheshimu sana kaununi ya 63; sitaki kuitumia, naomba kunukuu maneno aliyozungumza Mheshimiwa Naibu Waziri ikiwa yeze ni Alhaji karudi Makka hivi juzi naomba ninukuu; "Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Jeshi la Polisi limetenga jumla ya shilingi 2.2 billion, kwa ajili ya kupunguza madeni ya Wakandarasi waliotekeleza miradi mbalimbali ikiwemo mradi wa ujenzi wa Kituo ch Polisi Mkokotoni ambao umetengewa jumla shilingi milioni mbili ikiwa ni sehemu ya deni ambalo analodai mkandarasi." Kilichoandikwa ni kiswahili wala siyo kihindi. (*Kicheko*)

Sasa ananiambia nini Naibu Waziri kwa kanuni hii tunadanganya humu Bungeni huyu mtu anaumwa na ameshapata maradhi Bunge hili hili chombo hichi hichi kizito, anatuambia nini sasa? Na nilichouliza mimi lini...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa maswali ya nyongeza kwa wewe mwenye swalil ya msingi ni mawili. Kwa hiyo umeshayauliza hapo mpe fursa Naibu Waziri akujibu.

Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu kwa maswali hayo.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Mheshimiwa Jaku amekuwa akiuliza swali hili na nadhani sasa hivi ni zaidi ya mara nne katika Bunge hili tukufu. Lakini nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo hili, Mbunge wa Jimbo la Tumbatu ambaye na yeYe amekuwa akilifuatilia suala hili kwa *style* yake ya kimyakimya. Nadhani kama Mheshimiwa Jaku angepata fursa ya kuweza kukaa na Mbunge wa Jimbo hili pengine leo asingeleta hili swali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na hoja yake ya msingi ni kwamba kwanza nashukuru ameipongeza Serikali kwa hatua ya kwanza ambayo ni ya msingi kufanyika. Kama mnavyojua kwamba wakati Serikali ya Awamu ya Tano inaingia badarakani kulikuwa kuna changamoto nyingi ikiwemo malipo hewa, na aina mbalimba za ubadhirifu uliokuwa unafanywa na kusababisha fedha ya wananchi kupotea na kulipwa kwa watu wasiostahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kitendo cha sisi kufanya uhakiki na kwa asilimia zaidi 98.4 ya madeni yote yaliyoko katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi yameshaanza kulipwa ikiwemo madeni...

Mheshimiwa Naibu Spika, samahani yameshahakikiwa, na yako mionganoni mwa madeni hayo ambayo yameshaanza kulipwa. Lakini Mheshimiwa Jaku lazima ufahamu kwamba madeni haya ni mengi na Serikali haiwezi ikayalipa madeni haya kwa wakati mmoja ikayamaliza. Yako madeni mengine ambayo yanaendelea mpaka sasa hivi wazabuni kutoa huduma kwa mfano madeni ya vyakula kwa wanafunzi vyuoni, madeni ya vyakula kwa farasi, mbwa na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimhakikishie kwamba Mheshimiwa Mbunge kwamba dhamira ya Serikali ni kulilipa hili deni na deni hili litalipwa. Kwa kuwa hatua ya kwanza ya uhakiki imekamilika basi awe na imani na Serikali, kwamba uhakiki huo utafanyika na sasa hivi utaratibu wa

kulipa deni hili utalipwa kuptitia Wizara ya Fdeha kuptitia Hazina.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tuliwahi kutenga 2.2 *billion* kwa ajili ya kulipa madeni mbalimbali. Lakini kama mnavyojuu kwamba si mara zote ambapo tunaweza kuweza kupata fedha zote kukamilisha kukidhi haja ya kibajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimalizie kwa kuendelea kumsihi Mheshimiwa Jaku avute subira hatua iliyofikiwa ni nzuri na deni hili pale ambapo taratibu zitakamilika litapatiwa ufumbuzi wa kudumu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu lakini pia na Ofisi ya Bunge swali moja likiulizwa mara nne humu Bungeni sidhani kama ni sawasawa. Swali likishaulizwa mara moja mambo hayo yatafutiwe ufumbuzi kwa kadri ya majibu yaliyotolewa. Kwa sababu sasa yaani maswali mengine yanakosa fursa kama swali linarudia lile lile na pia Ofisi ya Bunge mtusaidie maswali yanapokuja yale yale ambayo yalishajibiwa yatafutiwe ashauriwe Mbunge kufuatilia yale majibu yaliyotolewa kwa sababu majibu yanatolewa yaleyale kila wakati. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge tunamalizia swali la mwisho, Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi sasa aulize swali lake.

Na. 53

Ujenzi wa Kituo cha Polisi Kilindi

MHE. OMARI M. KIGUA aliuliza:-

Serikali imekuwa ikifanya jitihada kubwa ya kujenga vituo vya polisi pamoja na nyumba za askari polisi.

(a) Je, ni lini Serikali itajenga kituo kipywa na cha kisasa katika Wilaya ya Kilindi?

(b) Je, Serikali ipo tayari kutoa jengo jipya liliopo karibu na Ofisi za Halmashauri ambalo halijatumika toka liliopojengwa?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kilindi ni moja kati Wilaya mpya zilizoanzishwa hivi karibuni ambazo bado zina changamoto mbalimbali ikiwemo ya uhaba wa vituo vya polisi vyenye hadhi ya Wilaya pamoja na makazi ya askari. Aidha, Serikali inatambua mahitaji ya kuwa na vituo vya polisi vya kisasa vya Wilaya nchini ikiwemo Wilaya mpya ya Kilindi ili kutoa huduma ya kipolisi kwa wananchi wa maeneo husika kwa ufanisi zaidi. Hata hivyo, Serikali itaendelea na jitihada za kuboresha na kujenga nyumba za makazi ya askari pamoja na vituo vya polisi kwa kadri ya upatikanaji wa fedha utakavyoruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kutoa jengo liliopo karibu na Ofisi ya Halmashauri ambalo halitumiki Wizara yangu itawasiliana na mamlaka husika ili kuona uwezekanaao wa kupatiwa jengo hilo ili iweze kutumika.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua swali la nyongeza.

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri na katika majibu yake, amekiri kwamba Wilaya ya Kilindi ni mionganoni mwa Wilaya mpya ambazo zina changamoto hizi.

(a) Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kuitengetea Wilaya ya Kilindi kuwa ni mionganoni mwa Wilaya chache ambazo zitajengewa kituo cha polisi?

(b) Kwa kuwa kuona ni kujiridhisha, yuko tayari sasa kwenda Wilaya ya Kilindi ili kujionea hali halisi ya hili ambalo nimelisema hapa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali lake la kwanza, nimhakikishie kwamba tuko tayari na hiyo ndiyo mipango ya Serikali kwamba Wilaya ya Kilindi ni miongoni mwa zile Wilaya ambazo tutakapokuwa tumefanikisha mchakato wa ujenzi wa vituo nayo itahusika.

Lakini vilevile nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuendelea kuhakikisha kwamba anajitahidi sana kusimamia vyombo vya usalama vilivypo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi katika Jimbo lake. Amekuwa mara kadhaa akiulizia kwa utaratibu rasmi na usio rasmi na aliwahi vilevile kipindi cha kuniambia twende katika Jimbo lake. Nataka nimhakikishie ahadi yangu ambayo nilimpatica wakati ule naithibitisha leo kwamba tutakwenda katika Jimbo hilo la Kilindi ili tuweze kuangalia pamoja na mambo mengine tushirikiane kutatua changamoto za vyombo hivi vilivyo chini ya Wizara yetu.

NAIBU SPIKA: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mbunge wa Buhigwe sasa aulize swali lake.

Na. 54

**Shule za Sekondari Katika Jimbo la Buhigwe Kuwa na
Kidato cha Tano na Sita**

MHE. ALBERT O. NTABALIBA aliuliza:-

Je, ni lini shule za sekondari Munzese, Muyama, Buyenzi na Kinazi zitakuwa na kidato cha tano na sita kama ilivyopendekezwa?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mbunge wa Buhigwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ili shulke iweze kupata kibali cha kuanzisha mikondo ya kidato cha tano na sita inatakiwa kuwa na vyumba vya madarasa angalau vinne, mabweni mawili, maabara tatu kwa mikondo ya sayansi, vyoo vya kutosheleza watumishi na wanafunzi, jiko, bwalo, samani za kutosha, vitabu vya kiada na walimu wa masomo husika. Baada ya mmiliki kujiridhisha na kiwango cha ukamilifu wa vigezo anapaswa kutuma maombi ya kuanzisha kidato cha tano na sita Wizarani. Aidha, Serikali hutuma wadhibiti ubora wa shule kufanya ukaguyzi maalum ili kujiridhisha na kiwango cha ukamilifu wa vigezo kabla ya kutoa kibali.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa kutoka Ofisi ya Udhibiti Ubora Kanda ya Ziwa Magharibi zinabainisha upungufu wa miundombinu muhimu kwa ajili ya kuanzisha kidato cha tano na sita katika shule zilizopendekezwa. Katika shule ya Muyama hakuna mabweni, jiko, bwalo, madarasa, vyoo na samani; katika shule ya Bunyenzi hakuna mabweni, jiko, bwalo, madarasa, vyoo na samani; Munzese hakuna mabweni, jiko, bwalo, madarasa, vyoo na samani na shule ya Mkoza hakuna iliyopo kijiji cha Kinazi hakuna Mabweni, jiko, bwalo, vyoo na samani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashautri ya Wilaya ya Buhigwe inaelekezwa kuongeza kasi ya kukamilisha vigezo vya kuanzisha mikondo ya kidato cha tano na sita kwenye shule husika na Serikali haitasita kutoa kibali baada ya vigezo kuwa vimekamilika.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba swali la nyongeza.

MHE. ALBERT O. NTABALIBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu kwa majibu yake lakini ninayo amswali mawili ya nyongeza.

Kwanza ni ukweli unaojulikana kwambawatu wengi Tanzania wanaomaliza kidato cha nne karibu robo tatu wanakuwa wamefaulu lakini wanakosa nafasi ya kuingia kidato cha tano na cha sita kwahiylo ni janga la kitaifa ambalo kuingia cha tano na cha sita bado tuna tatizo vijana wetu wana-*drop* sana, lakini Halmahsuari yetu ya Buhigwe ime...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Obama naomba uulize mswali yako tafadhali.

MHE. ALBERT O. NTABALIBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Swali, kwa kuwa Wilaya tunejitahidi kuendelea na ujenzi huu na unaziba haya mapungufu. Nini msaada wa Serikali ili tuweze kwenda *faster*?

Lakini la pili, kwa kuwa baadhi ya shule tumeanza kufikia hatua nzuri, je, tutakapokuja kwenye Wizara yako utatupa msaada wa haraka?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Obama kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge kauliza kwamba kwa sababu ya changamoto Serikali itasaidia vipi kuweza kukamilisha miundombinu ambayo tayari wamejenga? Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI ni kawaida inashirikiana na wananchi kukamilisha miundombinu pale wananchi

watakapokuwa wamefikia kiwango cha maboma kwahiyo waendele kushirikiana katika Halmashauri ya Buhigwe ili shule hizo ziweze kukamilika.

Lakini kuhusu ni msaada gani wanaweza kupta kutoka kwenye Wizara ya Elimu, hata Wizara ya Elimu kwa nyakati fulani fulani na kwa mahitaji maalum, tunaweza kusaidia katika ujenzi wa miundombinu, kwa hiyo, vilevile wanaweza kuwasiliana na sisi tuna mpango ule wa kulipa kulingana na matokeo (*EP4R*) tunaweza tukasaidia na tumesaidia kwenye baadhi ya shule. Kwa hiyo, asisite kuwasiliana na sisi, lakini jukumu la kukamilisha miundombinu bado linabebwa na wananchi wenyewe kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na sasa nitaleta kwenu matangazo kabla hatujaendelea na ratiba iliyio mbele yetu.

Kwanza ni wageni wa Mheshimiwa Spika ambaao wako kwenye Jukwaa la Spika, wa kwanza ni Mheshimiwa Hamdi Abuu Ali ambaye ni Balozi wa Palestine nchini akiambatana na maafisa wawili. Mheshimiwa Balozi ameambatana na maafisa wawili kutoka Wizara ya Mmabo ya Nje ambaao ni Bwana Ayoub Mndeme, Mkurugenzi Msaidizi na Bi. Kisa Doris ambaye ni Afisa wa Mambo ya Nje, karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge mgeni mwingine wa Mheshimiwa Spika ni Ndugu Heri James ambaye ni Mwenyekiti wa UVCCM-Taifa. Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge kwa heshima mliyompa *Comrade* Heri James. Karibu sana *comrade* Bungeni. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, yapo matangazo ya wageni wengine na nianze na wageni mahususi kabisa siku ya leo na hawa ni wageni wa Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe kutokea Kyela. Hii ni timu ya wachezaji wanaocheza daraja la kwanza kutoka Wilayani Kyela wakiongozwa na mchezaji mkongwe, Ndugu Gaudence

Mwaikimba. Waheshimiwa Wabunge hii timu inaitwa *Boma FC*. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wengine mahususi kabisa ni wageni 42 wa Mheshimiwa Anthony Mavunde, nao hawa ni timu ya mpira, wao timu yao inaitwa *Dodoma FC*, Hawa wanaongozwa na Ndugu Ibrahim Abdallah. Karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, labda taarifa za ziada kuhusu wageni hawa mahususi ni kwamba kesho watakuwa wanamenyana pale Jamhuri stadium kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mnakaribishwa kwenda kuangalia timu Mwakyembe na timu Mavunde. Watu itabidi tugawanyike hapo lakini niwakumbushe pia muende na maji uwanjani ku-support timu zenu, mwende na maji itazisaidia timu zetu. Karibuni sana wachezaji wetu, tunaamini kwamba timu yetu ya Taifa na Mheshimiwa Mwakyembe utakuwepo pale watapata wachezaji kutoka kwenye hizi timu. (*Makofi/ Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, wageni wengine ni wageni 52 wa Mheshimiwa Stella Ikupa ambae ni Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Watu Wenye Ulemavu na hawa ni akina mama kutoka Asasi ya Mabinti wa Maria Immaculate ya Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Theopista Mwalyangu. Karibuni sana akina mama, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni wa Mheshimiwa Jumaa Aweso ambaao ni Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji ambaao ni shangazi yake Ndugu Mtanga Aweso na kaka yake Ndugu Zuberi Nyundo kutoka Pangani Mkoani Tanga. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunae pia mgeni wa Mheshimiwa Yahaya Massare ambaye ni mpiga kura wake kutoka Itigi Mkoani Singida na huyu ni Ndugu Gasper Paulo Sakalani. Karibu sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni name wa Mheshimiwa Flatei Massay ambaao ni wajasiriamali kutoka Mbulu Mkoani Manyara

wakiongozwa na Mwenyekiti, Ndugu Catherine Isaac. Karibuni sana akina mama kutoka Manyara. (*Makofi*)

Tunae mgeni wa Mheshimiwa Jasson Rweikiza ambaye ni Mjumbe wa Kamati ya siasa ya Mkoa wa Kagera na huyu ni Ndugu Christopher Kilaja. Karibu sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni wanne wa Mheshimiwa Allan Kiula ambao ni familia yake kutoka Mkoani Singida wakiongozwa na mke wake Ndugu Iness Kiula. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni wanne wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ambao ni rafiki zake kutoka Mkoani Mbeya wakiongozwa na Mheshimiwa Diwani wa Mbarali, Mheshimiwa Dira Funika. Karibuni sana. (*Makofi*)

Nimeletewa tangazo hapa tena la mgeni mwingine, mgeni mahususi kabisa huyu, huyu ni mgeni wa Mheshimiwa..., naona anajaribu kuwatisha *Boma FC* huyu. Mgeni wa Mheshimiwa Anthony Mavunde, kocha wa *Dodoma FC*, Ndugu Jamhuri Kihwelu. Mheshimiwa Mavunde usiwatishe *Boma FC* wanae Mwaikimba kule. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine la wageni, ni wageni nane ambao ni wakazi wa Michese, Jijini Dodoma waliotembelea Bunge kwa ajili ya kujifunza namna Bunge linavyoendesha shughuli zake wakiongozwa na Ndugu Rebecca Jikolo. Karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge tunayo matanganzo mengine ya kazi, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Bajeti, Mheshimiwa George Simbachawene anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa leo Kamati ya Bajeti itakutana na wadau ili kupokea maoni kuhusu Muswada wa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha wa mwaka 2018 yaani *The Microfinance Act 2018*. Kwa kuwa muswada huu unagusa wadau wengi wanaojihusisha na sekta hii ya huduma ndogo za fedha, Kamati inawaalika Wabunge kuhudhuria kwenye kikao hicho na kikao hicho kitafanyika Ukumbi wa Msekwa

mkubwa kuanzia saa 7:00 mchana. Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa. (*Makofi*)

Lakini pia Waheshimiwa Wabunge mnatangaziwa matangazo yafuatayo kutoka kwenye Ofisi ya Katibu wa Bunge; kwanza, hafla ama *cocktail party* ya *NMB* iliyokuwa imepangwa kufanyika leo Ijumaa hapa Bungeni imeahirishwa hadi hapo itakapotangazwa tena.

Pili, semina ya Wabunge wote iliyokuwa ifanyike kesho Jumamosi tarehe 10 Novemba, 2018 kuhusu masuala ya afya kwa uratibu wa Kampuni ya Bima ya *Resolution*imeahirishwa mpaka hapo baadae.

Waheshimiwa Wabunge, tatu, waliojiandikisha kushiriki kwenye mbio za *Dodoma Marathon* kesho Jumamosi tarehe 10 Novemba, 2018 mnakumbushwa kuwa mbio hizo zitaanza katika Uwanja wa Jamhuri saa 12:30 asubuhi hivyo mnaombwa kuzingatia muda.

Kuna Waheshimiwa Wabunge walikuwa wanauliza timu ya *Boma FC* na *Dodoma FC* wanacheza mpira saa ngapi? Ni kesho jioni saa 10:00.

Tangazo lingine linatoka kwa Mheshimiwa Jasson Rweikiza ambaye ni Katibu wa Wabunge wote wa CCM, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wa CCM kuwa leo saa 8:00 mchana kutakuwa na kikao pale *White House*, wote tuhudhurie bila kukosa.

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo matngazo tuliyokuwa nayo leo kwa hiyo, tutaendelea na ratiba iliyoko mbele yetu.

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo, mwongozo, mwongozo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jaku naomba ukae.

MHE. JAKU H. AYOUB: Naam.

NAIBU SPIKA: Naomba ukae.

MHE. JAKU H. AYOUB: *Hewallah Mama.*

NAIBU SPIKA: Katibu.

NDG. HUSSEIN ATHUMANI-KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

**Mpango wa Maendeleo wa Taifa Unaokusudiwa
Kutekelezwa na Serikali pamoja na Muongozo wa
Kuandaa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa
Mwaka wa Fedha 2019/2020**

(Majadiliano Yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Katibu.

NDG. HUSSEIN ATHUMANI - KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MIPANGO

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na kuchangia, nimeletewa majina hapa kama ulivyo utaratibu wetu na vyama mbalimbali. Tutaanza na Mheshimiwa Najma Giga atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mheshimiwa Khatib Said Haji ajandae.

MHE. NAJMA MURTAZA GIGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii kuwa mchangiaji wa mwanzo kwa siku ya leo katika kuboresha Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuwa hai na wazima hadi leo na afya njema tukaweza kuendelea na majukumu yetu, kwa hiyo naomba nianze moja kwa moja kuboresha mpango

wetu huu ambao umeletwa mbele yetu katika eneo la uwezeshaji wanawake kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili ni muhimu sana na ndiyo maana nimelitenga kwa upekee wake niweze kulichangia kwa siku ya leo. Pamoja na kuipongeza sana Serikali kwa mkakati ambao unafanywa katika kuongeza juhudzi za kuwawezesha Wanawake kiuchumi katika maeneo mbalimbali hasa kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu mimi naomba nielekee kwene maeneo hayo ambayo yanashughulikiwa hasa na Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la mpango wa *TASAF*, najua nia ya Serikali ni njema hapa lakini niseme tu kwamba mpango huu unawanufaisha wale wanawake ambao wako mfuko tu na pia hao wanawake ambao wako kwene mfuko huu wa *TASAF* au mpango huu wa *TASAF* wananaufaika kwa kiasi gani hilo hatujui, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri labda pengine ukija utueleze namna gani wanawake ambao wako kwene mpango huu wa *TASAF* wananaufaika kwa kiasi gani, lakini ambao awamo kwene mpango huu hawana manufaa yoyote wanayoyapata kwa hiyo bado mpango huu haujawafikia wanawake kwa namna ambavyo inastahiki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tuna Benki ya Wanawake ambayo imeunganishwa sasa na *TPB* na kufunguliwa dirisha maalum kwa ajili ya wanawake, mimi nashauri sana Mheshimiwa Waziri dirisha hili likusudiwe kwa lengo lillokusudiwa yaani lifanyiwe kwa kazi kwa lengo lillokusudiwa ikiwa ni dirisha la wanawake liwe ni la wanawake tu na kisingiie kitu kingine chochote na isiwe kwavikundi ianzie *from individuals to the group* ili mwanamke wa kitanzania afaidike na hii benki ambayo imewekwa kupitia *TPB* au dirisha hili la wanawake ambalo limewekwa kupitia *TPB*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tukija kwene mpango mwengine ambao umeanzishwa na Serikali ni uanzishwaji wa jukwaa la kuwawezesha wanawake kiuchumi nawapongeza

sana dhamira ni njema lakini hatujui bado jukwaa hili kwa kiasi gani litawenza kuwafikia wanawake wote Tanzania na kuweza kuwezesha ili tuone uchumi wetu unazidi kupaa kwa kasi kabisa. Kama amabvyo nimesema benki ya *TPB* ambayo tuna dirisha ya wanawake bado kuna umuhimu wa kuonyesha kwamba benki hii itawafikiaje wananchi wanaoishi vijjini kwa sababu lengo si kuwasaidia wanawake walioko mijini tu uvezeshaji wa wanawakekiuchumi ni kwa watanzania wanawake wote. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tukija kwenye suala la asilimia nne ya vijana; asilimia nne ya akina mama na asilimia mbili inayoenda kwa watu wenyewe ulemavu katika Halmashauri zetu hii bado ni changamoto kwa sababu ile asilimi nne inaenda kwenye vikundi maalum, kwa hiyo hitaji la mwanamke kama mwanamke na familia yake bado hajafikiwa kwa lengo lillokusudiwa, watapata mahitaji kwa kiasi cha chini, mahitaji madogo kama ya chakula kwa hiyo si mbaya lakini tuzidi kuiboresha. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nilikuwa nataka njue hii asilimia mbili ambayo inaenda kwa wenzetu wenyewe ulemavu hawa hawana makundi, lakini kuna walemauvu wenyewe ngozi na waliokuwa hawaoni, kuna ambaao walemauvu wa masikio, wako kila aina sasa sijui utekelezaji wake unakuwaje labda Mheshimiwa Waziri utakapokuja utuneshe namna gani asilimia mbili hii inayoenda kwa wenzetu wenyewe ulemavu inatekelezwa na inawafikia na labda faida zake zilizopatikana mpaka sasa hivi katika hiyo asilimia mbili ambayo inaenda labda itapatikana vipi faida katika himzo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri kwa heshima zote nimeamua kusudia kuweka kwenye eneo hili la uvezeshaji wa wanawake kiuchumi kwa sababu nina sababu nydingi sana, wanawake Tanzania tuko wengi, wanawake Tanzania tunajiweza kwa mambo mengi, kwa hiyo tunapopata fursa ya uchumi katika nchi hii Mheshimiwa Mpango na mipango yako mizuri uliyonayo basi uchumi wa Tanzania utakwenda kwa kasi kuliko hiyo ambayo umefikiria. Kwa hiyo mimi nasema hili kwa maana ya kwamba nina

sababu za msingi, mwanamke anapojiweza kiuchumi familia yake inaimarika, hatokubali mtoto asiende shule, ataelimisha kwa kadri ya uwezo wa mtoto kusoma. Lakini pia lishe ya nyumba itakuwa safi ya baba na watoto, pia afya itakuwa imezidi kuimarika katika familia tutapunguza matatizo mengi yaliyo changamoto katika Serikali yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la utekelezwaji wa watoto litapotea itakuwa si changamoto tena, mwanamke anajiweza kiuchumi, wewe mtelekeze ye ye anaendelea na shughuli zake. Kwa hiyo jamani kuwezesha mwanamke kiuchumi ni jambo la msingi kabisa katika Taifa letu. (*Makofii*)

Naona wanawake tumefurahi lakini ndio ukweli ulivyo hivyo kwamba wanawake Tanzania Mheshimiwa Waziri Mkuu unanisikia ikiwa tutawezeshwa vizuri basi nakwambia uchumi wa nchi hii utapaa kwa namna ambayo ni ya ajabu sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa wana baba nawaombeni tuna Mheshimiwa Rais wetu mpendwa kabisa ambaye anajaribu kuweka njia ya kuinyoosha Tanzania tuelekee kule ambako tunakutaka na mimi naomba aendelee hivyo nashukuru sana Mwenyezi Mungu ametuletea kiumbe ambaye anajaribu kunyoosha pale tulipopinda. Kwa hiyo, naomba Mungu atujalie tuendelee hivyo kwa hiyo lakini turudi siharibu hebu niacheni.

Sasa naomba nirudi kule kwa sababu kama hili ambavyo anatunyoosha kuelekea kwenye mambao mazuri tunayoyataka na wanawake atunyooshee tuendelee hivyo hivyo tutafika pahala pazuri sana Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Mipango. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli mpango huu ambaao nimeusoma baada ya kutoka kwenye ajenda yangu hiyo, huu mpango mimi wala sina pingamizi nao najua kazi unayofanya ni nzuri na hii kazi ni nzuri zaidi kwa sababu pembeni yako kuna mwana mama hapo ambaye yuko vizuri, ana upendo, ana huruma na yuko makini sana hapo, kwa

hiyo haya mambo yanakwenda vizuri mimi naamini Wizara zikiwa na mama na baba mambo yatakwenda vizuri kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naendelea kusema kwamba huu mpango kwa kweli naomba niwaambie Watanzania najua lazima mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni kazi zinazofanywa sio mbaya na tusiwandanganye Watanzania si kila jambo litakalofanywa na Serikali litawanufaisha watu wote ndege zinapoboreshwa Tanzania, watakaonufaika wapo na ambao watakuwa hawajui faida yake wapo lakini wakiwa wanufika si wananaufaika katika nchi hii. Kwa hiyo sasa leo ndege yetu inakwenda China wafanyabiashara wataacha *Ethiopian Airline*, wataacha *Kenya Airways*, watapanda ndege yetu ya Tanzania watakwenda kufanya biashara zao kwa hiyo na mambo mengine mengi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaboresha umeme ukawa umeme mzuri zaidi tutafaidika na viwanda ambavyo tunavipigania, yote ni sahihi tuna changamoto, changamoto ni sehemu ya maisha, hizi changamoto ambazo amesema hapa Mheshimiwa Mpango ziko dunia nzima. Kwa hiyo hayo sio tatizo lakini na *conflict* (migogoro) katika dunia ipo sehemu zote kuna migogoro ya kisiasa, kuna migogoro ya kiuchumi, muhimu ni namna gani ya *control* ile migogoro isiletet madhara katika dunia. Kwa hiyo, hayo naomba tuweke umakini sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala langu ambalo nimelizungumzia huu mpango huu pamoja na uzuri wake wote suala la uwezeshaji wanawake kiuchumi ndio mpango mzima, kama nilivyosema kwamba hii mipango ni mizuri sana lakini sekta tukimuweka mwanamke akawezeshwa basi mipango yote hii imeshamalizika haina jambo jingine ambalo litakuwa la ziada. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa muda wako umekwisha nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu atafuatiwa na Mheshimiwa Khatibu Said Haji,

Mheshimiwa Tunza Malapo ambaye atachangia kwa dakika tano ajiandae.

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kidogo. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti kwa hiyo mambo mengi nimeyachangia huko sasa nataka kusema mambo machache tu madogo.

Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi anayofanya na aendelee, niseme tu kwamba nchi inayojenga uchumi na hasa uchumi wa viwanda kuna mambo kama sita ya msingi ambayo yanatakiwa iyafanye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ni kujenga miundombinu ambayo *ita-support* uchumi huu ambalo Serikali inalifanya vizuri, lakini mazingira ya biashara ya kufanyia kazi na kuwekeza ni jambo muhimu pia. Jambo la tatu ni upatikanaji wa mitaji mikubwa *ku-support* miradi hiyo na mitaji hii inatoka nje na mingine iko ndani, jambo la nne ni ujenzi wa viwanda mama kama vyatya chuma, *industrial evolutionary* ya Ulaya ilitokea kwa sababu walijenga viwanda vyatya namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tano ni kuongeza matumizi ya malighafi za ndani tumesikia hapa wananchi wa Bunge wanasema kwa nguvu sana mazao ya kilimo yatumike hapa ndani, kuna mazao ya madini tuyatumie hapa ndani, *tu-add value* kwenye bidhaa tulizonazo hapa ndani. Na jambo jingine kubwa la mwisho ni matumizi ya teknolojia na wataalam, mafundi mchundo ndio wanaoweza *ku-support* jambo hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kidogo sasa kwenye mambo hayo kadri muda utakavyokuwa kutoa ushauri kidogo. Kwenye suala la miundombinu naona mpango unapendekeza vizuri na unafanya vizuri tunaona barabara zinajengwa, reli inajengwa, miundombinu ya bandari inajengwa mambo haya ni muhimu umeme. Lakini kuna changamoto kidogo ambazo zinajitokeza na Wabunge

wanasema, kwa mfano kwenye ujenzi wa reli tunafanya vizuri sana, lakini changamoto tuliyonayo ambayo nafikiri Serikali inatakiwa iangalie ni namna jinsi ambavyo tunaweza kupata fedha za kutosha kujenga hii reli kwa haraka, tunapojenga vipande kwa kweli tunaweza tukachelewa, tunaweza tukafika mwisho 2025 hatujafika kule ambako kuna mizigo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naishauri Serikali na Wabunge wengine wamesema tutengeneze huu mradi mmoja mkubwa kama tunaweza na tukope kwa *concession* kama inawezekana ni vizuri Serikali mkaendelea kuliangalia jambo hili kwa sababu tukiendelea kutafuta hela kidogo namna hii tunaweza kuchelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni lazima tuendelee kupanua miundombinu ya ndani barabara najua tunafaya vizuri lakini tuongeze juhud. Kwa mfano kuna barabara moja kule mikoa ya kanda ya ziwa kule inayounganisha mikoa zaidi ya mitano ambayo inapita kwenye sehemu za kilimo cha pamba, barabara hii inapita kwenye kilimo cha mpunga, kwenye mifugo kwenye mazao ya misitu na inaunganisha vipande vingi sana vya shughuli za kilimo. Barabara hii inatoka Korandoto kwenye barabara inayotoka Shinyanga kwenda Mwanza na inapita Ukenyenge kwenye Jimbo hili la Kishapu kwa Mbunge *sharp* inaingia Jimbo la Igunga inaenda Jimbo la Igalula ikitoka hapo inaenda mpaka Tura inaunganisha barabara kutoka Dodoma kwenda Tabora. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii inapita kwenye maeneo makubwa sana ya uchumi, naomba sana mpango huu kama inawezekana Mheshimiwa Mpango muiweke kwenye mpango, itasaidia sana kilimo cha pamba hata ule mkakati wa *C to C (cotton to clothing)* tunaweza kuutekeleza vizuri zaidi naomba sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili mazingira bora ya kufanyia biashara ni jambo ambalo limesemwa vizuri sana kwenye mpango, lakini bado kuna changamoto,

wafanyabiashara na wajenzi wa viwanda wanahangaika wanapiga kelele kwa kweli, mahusiano kati yao na watendaji ni shida, wote mmesikia *TRA* mpaka Mheshimiwa Rais mwenyewe akasema *TRA* msiwe polisi sana, naomba jambo hili tulienendeze tuhakikishe ushirikiano huu usiwe wa kipolisi na raia uwe wa *partner, partnership* ni muhimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona muda unakwenda jambo la pilii mitaji kutoka nje na ndani, mitaji mikubwa ni lazima hii tuihamasishe, mazingira ya kufanya biashara wawekezaji kutoka nje tuwahamasishe waje, najua Serikali mmetengeneza *blue print* basi muitekeleze, mazungumzo na wenzeru hawa wanaowekeza kutoka nje myaendeleze na muwe marafiki zaidi, tusiwaone wawekezaji kutoka nje mara nyingi nimesema kama wanyang'anyi na wezi hapana, hawa ni wadau wetu, watatuletea fedha, tutafanya vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni ujenzi wa viwanda mama kama nilivosema Mchuchuma na Liganga ni *project* ambayo ni mama kweli tukipata chuma leo kwa kweli tutatoka haraka kabisa, bahati mbaya mradi huu umesuasua miaka mingi, kila mwaka maneno ni yale yale. Kamati tumesema jamani huu mradi sasa ufile mwisho, tukipata chuma tukapeleka kwenye viwanda vyote vya nondo na vya misumali tukatumia chuma kujenga reli yetu, majengo haya makubwa tukatumia chuma ya ndani tumetoka kiuchumi vinginevyo tuna kazi kubwa sana tutachelewa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni kuhusu teknolojia, matumizi ya teknolojia na watalaam, kwenye mpango Mheshimiwa Mpango umesema vizuri sana, kada maalum za taaluma mnaziendeleza lakini juhudhi hazionekani ni lazima *VETA* hizi tuzipe fedha ya kutosha, tuwapate hawa watalam na mafundi mchundo wa kwenda kwenye viwanda vyetu, bila kufanya hivyo nchi ya India kwa mfano waliwekeza sana kwenye hiyo shughuli au shule za kuwafundisha mambo haya ya ufundi na wameweza sana kuendeleza viwanda vyao na sisi tunatakiwa tufanye jambo hili kwa nguvu nyingi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kusema...

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Kengele ya pili hiyo Mheshimiwa, ahsante sana.

MHE DKT. DALALY P. KAFUMU: Mungu atusaidie, ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Khatibu Said Haji atafuatiwa na Mheshimiwa Tunza Malapo kwa dakika tano, Mheshimiwa Joseph Musukuma ajiandae.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana awali ya yote nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia leo kuweza kusimama hapa na kUweza kutoa mchango katika hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuanza kuchangia naanza na utangulizi ambaeo ni muhimu kwa ninavyoona. Katika siku za karibuni kwenye nchi yetu umezuka mjadala mpana kuhusiana na juu ya ndoa za jinsia moja. Tumesikia sauti/kauli za baadhi ya Mawaziri akiwemo Mheshimiwa Kangi Lugola na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje. Katika kauli zao inaonekana kuna kamtego wa juu ya kuonekana kwamba kukubaliana na jambo hili na kukinzana na jambo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niwaambie Waheshimiwa iwe ni mtego au ni bahati mbaya, lakini sisi Watanzania hatutoingia katika mtego wa ushoga, Watanzania hatutaki ushoga hiyo ni mtego. Narudia kama alivyosema Mheshimiwa Kabudi iwe mmetumwa au ni bahati mbaya Watanzania hatutoingia kwenye mtego wa kukubali ndoa za jinsia moja na nawaambia *m-take note please, u-take note* Mheshimiwa Lugola, Tanzania ni Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania, ni muungano wa nchi mbili Zanzibar na Tanganyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar asilimia 99 ni waislamu na waislamu kwa vyovoyote suala la ushoga hawalikubali, tunawaambia nyooresheni maneno sawa, nchi yetu haikubali ushoga na huo ndio msimamo wa Tanzania nadhani mmenielewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naumia sana moyoni mwangu kuona nchi iliyostaharabika, nchi yenye utamaduni wetu wa asili, leo kuna baadhi ya watu wanasingizia misaada iwe ni ajenda ya kututoa sisi kutupeleka kwenye ubaradhuli, haiwezekani, hili jambo ni baya na Watanzania hawataki kusikia kabisa. Nawaomba viongozi wetu kama hili jambo likae kimya kama hamuwezi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hapa tumezungumza kuna mawe yale ya chuma kule Liganga, hivi kwa nini tusitumie akili zetu kwa rasilimali alizotupa Mwenyezi Mungu mpaka tunafikiria kulainisha maneno ooh, hatutawanyanya, hatutawafanya hivi. Watanyanyaswa kwa sababu sheria ya nchi yetu haikubali ushoga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kuchangia sasa, Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne, Rais aliyepita Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete aliwahi kusema...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Khatib na kuna taarifa Mheshimiwa Waziri anataka kutoa.

TAARIFA

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Khatib, rafiki yangu kwamba Bunge hili kwa mfano tunapokuwa tumekaa kwenye Bunge la Bajeti huwa tunatenga fedha kwa ajili ya matumizi mbalimbali kama maji, barabara, afya lakini kuna wakati tunaweza tukafanya *reallocation* ya kubadili matumizi fedha labda za maji ziende kwenye barabara au afya; afya

ziende kwenye maji, lakini hawa mashoga anaowazungumzia ambaao ni binadamu wenyewe viungo mbalimbali vya mwili, viungo ambavyo mashoga wanavitumia vina kazi maalum kwa mujibu wa uumbaji wa Mwenyezi Mungu. Serikali yetu kamwe haitaruhusu mwanadamu yejote kubadili matumizi ya kiungo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubadili matumizi ya kiungo ambacho kimekusudiwa kwa ajili ya kutolea haja kitumike katika matumizi mengine ambayo Mungu hakukusudia. (*Makofi*)

Kwa hiyo, nimpe taarifa kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Dkt. John Pombe Magufuli kwanza tuna sheria yetu ya Kanuni ya Adhabu ambayo inazuia makosa ambayo yanaitwa *unnatural offences*, kwa hiyo yanazuia kubadilisha matumizi ya kiungo cha mwanadamu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo asiseme kwamba labda Serikali inajichanganya juu ya jambo hili. Ni maelekezo ambayo tunayatoa pengine labda vyombo ndiyo vinaweza vikawa vinaandika tofauti, lakini Serikali yetu kamwe! Tanzania ni hekalu la roho mtakatifu. Serikali haiwezi kukubali hekalu la roho mtakatifu likatumika kwa mambo machafu ambayo hayakubaliki. Naomba nimpe taarifa tu. (*Makofi/Vigelegele*)

MWENYEKITI: Mnampa wakati mgumu kweli Mwenyekiti leo ni Mwanasheria. Mheshimiwa Khatib unaipokea Taarifa hiyo?

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Taarifa bora zilizowahi kutolewa kwenye Bunge hili, hii itakuwa inaongoza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitegemea majibu ya kiuanaume kama hilo lililotolewa na Mheshimiwa Kangi. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kuchangia...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Khatib, humu ndani kuna wanawake, wanakupigia sana makofi sasa majibu ya kiume ndiyo yakoje hayo?

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu matamu kwa wote. Nilitumia dakika moja sasa naanza upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais Mstaafu Jakaya Mrisho Kikwete wakati alipoazimia na akaweka nia ndani ya moyo wake kwamba Tanzania ipate Katiba Mpya alikuwa na maono mapana juu ya kuipeleka nchi hii katika mema tunayoyatarajia. Nataka ninukuu baadhi ya maneno machache aliyojasema Mheshimiwa Rais Mstaafu wakati wa maazimio ya kutunga Katiba Mpya. Mheshimiwa Rais Mstaafu Kikwete alisema, nanukuu;

(i) "Tutatunga Katiba Mpya itakayoainisha Muungano wetu kwa kuondoa changamoto zilizopo sasa.

(ii) Tutatunga Katiba mpya itakayoipa nchi yetu mfumo bora wa kuongoza na kuendesha mambo yetu.

(iii) Katiba itakayoimarisha upendo, ushirikiano na mshikamano miongoni mwa wananchi wa Tanzania licha ya tofauti zao za asili kwa upande wa Muungano na maeneo wanakotoka na tofauti za jinsia, rangi, kabila, dini, ufuasi wa vyama vya siasa.

(iv) Katiba itakayodumisha amani na usalama wa nchi yetu.

(v) Katiba itakayostawisha zaidi demokrasia, kuheshimu haki za binadamu, utawala wa sheria, utawala bora na kudhibiti maovu." (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli hii na maneno haya hakuna yejote ambaye anaweza kuyapinga kwamba ni

kauli iliyo hai na ni kauli ambayo haitakufa milele na milele na milele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais John Pombe Magufuli wakati wa kulifungua Bunge hili aliwahi kutamka uzuri wa juu ya kazi aliyorahisishwa na Rais aliyeppita wa kuandaa Katiba Mpya na akawaeleza Watanzania kwamba yeye ataendeleza pale palipobakia. Hiyo ni ahadi aliitoa ndani ya Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi tumemsikia tena Mheshimiwa Mtukufu Rais akisema kwamba hayuko tayari kutoa pesa watu waje wale bure kwa ajili ya Katiba Mpya. Mimi nataka kutoa ujumbe kwa Watanzania, Mheshimiwa Rais alipozungumza na akasema kwamba ataiendeleza Katiba ile alisema akiwa ndani ya Bunge hili, Bunge la wananchi na hii ndiyo nchi ya Tanzania. Yeye Mheshimiwa Rais ni sehemu ya Bunge na Bunge hili aliliaminisha hivyo, kwa hiyo nawaomba Watanzania bado waichukue kauli ya Rais kwamba ile iliyotoka kweney Bunge ndiyo kauli *official* ya umuhimu wa kuendeleza Katiba Mpya mpaka pale itakapopatikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti,...

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu. Kuhusu Utaratibu.

KUHUSU UTARATIBU

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Khatib leo alianza na hoja za msingi lakini katika hili analoendelea nalo kwa mujibu wa Kanuni ya 67(1) lakini nikienda Kanuni ya 64(e).

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa majukumu ya Rais unazingatia Katiba na vilevile suala la mfumo mzima wa uongozi na utawala wa Serikali na madaraka ya Rais yanazungumziwa pia kwenye Kanuni hiyo ya 64(1)(e) na inakataza kabisa kuzungumzia mwenendo mzima wa utendaji kazi wa Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, nini ambacho Mheshimiwa Rais anafikiriakukifanya, kukitekeleza, ziko *instrument* atakazozitumia pamoja na llani ya Uchaguzi ya chama chake, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayomuongoza, lakini kwetu sisi humu ndani tunapozungumzia utendaji wake wa kazi pia tutaongozwa na kanuni hiyo ya 64(1)(e) ambayo imeweka wazi jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ningependa tu kupata jambo hili la utaratibu la kuendelea kuangalia na kujadili yale ambayo ni vipaumbele vya utendaji kazi na utekelezaji wa shughuli za kila siku za Mheshimiwa Rais.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, mmemsikia Mheshimiwa Jenista akizungumza Kuhusu Utaratibu na ametaja Kanuni ya 64(1)(e) ambayo inakataza mambo kadhaa. Hii Kanuni ya 64 inakataza mambo mengi tu hilo likiwa ni mojawapo.

Mimi niwaombe Waheshimiwa Wabunge, Kanuni zetu zinatutaka tujielekeze kwenye hoja iliyoko mbele yetu. Kwa hiyo, tujielekeze kwenye mpango ndiyo unaojadiliwa sasa hivi tafadhali ili tusikatishane katika kule kuendelea kujenga hoja zetu mbele za Wabunge, lakini pia kumpa fursa Mheshimiwa Mpango na Naibu Waziri hapa waweze kupata mapendekezo yetu Wabunge katika mpango ambao watatuletea mwakani utakaotuongoza 2019/2020.

Waheshimiwa Wabunge, tusipofanya hivyo, utakuja mpango hapa tutakuja na malalamiko kama tunavyolalamika sasa. Tushiriki kikamilifu katika kuhakikisha mpango huu unakuwa bora kuliko iliyopita, ili tutakapokutana mwakani tusiwe na malalamiko tulionayo sasa. Tujielekeze kwenye hoja iliyoko mezani Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Khatib malizia dakika zako chache zilizobaki.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi mpango uliopita Mheshimiwa Mpango hapa nilishauri nikamwambia hivi, kodi zetu si rafiki kwa wafanyabiashara na nilikutolea mfano wa kontena moja la vitenge katika *tariff* zenu ninyi *TRA* hapa Tanzania mnai-charge karibu milioni 80; lakini kontena hilo hilo likifika Zambia wana-charge kama milioni 20. Matokeo yake mzigo unapita kwenye Bandari ya Dar es Salaam, unaenda kupelekwa Zambia na wafanyabiashara wetu wanalipia Zambia mzigo ule unakuja kidogo kidogo unauzwa katika soko la nchi yetu. Hilo nililishauri nikakwambia angalieni kodi rafiki, wafanyabiashara waweze kulipa, hamkulizingatia. Sasa ndiyo maana tukaona hata tukishauri hamfanyi kitu, turudi huku kwenye Katiba Mpya ndiyo itakayotuongoza ili tufikie mafanikio. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii mipango tumekuwa tukishauri mambo mengi sana. Wewe unaelewa Mheshimiwa Mpango kama biashara Tanzania imeanguka, wafanyabiashara wanakimbia nchi, tumeshauri njia. Mheshimiwa Zungu jana alisema gharama za Bandari ya Mombasa na Dar es Salaam ni tofauti kama ardhi na mbingu. Yanashauriwa hayo hamna mnachokifanya, turudi kwenye Katiba, Katiba ikituongoza tukipata uongozi bora, yote haya yataondoka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapolilia Katiba iwe bora, tunapolilia uongozi bora matokeo yake ziko nchi walizoweka miundombinu yao ya reli iwe na kila kitu. Ziko nchi ambazo zilifanikiwa katika mambo yote, walichokosa, ni uongozi bora dakika tano iligharimu mazuri yote yaliyotokana na walio tekeleza, Syria iko wapi leo, Libya iko wapi, Misri iko wapi leo? Ilikuwa hawana shida ya pesa wala miundombinu. Walichokosa ni uongozi mzuri, ushirikisho wa wananchi katika nchi zao ilisababisha kila kitu. Hii leo tunajenga hizo reil, *Stiegler's Gorge* na vitu vingi tunafanya, tutakapokosa ushirikiano, amani, uongozi bora, siasa safi matokeo yake

itakuwa tunafanya kitu cha hovyo. Dakika tano nyangi inaweza kuja kutokea watu wabaya wakamaliza jitihada zote kubwa mnazofanya zikaonekana hazikuwa na msingi wala maana yoyote. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa. Dakika zako zimekwisha. Mheshimiwa Tunza Malapo, dakika tano, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Musukuma, Mheshimiwa Jesca Kishoa ajiandae.

MHE. TUNZA I. MALAPO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Awali ya yote niombe Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha atuambie kwanini kwenye Mpangu huu hatuoni Hospitali ya Kanda ya Kusini, haipo kwenye mpango huo, haionekani kabisa kwa hiyo hatuelewi kama haitakuja kutekeleza ujenzi wake kuendelezwa au vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hilo niseme kwamba wafanyabiashara siku zote wanabembelezwa au kunatakiwa kuwe na majadiliano yenyе kuleta tija na sio vitisho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokiona watu tukisema biashara zinakufa mnasema zinazaliwa zingine. Wewe hata ukiwa na watoto 10 hautamani hata mmoja afe, isipokuwa unachokuwa unatamani uzae wengine waongezeke. Sasa mtu leo akiona biashara zinafungwa anashangilia kwamba wale walikuwa wezi, walikuwa nini! Baba yangu Dkt. Mpango huko tunakoelekea sio kuzuri.

Mimi nakusahuri kwa nia njema kabisa kaa na wafanyabiashara, muelewane, muone vikwazo vyao, mnatakiwa mtatue vipi na mfikie *negotiation*, ukija kwa mfano kwenye suala la korosho, watu wameitwa wamekaa mezani, wameitikia labda kwa hofu baada ya kuitikia tumefuata nini wewe mwenyewe unajua mimi sina la kulieleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie hili la kusema kwamba kuna wafanyakazi wachache *TRA*, vifaa

havitoshelezi; ni kweli hata ukisoma ripoti ya CAG imeeleza Halmashauri ya mama yangu pale Dkt. Kijaji inatakiwa kuwe na mashine 100, ziko 22 kwa mujibu wa ripoti ya CAG. (*Makof*)

Sasa mimi nishauri mzee wangu Mkuchika hapa wa Utumishi, hebu muangalie wapatikane wafanyakazi wa kutosha kwa ajili ya *TRA*, kutokuwa na wafanyakazi wa kutosha ndiyo huko kunakosababisha wale wachache wanawafikia watu wale wale kila siku, wanawalazimisha kulipa kodi zisizowezekana wakati kuna sehemu zingine mnaziacha. Kidogo kidogo hujaza kibaba kuliko mnapotamani mkamue ng'ombe kwa kiasi kikubwa, matokeo yake mnamfilisi, anakufa! *At the end of the day hamfaidiki ninyi wala hafaaidiki yule mfanyabiashara.* (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lingine ninalotaka nilzungumze, ukiangalia kwenye mpango nimesoma kwenye hotuba ya Kamati wanasema kwamba bajeti ijayo mnapendelekeza iwe triliioni 33.5 kutoka triliioni 32.47 na wakati huo huo utekelezaji ulikuwa 57%. Sijaelewa ni kwanini mnataka iongezeke wakati huo huo ukienda kwenye misaada na mikopo mnasema imepungua lakini kuna ongezeko la asilimia 26.3 kwenye pendeleko lijalo. Hii pesa inatoka wapi wakati mnasema imepungua, kwa nini tena mnazidi kuongeza na kwa nini wamepunguza?

Je, mmeefanya *analysis* mkajua kwanini inapungua? Mahusiano yetu na hizo nchi wahisani yakoje? Labda ndiyo yanasaabbisha haya mambo kwa hiyo utakapokuja kuhitimimisha naomba tupate majibu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu lingine ninalotaka kulzungumzia nataka kuzungumzia mradi wa gesi katika Mkoa wa Mtwara. Kuna *issue* ya *LNG plant* pale Lindi nataka kujua Serikali hivi vitu vimewashinda au mna mkakati gani wa dhati wa kuhakikisha vinatekelezeka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo uwekezaji katika sekta ya gesi ungefanyika kikamilifu nchi hii ingekuwa na umeme wa kutosha na ninyi Wabunge ndiyo mlikuwa

mnashangilia tunafanya uwekezaji katika gesi, gesi itatusaidia, gesi ina manufaa mengi, lakini leo wote tumegeuka tunashangilia, wote mmegeuka mimi simo, wote mmegeuka mnashangilia *Stiegler's Gorge* habari ya gesi tena basi! Sasa tunakwenda wapi? *Our vision ni nini?* Kwa sababu kwenye gesi tungepata viwanda vya mbolea, kwenye gesi tungeongeza ajira na vitu kama hivyo.

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa, kengele imeshagonga. Ahsante sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Joseph Musukuma, atafuatiwa na Mheshimiwa Jesca Kishoa, Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa ajandae.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. Nampongeza sana rafiki yangu Mheshimiwa Khatib kwa maneno mazuri sana leo aliyozungumza lakini hata vitabu vya dini vinasema umpende jirani yako kama unavyoipenda wewe mwenyewe. Kwa hiyo, maneno matamu aliyooongea na mazuri yenye usia mzuri kama Mtanzania halisi angeanza kwanza kushauriana na majirani wakimsikiliza kwamba ushauri wake ni mzuri sisi wa mbali tutapokea bila wasiwasi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nichangie upande wa biashara ya madini. Sisi tunatoka kwenye maeneo ya madini, nilitaka nimpe ushauri kaka yangu Mheshimiwa Mpango, biashara ya madini ni ngumu sana na kodi iliyowekwa kwa mchimbaji wa kawaida ni asilimia saba, maana yake *loyalty* asilimia sita na *export levy* ni asilimia moja na wachimbaji wameitikia wito wa kulipa hiyo kodi, hawana tatizo. Wanapomaliza kulipa hizi kodi unawarudishia tena dhahabu wakauze wao wenyewe, haijalishi ina ukubwa wa kiasi gani. Sasa hawana uwezo wa kupeleka Kenya, pengine hawana *passport*, hawana nini wanaenda kuuza kwa watu

wa kawaida, lakini baada ya mwaka unakuja tena kuwakamata unataka wakupe *document* ya ku-export ile dhahabu, biashara ya dhahabu ya dola moja faida yake ni shilingi 15,000 au 20,000 mtu hawezi ku-afford kwenda kuuza dhahabu Kenya au wapi, anauza humu ndani kwa watu wa kawaida anaendelea na biashara yake. Baada ya mwaka unakuja kumwambia tunaomba *document za export levy* na kama hauna utulipe 18% ya VAT.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu hiki sio sahihi na ninyi Serikali mimi nawashangaa kwa sababu unawezaje kuchukua dhahabu ukaitoza kodi halafu ukamrudishia mwenyewe akauze huku mnahangaika na kangomba, mnahangaika na kahawa, kwa nini msinunue hii dhahabu mkaiweka *stock* kuliko kuhangaika na mbaazi na kangomba hawa wanaotusumbua. Mnachukua hii kodi mnaenda kuhangaika na kangomba Mtewa. Nakuomba sana kama kuna uwezekano sisi tumeitikia kulipa kodi vizuri muichukue hii dhahabu, muiweke *stock* kwa sababu dhahabu haishuki bei kama hizi kangomba tunazohangaika nazo humu ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nilikuwa nazungumzia suala la upanuzi wa viwanja vya ndege. Mheshimiwa Waziri ninakuomba sana katika viwanja hivi ambavyo kiukweli vinaisaidia shirika letu kama Mwanza na Mbeya, tengeni pesa ya kutengeneza hivi viwanja tuache maneno ya kusema kila siku kitu ambacho hakitekelezeki.

Mimi nataka niwape mfano Waheshimiwa Wabunge wanaotumia uwanja wa Mwanza, ukienda ndege ya jioni inapoenda *Dreamliner* inaenda na watu zaidi ya 200, Wasukuma wameitikia kuchangia nchi yao. Inaenda *FastJet* na watu 100, inaenda *Precision Air* ina watu 70, mnapoteremka kwa wakati mmoja ni aibu, Mheshimiwa Waziri usipite *VIP* hebu pita huku wanapopita watu wa kawaida, ni msongamano ambaao kile kichumba kinaweza kupokea wageni 30, kinapokea watu zaidi ya 400 na kama hatuna hela basi mruhusu tuweke hata maturubai maana kuna mvua na kuna vitu vingine, lakini nikuombe ujaribu

kuangalia uwezekano wa kuwahisha ujenzi wa nyumba ya kupokelea wageni pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine Mheshimiwa Waziri, tunakubali kabisa kwamba tunahitaji nchi yetu tulipe kodi na tuchangie kwa kutumia *EFD machine*. Mimi naijuliza hizi hesabu wanazopiga pengine Wakuu wa Mikoa na Serikali inaruhusu, ukikaa hapa Dodoma ikifika saa 5.00 usiku karandinga inazunguka, kalaleni. Wageni wakija hapa, sasahivi nchi imehamia Dodoma unaweza ukaja kumuona Waziri, huna kazi nyingine hamjui mtu, ukaambiwa utamuona Waziri kesho kutwa, inabidi ukae kusubiri, kwa hiyo, mchana wote unaambiwa ukakale baa hazifanyi kazi, vitu vingi vimelfungwa, kuna tatizo gani? Kwani mnaambiwa na nani kwamba, mkiwalaza watu saa 5.00 usiku wanaenda kulala?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pengine watu wanaingia vyumbani wanajifungia, lakini mngeruhusu watu wakanywa bia watachangia pesa. Watu wakiingia kwenye ma-guest watapewa risiti. Tuache huu ukiritimba wa kuwalaza watu saa 5.00 usiku tujifunze kwenye nchi zinazoendelea. Sio kwamba, mkiwalaza watu saa 5.00 usiku ndio itakuja hela, tunapoteza pesa kwa vitu ambavyo tunataka kujiuliza tuna wasiwasi gani kwamba, ma-group ya majambazi yana nguvu kuliko polisi wetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye usafiri mnataka magari yasisafiri mwisho saa 5.00 usiku. Mtu anataka afanye kazi Mwanza aende akanunue vitu Dar es Salaam, polisi ni wengi wafanye doria na magari yaruhusiwe pia kutembea usiku na mchana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la viwanda. Suala la kufungua viwanda Tanzania kiukweli mnahamasisha vizuri na Rais wetu anafanya kazi nzuri, lakini sijui kama mnajua hizo adha zilizoko kwenye ufunguzi wa viwanda; unafuata *procedure* zote *TIC*, ukienda *TIC* pale *OSHA* yupo, *migration* yupo, taasisi zote zipo, lakini hazina *mandate* ya kuruhusu. Ukimaliza kujadili pale tena wanabeba makaratasi kumtafuta Waziri aweke muhuri, hiyo ni miezi sita.

Ukiruhusiwa kufungua kiwanda tena anakuja mtu wa mazingira anafunga, mtatuua na madeni tutauzwa na benki, jaribuni kutengeneza utaratibu mwингine. Jaribuni kuangalia hivi vitu vyote viishie *T/C* pale kuna kila kitu kiko pale, kwa nini tunawasumbua wawekezaji wetu? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri mimi juzi wakati imetangazwa kwamba kutakuwa na mdahalo wa wanachuo kikuu pale wanaojadili uchumi, sikutoka nje na niliweka mpaka *tv* huko jimboni kwangu watu waone Serikali ilivyofanya kazi, lakini haya mambo huwa ninazungumza kila siku wasomi wetu ndio tatizo mnapotukisha. Mimi nilidhani mtachambua na kuwaeleza watu kwamba, uchumi wetu kutoka miaka mitatu alipoingia Rais Magufuli tumefanya hiki kwenye kitengo fulani, tumefanya hivi kwenye dhahabu, tumefanya hivi kwenye nini, badala yake tena wasomi wetu mmeenda kuchambua tu hotuba za Rais ndio mmetuwekea kwenye *tv*. Maana yake Rais wetu anafanya kazi nzuri, wasomi wakubwa mmeshindwa kuwaelimisha watu wakajua tulikotoka na tulipo kelele hizi zikaisha? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnaenda kuchambua maprofesa wazima mnachambua hotuba za Rais zilezile ambazo Mheshimiwa Rais Magufuli anatueleza na tunampenda kwa sababu hiyo hiyo. Nilikuwa naomba sana maprofesa mliomo humu, ikitokea tena mnafanya huo mjadala mtukumbuke na darasa la saba tuna akili za kushauri kuliko za kwenu za makarasi. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka kuchangia kuhusiana na biashara ya sukari. Nimesikia kuna wafanyabiashara kule Kahama na wapi wamekamatwa. Mimi najiuliza hebu mfanye utafiti, *issue* hapa sio kukamata wafanyabiashara, watu wanarudishwa maisha yale ya kawaida na ninasikia Wabunge wengi kila mtu anasimama anasema hali ni mbaya hali ni mbaya, ningekuwa nategemea kila Mbunge aseme Rais alegeze wapi, pesa zilizopotea ni zile za wizi na kanjanja, haya maisha sisi tumeyazoea vijijini siku zote wala hatuna tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pesa zilizopotea sio kwamba labda ziko kwenye biashara ya sukari, mimi nikiuliza leo uki sema sukari sijui inaletwa kutoka nje, kama biashara ya sukari inaletwa kutoka nje wanafanya *re-bag* wanaweka kwenye mifuko ya Tanzania tumuite na mtu wa biashara ya majani ya chai tumuulize naye kama anauza na yeye biashara ni mbovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi niombe tu haya mambo bya mabadilliko ya tabia ambayo sasa hivi Watanzania tunaishinayo tutapata taabu sana kuyaelewa kama tutakuwa hatufanyi *research* za kutosha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala lingine nilikuwa nataka kuzungumza kuhusiana na suala, niliwahi kuzungumza humu watu wengi wakanicheka na sioni ajabu kuzungumza, suala la bangi. Mnaona na bahati nzuri mimi natumla simu ya tochi, ninyi wote humu wengi mna simu za *whatsapp*, za mitandao hizi na nini, ukiangalia Canada juzi wameruhusu, foleni iliyokuwepo hajjawahi kutokea utafikiri wanachagua Rais wa nchi, kwenda kununua bangi iliruhusiwa hadharani, ukienda Lesotho, ukienda Zambia, ukienda *South Africa* hivi vitu vimeruhusiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka niwambie wataalam mnaofanya *research* mnasema bangi ina matatizo, mimi sio mvutaji, ina matatizo, mnaokula *diclopa*, mnakunywa *coca cola*, *red bull*, hizi zote ni bangi ni ganzi...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Musukuma. Ahsante sana kengele ya pili imegonga. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Waziri wa Fedha amesikia ushauri huo muhimu wa kufanya utafiti jambo hili. Mheshimiwa Jesca Kishoa atafuatiwa na Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub ajiandae.

MHE. JESCA D. KISHOA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kujadili kwenye hotuba hii muhimu ya mpango wa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapojadili mpango wa maendeleo kimsingi tunajikita kwenye mambo matatu makubwa, jambo la kwanza tunajadili ni namna gani tunakwenda kuongeza mapato; jambo la pili, tunajadili ni namna gani tunakwenda kupunguza gharama ambazo sio muhimu kwa maana ya kupunguza matumizi yasiyo ya lazima, lakini jambo la tatu tunazungumza namna ya kutekeleza vipaumbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nitakwenda kugusia upande wa ni namna gani tunaweza kuongeza mapato. Nitajikita kwenye eneo ambalo ninaamini kwa sehemu kubwa sana tunapoteza mapato; tunapoteza mapato mengi kwenye eneo la mikataba mibovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni bahati mbaya sana na ninashindwa kuilewa *commitment* ya Serikali katika hili. Kwamba, ni kwa nini mnashindwa kufanya *review* kwenye mikataba mibovu ambayo tunapoteza mapato mengi Serikalini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 5 mwezi Mei mwaka huu alisimama AG humu ndani, kipindi cha Bunge la Bajeti akiwa anajibu hoja yangu ya mikataba mibovu, *specifically* kwenye Mkataba wa *SONGAS*. Ali-*declare* na akakubali kwamba, mkataba wa *SONGAS*ni mkataba ambao uko *very complicated* na *Hansard* ninayo hapa ya siku nzima ya tarehe 5, kwa sababu ya muda siwezi kumnungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali aliahidi kwamba, mikataba mibovu ukiwepo mkataba wa *SONGAS* utakwenda kufanyiwa marekebisho ndani ya miezi miwili kuanzia mwezi wa tano, lakini mpaka hivi ninavyoongea leo huu ni mwezi wa 11 hakuna mrejesho wowote, hakuna chochote ambacho kumefanyika na kila mwezi kuanzia mwezi wa 05 mpaka sasahivi mwezi wa 11

tunapoteza dola milioni tano kila mwezi kutokana na mkataba huu mbovu *for 14 years*, kwa miaka 14 tumekuwa tukipoteza mapato kutokana na mkataba huu. Hapa ndio ambapo naweka kigugumizi ni kwa nini Serikali inashindwa kurekebisha kufanya *review* kwenye mikataba hii ambayo inaingiza hasara kubwa kwenye Taifa letu? Nataka wakati tunahitimisha Mheshimiwa *AG* aje atupe mrejesho wa wamefikia wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo ukienda ukiangalia *international standards* za *contracts* kuna kipengele kwenye mikataba ambayo, *especially* mikataba ya umeme, kuna kipengele kinaitwa *despute resolution*. Hiki ni kipengele ambacho kama kuna *conflict of interest* kwenye pande mbili kwenye mikataba basi, wanapata fursa kupitia kipengele hiki kwenda kufungua *account* ambayo inaitwa ni *Escrow Account*, wanaweka fedha kule mpaka mgogoro utakapokwisha. Kwa nini kwenye suala la *SONGAS* kunakuwa kuna kigugumizi cha kuchukua mapato yanayopatikana kupeleka kwenye *account* ya *Escrow* mpaka pale tutakapojua mbivu na mbichi ni zippi? *That is question number one.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ni kwa nini kwenye Mkataba wa *SONGAS* Serikali mnashindwa kuchukua kesi na kupeleka *arbitration?* *Who is behind this* kiasi kwamba, mnashindwa? Mbona kesi ngapi mnazipeleka *arbitration* kwa nini kesi ya *SONGAS* ambayo taarifa mmepoteza pesa nydingi kuliko hata kwenye kipindi cha *IPTL*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampuni hii tunaingia hasara kubwa sana kama Serikali, sijajua ni kwa nini tunasusua katika kuchukua hatua? Ninashindwa kuelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo kama Taifa tunapoteza mapato, hapa naomba niwazungumzie *TEITI* na nichukue fursa hii kuwapongeza sana *TEITI* (*Tanzania Extractive Industry Transparency Initiatives*). *TEITI*/wote tunajua ni muunganiko wa makundi matatu, kundi la kwanza ni asasi za kiraia wako watano, kundi la pili ni makampuni wawakilishi

kutoka kwenye makampuni ambao wako watano, makampuni ya sekta ya uziduaji, na kundi la tatu ni wawakilishi kutoka Serikali ni jumla wako 15 ni makundi muhimu sana. *TEITI* wameitoa ripoti mwezi wa nne mwaka huu ambayo inaonesha kwamba Serikali ya Tanzania inakiri kupokea shilingi bilioni 435 kutoka kwenye makampuni yanayo-*deal* kwenye sekta ya uziduaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo makampuni husika, kwa maana ya makampuni yanayo--*deal* kwenye *oil, gas and mining*, yanakiri kwamba yenyewe yamepeleka Serikali bilioni 465. Sasa na *TEITI* wanasesma kwamba huu utafiti walioufanya uli-*deal* na makampuni 50 kati ya makampuni 1,287. Unaweza ukajiuliza kama kwenye makampuni 55 peke yake ya sekta hii ya uziduaji wamegundua kuna upotevu wa fedha shilingi bilioni 30 *what if* wangefanya upekuzi kwenye makampuni 1,287 tungekuwa tumepata hasara kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *well and good* Mheshimiwa Waziri ali...

WAZIRI WA MADINI: Taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Madini.

TAARIFA

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nipende tu kumpa Taarifa mzungumzaji na bahati nzuri ni Mjumbe wa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini na tuliwawasilishia taarifa hii walitaka kujua taarifa ya ulinganisho wa mapato yaliyolipwa na kampuni za sekta ya uziduaji pamoja na mapato ambayo yalipokelewa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachofanyika kwa mujibu wa sheria ya *TEITI* ya mwaka 2015, kwa mujibu wa kifungu cha 18 cha Sheria hiyo ya *TEITI* ya mwaka 2015 ulinganisho unapofanyika kuna *factor* nyingi zinaangaliwa, lakini pili

wenyewe *TEITI* kuitia Kamati yao ya *Multisectoral Group* ndio wanaoainisha ni kiwango gani au ni kampuni ngapi zinazotakiwa kwenda kukaguliwa na wao wenyewe kwa mujibu wa kamati hiyo ya *TEITI* walichagua *threshold* ya milioni 300 au zaidi katika kodi ambazo zinalipwa na kampuni husika. Na katika kampuni ambazo ziko katika sekta ya uziduaij ni kampuni 1,287 na zilichaguliwa kampuni hizo 55 kwa kuwa ndizo ambazo zilikuwa zinalipa zaidi ya milioni 300 na zaidi katika malipo ya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, katika kampuni hizo 55 ndizo ambazo katika uchangiaji katika mapato ya madini...

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

WAZIRI WA MADINI: ...katika uchangiaji wa mapato ya madini wanachangia kwa zaidi ya 95%. Kwa hiyo, kusema kwamba kuna mapato yamepotezwa si kweli na ndio maana kwa mujibu wa kifungu cha 18 hapa ni ulinganisho kwa hiyo, taarifa ilitoa utofauti. Tofauti ya bilioni 30.5 ambayo kwa mujibu wa kifungu cha 18.3 *MSG* ya *TEITI* imepeleka taarifa hiyo kwa *CAG* na yeye atapitia, atafanya na yeye ulinganisho wake kwa mujibu wa taaluma yake na atarudisha ripoti stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Kishoa asitake kuleta sintofahamu kwenye Bunge, hebu tusubiri Taarifa ya *CAG* na ninaamini taarifa kamili itawasilishwa.

MWENYEKITI: Utaratibu, Mheshimiwa Kishoa naomba ukae. Mheshimiwa Salome kanuni iliyovunjwa?

KUHUSU UTARATIBU

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kwa Kanuni ya 68(1) inayoniruhusu kuomba Utaratibu.

MWENYEKITI: Nakutaka utaje kanuni iliyovunjwa, hiyo hiyo kanuni ndio nakutaka utaje kanuni iliyovunjwa.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa naangalia.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kishoa, unaipokea Taarifa hiyo?

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Salome, tutakusubiria kweli uitafute wewe kanuni? Unaposimama uwe nayo.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hiki kitabu ni kikubwa nitasoma kama biblia?

MWENYEKITI: Aahh haa, ultakiwa uwenayo, naomba ukae. Ultakiwa ukisimama useme kanuni gani amevunja, kama ndio unaitafuta huo sio utaratibu. Endelea Mheshimiwa Kishoa. (*Makofii*)

MHE. JESCA D. KISHOA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa sababu amezidi kuishindilia hoja yangu na kuthibitisha kwamba kuna sintofahamu ya shilingi billioni 30. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amesema kwamba wamepeleka taarifa ili *CAG* aweze kukagua haya makampuni. Swali dogo sana, wote tunajua kwamba, sheria haimruhusu *CAG* kufanya ukaguzi kwenye makampuni ambayo Serikali inamiliki *less than 50%* ya *shares* kwenye makampuni hayo. Sasa anatuthibitisha kwa kiwango gani kwamba *CAG* atapata mamlaka ya kwenda kufanya upembuzi na ukaguzi ambao ni wa uhakika na wakati bado hana *authority* ya kufanya hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hii niiseme tu, kipindi kijacho tutunge sheria ambayo itampa uwezo *CAG* aweze

kwenda kupenya mpaka kwenye makampuni ambayo Serikali inamiliki *less than 50%* ili kuweza kuondoa mapato yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tukishindwa kudhibiti mapato yetu yanavyoendelea kupotea hatuwezi kufanya maendeleo yoyote, miradi yoyote haiwezi kufanyika. Natambua zipo njia nyingi ambazo zinatumwi na makampuni mbalimbali kukwepa kodi na kupoteza mapato yetu. Na moja ya njia hizo, yapo makampuni ambayo yanatumia njia ya *transfer pricing*, yapo makampuni ambayo yanatumia njia ya *thin capitalisation* na yapo makampuni ambayo yanatumia njia ya *production cost* na eneo hili ndio sisi kama Taifa tunapoteza sana.

Kwa hiyo, nilikuwa ninaiomba Serikali kwa unyeyekevu mkubwa sana wala sina nia ya kumkomoa mtu ye yote hapa, ninachojaribu kukifanya ni kutaka kama Bunge, kama Serikali, kama nchi, tuhakikishe tunalinda mapato yetu na hatupotezi mapato yetu kwa namna yoyote ile. Kwa sababu siku ya mwisho wanaokwenda kuumia ni sisi wenywewe. Tunakaa hapa, tunakaa Bungeni tunakula fedha za wananchi kwa njia ya posho tunajadiliana mambo ambayo utekelezaji wake ni mdogo sana kwa sababu kubwa usimamizi wa mapato bado ni mdogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili ni jambo la msingi ambalo nashauri sana na wala nisitafsiriwe tofauti, ni kwa nia ya kutaka kujenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa muda wako, hii ni kengele ya pili. Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, Mheshimiwa Ali Saleh Khamis ajiandae.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu aliyenijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako hili tukufu, lakini nikushukuru sana wewe kwa kunipa fursa ya kuchangia katika mapendekezo haya ya mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema kwamba lengo kuu la Serikali ni ustawi wa Wananchi wake. Na Wananchi ndio msingi wa mamlaka na Serikali itapata madaraka na mamlaka yote kutoka kwa Wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya mpango yana mambo saba ambayo yamezingatiwa. Jambo la kwanza liliozingatiwa wakati Mheshimiwa Dkt. Mpango anaandaa mpango wake ni Dira ya Taifa ya Maendeleo mwaka 2025, lakini pia Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano 2016/2017, 2020/2021, lakini pia llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2015/2020 pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuzingatia kuyandaan haya mpango pia ni lazima uzingatie Katiba, lakini pia uzingatie sheria na maelekezo ya viongozi. Maelekezo ya viongozi ni sheria kama ambavyo leo hii tunapitia mpango na baadae mapitio yale yatakuwa ni sheria ambayo yatakwenda moja kwa moja katika kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona nianze na hili na niseme tu kwa nia njema kabisa, kumekuwepo na sintofahamu ambayo baadhi ya Wabunge wamezungumzia kutoridhishwa na baadhi ya majibu ya Waziri wetu wa Ujenzi.

Sisi ni miuongoni mwa watu ambao tulimpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi akiwa Waziri wa Maji, lakini amekuwa akitoa kauli ambazo wakati fulani haziridhishi na mimi nichukue nafasi hii kumuomba sana kwamba ile kazi nzuri aliyofanya akiwa Waziri wa Maji basi aweze kuiendeleza. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako maeneo ambapo Mheshimiwa Rais aliweka ahadi. Ahadi zile ni sheria ambazo zinahitaji kutekelezwa, lakini sasa wewe Mheshimiwa Waziri ukinijibu mimi kwamba yale uliyoachiwa na Mheshimiwa Profesa Mbarawa wewe hauhusiani nayo, ninapata taabu sana kuelewa ni namna gani sasa umeamua kuwasaidia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunafahamu kwamba sheria ya uongozi inatutaka viongozi kugusa mioyo ya wananchi wetu na kutugusa sisi wenyeewe, *leaders touch the heart before they ask for hands*. Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Waziri arekebishe na arejee kwenye kasi yake nzuri aliyokuanayo akiwa Waziri wa Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 9 ya Katiba inazungumzia namna ambavyo shughuli za Serikali zinatekelezwa kwa njia ambazo zitahakikisha utajiri wa Taifa unaendelezwa, unahifadhiwa na unatumwiwa kwa manufaa ya Wananchi wetu wote, lakini Ibara ya 9(d) inasema kwamba maendeleo ya uchumi wa Taifa yanakuzwa na kupangwa kwa uangalifu na kwa pamoja. Mheshimiwa Dkt. Mpango amezungumza changamoto nyingi ambazo kimsingi ndio mijadala ya Bunge letu hili tukufu, amezungumzia ugumu wa ukusanji wa kodi, amezungumzia kushuka kwa biashara za Kimataifa, amezungumzia upungufu wa wafanyakazi (ajira), lakini pia amezungumzia kupungua kwa misaada na pia amezungumzia madai ya watumishi.

Mimi nimuombe sana Dkt. Mpango wakati sasa anakuja kujibu hapa hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge, kwanza kabisa atambue kwamba lipo andiko liliwahi kutolewa na Tony Cliff katika kitabu chake alichowahi kuandika *Building the Party* ambacho kimetolewa mwaka 1975, akimnukuu Lenin.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Taifa lolote ni vyema tukajuliza tulichonacho na namna ambavyo tunataka tukitumie, mimi kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Rufiji na kwa Watanzania wote, nichukue nafasi hii

kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa nia yake thabiti katika ya kutekeleza mradi wa kuzalisha umeme yaanai *Stigler's Gorge*, mradi wa kuzalisha umeme kule Rufiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki ni kilio cha muda mrefu sana cha Watanzania, kwa kuwa historia inatuambia kwamba jambo hili lilianzia miaka ya 56.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Mwalimu Nyerere ye ye akiwa ni *pioneer* wa jambo hili, alisisitiza sana kwa mchakato huu wa uzalishaji wa umeme ambao utakwenda kuwasasidia Watanzania wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nipongeze Serikali, lakini pia niwapongeze sana wananchi wangu wa Jimbo la Rufiji kwa kuwa jambo hili wao walinikabidhi mwaka 2015 na ilikuwa ni ahadi yetu sisi nyakati za kampeni, lakini pia mwaka 2016 niliingia nalo ndani ya Bunge lako hili tukufu. Nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, lakini pia nimpongeze sana Waziri wa Nishati atambue kwamba wananchi wetu wa Jimbo la Rufiji wanamuunga mkono sana, na kwa kuwa mradi huu upo Rufiji, asikate tamaa na sisi tunasema kwamba Serikali iendelee na mchakato wote wa kuandaa miundombinu ya ujenzi wa bwawa hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini zipo changamoto ambazo sisi wananchi tunaziona. Leo hii tunatambua kwamba hata tukiwaliza Mawaziri wetu wanaohusika suala la wakulima na wafugaji, halijazungumzwa sana katika vitabu vyetu hivi, hata Dkt. Mpango hajalizungumzia sana ambavyo ni namna gani Serikali itakwenda kuwasaidia wafugaji katika kuandaa maeneo ambayo wataweza kufanya mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamuunga mkono Mheshimiwa Rais kutekeleza ujenzi huu wa uzalishaji wa umeme katika Bwawa la *Stigler's Gorge* pale Rufiji, lakini tunahofia sana wananchi wa Rufiji, kwa kuwa leo hii mifugo imeingia sana katika eneo la Bonde la Mto Rufiji na pengine tunalaumu sana Serikali wakati ule miaka ya 2005

walipoamua kuondoa mifugo katika Bonde la Ihefu na kuleta mifugo katika Bonde la Mto Rufiji wakijua kabisa kwamba dhamira ya Mwalimu Nyerere ya mwaka 1956 ilikuwa ni kulilinda Bonde la Mto Rufiji na ndio maana Mwalimu Nyerere mwaka 1978 alianzisha sheria maalum kabisa sheria ya kuanzisha *RUBADA* ili kuweza kulinda Bonde la Mto Rufiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana Serikali na nimuombe sana Dkt. Mpango, atakapokuja kuhitimisha hapa basi aone changamoto hii kubwa ambayo Mheshimiwa Rais leo hii anakwenda kutekeleza mradi huu wa *Stigler's Gorge*, mradi wa kuzalisha umeme Bonde la Mto Rufiji. Lakini leo hii tuna mifugo zaidi ya laki tano ndani ya Bonde la Mto Rufiji, tunafahamu Bonde la Ihefu lilikufa na uoto wa asili ukaharibika, mvua zilikuwa hazinyeshi na leo hii tunakwenda kuandaa Bonde la Mto Rufiji ambalo mifugo zaidi ya laki tano imeingia kwenye Bonde, hakuna jitihada zozote ambazo zimeandaliwa na Wizara ya K ilimo, Wizara ya Mifugo na Wizara ya Ardhi na Wizara nyingine namna gani wanakwenda kutatua kero kubwa ya wakulima na wafugaji, ili sasa kumsaidia Mheshimiwa Rais wakati anakwenda kutekeleza mradi huu wa kuzalisha umeme, kuwepo na maji ya kutosha kwa sababu tunatambua kwamba mradi huu utahitaji uzalishaji wa maji yaani mvua za zaidi ya miaka miwili au miaka mitatu kuweza kujaza bonde lile katika uzalishaji umeme.

Kwa hiyo, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri, atakapokuja kuhitimisha aelezee mpango wa Serikali ni namna gani sasa Serikali itakwenda kutatua kero kati ya wakulima na wafugaji. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub atafuatiwa na Mheshimiwa Ali Salim Khamis, Mheshimiwa Katani Katani ajiandae.

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kwanza kukushukuru kwa kuniruhusu kusimama hapa na kama sijithada zako baada ya Mwenyezi Mungu kuniruhusu, nitakuwa sijakufanya haki lakini nikushauri

tu na nikuombe, tunapoomba Mwongozo ungejaribu kutusikiliza kuna nini wewe ndio Mwenyekiti na unatoa *ruling*. Kuliwahi kutokea moto humu ndani wa simu, pengine lilikuwa jambo la hatari huwezi kujua, usidharau wito, dharaunaloitiwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jaku, inavyoonekana husomi vizuri Kanuni, ukitaka kulalamikia maamuzi ya kit, unaandika barua kwa Spika, ataitisha Kamati kwa ajili ya kazi hiyo. Kwa hiyo, usiyalete malalamiko dhidi ya kiti kirahisi rahisi namna hii, Kanuni zetu zinakataza sawa sawa.

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na ukurasa wa 25 wa kitabu hiki, ulipaji wa madai Serikali liliipa jumla ya shilingi bilioni mbili *point* ngapi za madai yaliyohakikiwa kwa Wakandarasi, watoa huduma, watumishi wa umma kwa madai mengineyo kati ya kiasi hicho shilingi bilioni 1.6 zililipwa kwa wakandarasi wa shilingi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi asubuhi, katika kipindi cha maswali na majibu nilitetea Kampuni karibu mara sita na Naibu Waziri akajibu alivyojua mwenyewe, lakini yule jamaa sasa hivi ni mgonjwa ka-*paralyze* na yote hii kutokana na mazoezi ya kupanda ngazi na kushuka kwenye Maofisi. Anafanyishwa mazoezi bila kutaka mwisho wake kapata mtihani, kwa hiyo niombe Serikali hili suala iliangularie katika madeni na huyu umuangalie na *Hansard* zipo haya sio maneno yangu. Mwenzi Novemba 2017 suala hili limeulizwa...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jaku nadhani ulimsikia Mheshimiwa Spika alivyotoa Mwongozo wa namna ya kuchangia mpango, kila mtu akileta jambo liliotokea kwao kwenye Jimbo lake saa hizi kwenye mpango si sawa, Mheshimiwa Jaku tuelewane usichangie jambo ambalo umeshalizungumza ni mahususi kwa ajili ya hiyo kampuni tafadhali. Changia mambo ya jumla kama unatumia huo kama mfano ni sawa, ukiendelea kusoma hivyo nasikitika nitakukatisha.

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye ukurasa wa 3 na 17 naomba uangalie maana nisijefika mahali nikawa nazungumza labda kitu sio. Niangalie kwenye hiki kitabu ukurasa wa 3 na 17 angalia halafu kama nitakosea nikosowe wewe ni mwalimu mzuri wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulihakikishia Bunge lako tukufu kwa ushauri, maoni yatakayotoka katika kikao hiki cha Bunge yatazingatiwa kikamilifu katika kuandaa rasimu ya mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, humu naomba kuisoma hii *Hansard* na juzi ulikuwepo tena ili iwe *record* katika Bunge hili nitakapokuja kufa angalau historia itanihukumu au itanikumbuka; "Sasa kwa sababu ahadi ilikuwa ni Bunge hili basi, tutasogezza ahadi kwa Bunge Ijalo, Bunge Ijalo halipo mbali sana, kwa hiyo ni vizuri kwa kweli mtakapotoka hapa basi mjithahidi Bunge Ijalo tusikie lugha nyingine ili tuendelee na mambo mengine, tunajua ni kubwa na lina mambo mengi, lakini umuhimu kwa sababu ya *interest* kubwa ya zaidi ya Muungano."

MWENYEKITI: Sema ni ukurasa wa kitu gani, wa ripoti hii, wa hotuba, wa kitu gani ili twende pamoja Mheshimiwa Jaku?

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: *Hansard* ya Bunge hili tena ni maneno ya Mheshimiwa Spika haya mazito yaheshimiwe.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jaku, hoja yako ni nini? Kwa sababu ukitusomea tu hivi tunashindwa kufuata kwamba unazungumzia nini, ukitusomea tu bila kusema una nukuu wa ajili ya kazi gani hatukuelewi Mheshimiwa Jaku.

Sasa usiongee kwa sababu mimi nimekukata kwa sababu hakuna hata anayekusikia wala hata mimi sikusikii. Nisikilize ninachozungumza, nasema hivi hoja yako ni nini, zungumza hoja yako halafu unukuu unachotaka kunukuu, ukianza kutusomea ambacho tunacho tayari kwenye Taarifa Rasmi kama unavyosema hatukuelewi unazungumzia nini na

hiyo taarifa unayonukuu umeanzia tu katikati, kwa hiyo hatukuelewi na mimi Mwenyekiti pia sikuelewi, ndio maana nataka tuliongoze Bunge ili tuelewane twende pamoja, unasoma nini na hoja yako ni nini.

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 17 miradi ya umeme. Utekelezaji wa miradi ya umeme na kufufua kwa kutumia vyanzo mbalimbali vya nishati ikiwemo maji na gesi, kuendeleza miradi ya umeme ikiwemo sakata hili la Zanzibar la VATumeme mara mbili, na sheria ya VATmradi wa mwisho unaotakiwa alipe VATile hili sakata la muda mrefu.

Kwa hiyo imefika mahali hili Bunge na haya maneno ni mazito katika chombo hiki, liliifika hili suala Serikali Itoe kauli, tulishaambiwa Bunge linalokuja, linakuja linakwenda, linearudi tunafika wapi? Kwa hiyo, hili suala liangaliwe, Mheshimiwa Waziri nilishajitahidi sana kumfuata anavyotaka yeye na Mwenyezi Mungu shahidi, nilishampa mpaka viongozi wakuu si vizuri kuwataja hapa kuzungumza nao hili suala linatusokota, hatutendewi haki na si suala hili tu la VATla umeme bidhaa yoyote iliyotoka Tanzania Bara ikaingia Zanzibar VAT mara mbili. Nini maana ya VAT, nini *formula* yake tupeni *definition* ya VAT. Imekuwa tunasokotana tu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitabu cha mapendekezo ya mpango wa maendeleo ya Taifa kujumuisha mapitio ya hali ya uchumi, utekelezaji mipango na maendeleo ya mwaka 2017/2018 robo ya kwanza ya mwaka 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa uchumi ikiwemo mabenki uchumi, leo *FNB Bank* ina mwaka wa tatu, watu wanateseka tumeuliza kwenye chombo hiki mara nne, mimi mwenyewe mara mbili, tumefanya semina na watu wa Benki Kuu humu ndani wakatuambia muda si mfupi pesa zitapatikana wengine wameshatangulia mbele ya haki kwa Mwenyezi Mungu, sasa huku wanataka kuhujumu uchumi pesa zimebaki tu kule, na pesa dhamana ni Waziri wa Fedha

kupitia Benki Kuu, hebu toeni ufanuzi hizi pesa na sio kama benki imefilisika, pesa ziko wapi, *Dutch Bank* ya Ujeruman. Tunaambiwa zinaletwa, zinaletwa kwa mguu au kwa baiskeli na hazifiki mpaka leo, wananchi wanaumia Serikali ndio wananchi na wananchi ndio Serikali, hebu fikeni mahali mliamue hili suala.

Lakini jambo lingine wafanyabiashara wadogo wadogo wa Zanzibar wenye hata *tv* moja, simu tatu za mkononi wakafika Bandarini Dar es Salaam wanapata fatiki, wananyanyaswa na hesabu inaanzia moja hata hao matajiri wakubwa walianza na hesabu hii moja, wakafika mbili, wakafika tatu. Mtoto akizaliwa haendi mbio siku hiyo hiyo, hutambaa akaokotwa, akaanguka, akakamata ukuta. Sasa mfike mahali wafanyabiashara wadogo muwathamini. Bandarini Dar es Salaam kumekuwa usumbufu maana utafikiru unakwenda wapi, hakuna mvua, hakuna juu, hakuna usiku, hakuna mchana. Tufike mahali Waziri wa Fedha uwaonee huruma, na wao wanataka kupanda *V8* hawa. Eeh hesabu inaanzia moja, mtoto hazaliwi akaacha ziwa siku hiyo hiyo. (*Kicheko*)

Mheshimwa Mwenyekiti, nige habari ya viwanda ukurasa wa 42 kama sikosei katika kitabu hiki maana itabidi twende kwa *data* sasa hivi. *No! no!* naomba *Hansard* ikae sawa 42 kuhusu udhibiti wa matumizi ya fedha za umma sio viwanda, matumizi ya fedha za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar niipongeze sana Benki Kuu sana unajua tuseme ukweli penye ukweli tuseme ukweli katika watu wanaolipa kwa wakati 4.5 Benki Kuu, hili niwapongeze sana Waziri wa Fedha nakutuma unipelekee salamu kwa Gavana hili lazima tushukuru. Lakini hii 4.5 toka urembo ungali tunguja wazee wetu walikuwa wakijifunga vile vitu vyatya ajabu ajabu kwenye masikio sasa hivi dunia imekuwa, *population* ya Zanzibar imekuwa 4.5 hii haikidhi, ifike mahali izingatiwe barabara zimeongezaka, watu wameongezaka, vituo vyatya afya vimeongezaka, *population* imekuwa. 4.5 imepitwa na wakati, kwa hiyo, mfike mahali mzingatie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu viwanda vya Zanzibar. Nadhani itakuwa kengele ya kwanza kama sikosei.

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ni ya pili Mheshimiwa, ahsante sana kwa mchango wako. Mheshimiwa Ali Salim Khamis, atafuatiwa na Mheshimiwa Katani Katani, Mheshimiwa Katani Katani yupo? Mheshimiwa Joseph Mhagama atafuatiwa na Mheshimiwa Peter Serukamba.

MBUNGE FULANI: Wa kusokota.

MHE. ALI SALIM KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kunipa fursa ya kuchangia machache katika mapendekezo ya mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hii ni mara ya tatu mimi nachangia mapendekezo ya huu mpango. Lakini kwa bahati mbaya, Waziri wa Mipango anapokuja hapa yale yote ambayo tunazungumza naye anakuwa hayazingatii kabisa.

Kwanza nataka niende katika masuala ya miradi ya kiuchumi ambayo jambo la kufurahisha jana yupo Mbunge mmoja alichangia hapa. Tulisema kwamba tokea awali baada ya dhamira ya kuanzisha miradi hii mikubwa kwa mfano, *Air Tanzania* ni kwa ajili ya uchumi wa nchi na tukasema kwamba tunakubalina kabisa kwamba tunahitaji Shirika la Ndege ili kuweza kunyanya uchumi wa nchi yetu. Lakini ilikuwa lazima tufanye utafiti wa kutosha, tutafute wataalam watusaidie ili tukianzisha Shirika liweze kuwa la mafanikio. Lakini haraka haraka shirika likaanzzishwa, hakuna tatizo, lakini nimwambie Mheshimiwa Waziri Mpango bado hujachelewa, biashara ya ndege ni biashara moja ngumu sana katika dunia, sio Tanzania tu katika dunia biashara ya ndege ni ngumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitaka kujua matatizo ambayo tunayakabili kwa sasa bado shirika letu halijaanza

kazi, ni kwamba tulianza na *Bombardier* lakini baadae tukaja kwenye *Boeing*, lakini leo Kampuni ya *Bombardier* kwa zile ndege za *JET* imenunuliwa na *Air Bus*, angalia sasa kwamba ndege hizi ambazo zinakuja sasa hivi *E220*, wanaozuhudumia sio *Bombardier* tena ni *Air Bus* kwa sababu hiki kiwanda kwa ndege za *JET* hiki kimenunuliwa na *Air Bus*. Lakini pia tuna hiyo *Boeing* ambayo tuna ndege moja tayari na nyingine inakuja mwaka 2020 na *Bombardier* tunazo hizi ndege zao za *Q400* ambazo *Bombardier* bado wenyewe wanazihudumia.

Sasa bado hatujachelewa, ndege zimeshanunuliwa sasa ni wakati wa kutafuta watalaam waweze kulisimamia hili shirika ili liweze kuendeshwa kwa faida, vinginevyo shirika hili litakufa. Kwa sababu leo vitabu vyako viwili vinatofautiana hivi, mapendekezo ya mpango ukurasa wa 14 na kitabu chako hiki ambacho cha hotuba yako uliyoisoma ukurasa wa 27 vinatofautiana.

Kwanza kwenye mapendekezo ya mpango umeelezea hapa kwamba ndege jinsi mlivyozinunua na nini, lakini baada ya kununua hizi ndege ndio sasa mnaenda kutafuta soko la hizi ndege. Hichi ni kitabu chako umeandika wewe mwenyewe vyote vitabu hivi viwili umeandika wewe mwenyewe. Kwa maana baada ya kuliimarisha shirika la ndege lakini pia ndio mnaenda kutafuta masoko sasa ya kuweza kufanya hii blashara ya ndege. Lakini huku unasema kwamba kwenye kitabu hiki cha mapendekezo ya mpango ambacho tulipewa kabla inasema kwamba ndege hizi zitaanza kwenda katika miji hii ambayo imetajwa hapa Bombay, Bujumbura, Guangzhou na Entebe. Lakini kitabu hiki ambacho wewe ulichotusomea hapa Bungeni, kinasema kwamba miji ambayo ndege yetu itakwenda ni Mumbay, Bujumbura, Guangzhou na Entebe. Sasa sijui kipi ni sahihi kati ya hivi viwili, kwa hiyo, naomba uangalie zaidi ili uone tujue wapi pana usahihi na wapi hapana usahihi. (*Makofi*)

Kwa hiyo, hilo ni jambo moja ambalo ninakushauri kwa sababu hili shirika mmetumia fedha nyingi sana kwa ajili ya kuliimarisha, kwa hiyo, kama mnataka lifanye faida na

linyanyue uchumi basi inabidi sasa patafutwe watu ambao ni wataalam, tuwape kazi hii ili watufanyie *reform* ya shirika letu. Lakini pia utakapokuja hapa utuambie hili shirika baada ya kununua hizi ndege, ni baada ya muda gani litaweza *break even* ili tujue kwamba tunakokwenda ni wapi. Kwa hiyo, naomba kwamba utakapokuja kuhitimisha hoja yako ile *business plan* ambayo mnayo mtuambie baada ya miaka mingapi shirika litakuwa limerejesha ule mtaji na lianzé kutengeneza faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ni kwamba katika mpango huu ambao ameuleta Mheshimiwa Waziri, hakuna kipengele hata kimoja kinachoonesha Zanzibar kimo katika mpango huu ili kuiendeleza Zanzibar na mara nyingi tumesema toka tumetaka kuanza bajeti ya mwaka 2015/2016 tumesema kwa nini haitafutwi japo mradi mmoja au miwili au mitatu ambayo inakuja katika mapendekezo ya mpango kwa ajili ya Zanzibar? Kwa nini kuna tatizo gani? Tatizo gani ambalo linatusababishia mpaka leo kila siku tuzungumzie Zanzibar kwenye mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba huu mpango kwa sababu ni mapendekezo ya mpango utakapoleta mpango halisi basi tuone kwamba Zanzibar, kuna mradi gani wa kiuchumi ambao utaweza kuisaidia Zanzibar. Halafu ukiangalia sisi Zanzibar tuna bahari kubwa tu na sasa hivi mwezi huu nafikiria mwishoni mwa mwezi kuna fanyika mkutano wanaita *blue economy* ambao unafanyika Kenya, ambao unahusisha mazao ya bahari unakwenda kufanyika, sasa kwa nini basi kusifanyike utafiti wataalmu wako, wasifanye utafiti wakaona kwamba kuna eneo hili mahususi la Zanziba likaweza kukuza uchumi wa Zanzibar kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia la mwisho niseme kwamba Mheshimiwa Mpango katika Bunge liliopita baada ya kutoa maelezo ya mwelekeo kuhusu deni la Zanzibar katika masuala ya *TANESCO* iliposemwa hapa ulitoa maelezo mazuri sana na Mheshimiwa Spika akakubali, na tukakubaliana kwamba Bunge hili likija hii *VAT* kwenye deni la umeme,

iondolewe lakini kwenye miswada hii imekuja hapa halikuondolewa hili suala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikwambie Mheshimiwa Mpango najua masuala yote yanapitishwa kwenye *cabinet*, lakini suala hili ujachukua juhudzi za makusudi kuhakikisha ili jambo lina malizika, wewe mwenyewe *personally* hujachukua juhudzi za makusudi kwa sababu sisi tunazungumza na viongozi ambao wa Zanzibar ambao unafanya nao mawasiliano, lakini ujachukua ile juhudzi ya makusudi ya kuonesha jambo hili lina malizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mtuambie kwamba sisi Zanzibar siyo ndugu zenu, ndugu zenu ni watu wa Rwanda, Kenya huko na Zambia hao ndiyo jamaa zenu sisi hatumo mionganini mwa Taifa hili ili tuijuwe haiwezekani kwamba *priority* anapewa kutoka Rwanda au kutoka Kenya lakini Zanzibar, anaonekana kama ni mtumwa tu analitumikia hili Taifa. Huu ukoloni utaisha lini? Sisi tumeungana hapa kwa nia njema kabisa, lakini leo sasa hivi, mnaanza kutubadilishia maneno mnatufanya kama sisi watumwa wenu tu, wala hamjali tukipiga makelele.

Mimi nawashauri Wazanzibari wenzangu kwamba sasa ni afadhali tutafute njia ya kutafuta umeme sisi wenyewe badala ya kuja kumpigia magot...
(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa muda wako umeisha, kengele ya pili imegonga.

Waheshimiwa Wabunge nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Joseph Mhagama, atafuatiwa na Mheshimiwa Peter Serukamba na Mheshimiwa Lathifah Chande ajiandae.

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kukushukuru kwa kunipa hii nafasi ya kuchangia Mapendelekezo ya Mpango ya Taifa 2019/2020. (*Makofii*)

Kwanza nimpongeze kwanza Mheshimiwa Waziri Mpango na nimpongeze sana Mheshimiwa Rais na Serikali ya Awamu ya Tano, katika ujumla wake kwa kuwa *consistency* katika kipindi hiki chote cha miaka mitatu kwa sababu mpango huu ni sehemu ya mpango mzima wa miaka mitano 2015/2016 - 2020/2021 na katika utekelezaji wake Serikali imekuwa *consistency* sana.

Pia nipongeze Serikali kwa kuzingatia maoni ya Wabunge kwa miaka yote mitatu ambapo tumekuwa tunatekeleza mpano huu. Maeneo kadhaa ambayo tulikuwa tunashauri yakiwemo maeneo ya kuongeza nishati tumeona *Stiegler's Gorge* imeendelea kupewa kipaumbele lazima tuipongeze lakini pia tumeona leo Liganga na Mchuchuma, inaanza kupata sura ya utekelezaji kwa maana kwenda sasa kujenga kiwanda cha kufua chuma Liganga. Sasa haya yote ni mapato ya kazi ya Bunge hili na nimatokeo ya kazi nzuri ya Awamu ya Tano, na lazima tuipongeze Serikali na kwa namna ya pekee Mheshimiwa Rais na Waziri Mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la kukua kwa uchumi wote tumejiridhisha pasipo mashaka uchumi wetu unakua kwa kasi kubwa sana na ukilinganisha na uchumi unavyokuwa duniani na uchumi unavyokuwa katika Afrika na maeneo mengine tunayopakana nayo sisi tunakuwa kwa kasi kubwa sana, kasi ya asilimia 7.2.

Sasa hili kimsingi kuna eneo dogo linatupa shida kidogo sisi Wabunge lakini Watanzania katika ujumla wake kwamba uchumi unakua, lakini mapato ya kukuwa uchumi huu tunayaona kwenye maeneo ya afya, tunaona kwenye masuala ya elimu, tunaona kwenye masuala ya miundombinu. Kwa hiyo, kimsingi faida za kukua uchumi huu tunaziona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ambayo mimi nilitaka nitoe mapendekezo, ya kuboresha wakati wa maandalizi ya huu mpango ni namna gani sasa kwa sababu mimi nina amini hatuwezi kupata mapinduzi ya uchumi kama hatutakuwa na mapinduzi ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilitaka nijaribu kushauri kwamba sasa Mheshimiwa Mpango akae na hizi *line ministry* zinazogusa sekta ya kilimo na uchumi kiujumla kuona namna gani sasa tunaweza ku-transform agricultural sector kwa namna ni *significant*. Waatalam wa kilimo wanapo takaa kujua changamoto kwenye sekta ya kilimo wanafanya upembuzi wa mnyororo wa thamani ya mazao ya kilimo na ukifanya upembuzi wa mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo katika ujumla wake utagundua kwamba tatizo kubwa kwenye sekta ya kilimo ni soko, yaani huo ndio mtego tunao na Serikali sasa lazima ikubali kwamba huo ndio mtego ambao tunao na tukiweza kuutegua huo sekta ya kilimo itakuwa kwa kasi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye huu mpango nashukuru Serikali imeweka vizuri sana *interventions* nydingi kwenye sekta ya kilimo, lakini utaona kwenye *interventions* zilizopendekezwa na Serikali kwenye mpango huu hazoneshi kwa usafaha namna gani tunaenda tunaenda kutatua tatizo la soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachomfanya mkulima aende shambani ni faida anayoipata kutokana na kilimo. Tumejiridhisha kwamba kwa namna yoyote ile kwa mazingira aliyopo mkulima huyu mdogo lazima achangie kwenye usalama wa chakula, lakini lazima atengeneze fedha kwa ajili ya kujikimu. Sasa *strategyya* Serikali lazima izingatie ukweli kwamba kumsaidia huyu mkulima mdogo apunguze gharama za uzalishaji na gharama za uzalishaji kwanza zinatokana na bei kubwa ya mbolea, nashukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu jana alieleza namna gani tunajipanga kupunguza gharama ya mbolea kwa kuzalisha mbolea yetu ndani, hilo litamaliza tatizo lakini kwenye mpango huu alijafafanuliwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini eneo la pili ni *transaction cost* kutoka eneo lile ulilozalisha mpaka kufika kwenye maghala ya kuhifadhiya mazao, barabara zetu vijiji hazileti tija kwa mzalishaji, eneo dogo la usafirishaji analipa gharama kubwa sana za kusafirisha mazao yake,

anapofikisha zao lake kwenye eneo la soko tayari garama zimeshakuwa kubwa. Kwa hiyo anapokutana na bei ndogo, *profit margin* inabaki kuwa ndogo sana au anaweza asiipate kabisa. Kwa hiyo, Serikali iwekeze kwenye kupunguza gharama za uzalishaji kwa kupitia pembejeo zetu, mbegu bora na mbolea, lakini pia miundombinu ya masoko, na miundombinu ya masoko ndiyo hizo barabara za vijiji ni zinatoka mashambani lakini madaraja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine baya linalochangia upotevu mkubwa wa mazao tunasema *post harvest losses* ni haya hadhi na sura ya maghala yetu na gharama za usafirishaji (miundombinu ya usafirishaji) asilimia 30 ya mazao yetu tunayoyazalisha yanapotea kabla hayajafika kwenye soko, sasa hiki kiwango kinacho potea nacho ni hasara kwa mkulima. Kwa hiyo pamoja kwamba hatuwezi kumsaidia mkulima kupata bei nzuri kutokana na hali halisi ya soko la dunia tunaweza kama Serikali kumwezesha huyu kuzalisha kwa gharama za chini na hii *profit margin* yake ikabaki kubwa na akawa ana visenti vya kwenda shambani. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliomba nimshauri Mheshimiwa Mpango na Serikali katika ujumla wake katika eneo hilo na ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja, ahsante. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Peter Serukamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Lathifah Chande ambaye atachangia kwa dakika tano na Mheshimiwa Innocent Bashugwa ajiandae.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nianze kwa kumpongeza sana Waziri wa Fedha na timu yake kwa mpango huu mzuri sana. Mpango huu mimi naukubali wote kama ulivyo shida yangu mimi ipo kwenye *ku-finance* kama kuna eneo tukubaliane vizuri ni namna ya haya tuliyoyapanga tutayatekeleza namna gani? Hapa kwangu mimi ndiyo napaona ukienda *page* ya 50 na mwenyewe

amesema mpango huu unatarajiwa kugharimiwa na sekta ya umma na binafsi kupelekea uwekezaji wa moja kwa moja au kwa njia ya ubia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma mipango yote sijaona popote ambapo tunajadili kama miradi hii itatekelezwa kwa ubia ama miradi hii itatekelezwa na *private sector* na mimi Mheshimiwa Waziri hili ninaliamini nitalisema kila nitakapo simama, nina amini iko miradi ingeweza kutekelezwa na *private sector* na bado tukapata mambo mazuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, duniani kote ukienda, China, Malaysia, kote nchi zimeendelea juzi wanatumia sana *PPP* kwenye miradi mingi hasa hii ya kiuchumi. Kwa bahati mbaya sijaelewa tunatunga sheria na juzi umeleta sheria nzuri sana, lakini sioni miradi ambayo tuna *i-push* kwa ajili ya *PPP*. Kwa mfano, barabara ya kutoka Dar es Salaam kuja Chalinze utmeongea huu mwaka wa 10 ambao mimi ninaamini barabara hii tukiamua *ku-push* tutapata mtu wa kujenga na kwa kweli tukitafuta *private sector* kitakachotokea tutapata fedha nydingi ambazo tutapeleka kwenye *social services* kwa maana ya elimu, kwa maana ya maji, kwa maana ya afya na tutapandisha mishahara ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama tutaamua miradi yote hii mikubwa tunafanya kama Serikali peke yake, madhara yake yako kwenye *social services*. Mipango hii ni mizuri sana kwa hiyo mimi ningeomba Mheshimiwa Waziri jambo hili kubwa na miradi hii umeipana vizuri, vipaumbele ni vizuri lakini umefika wakati tubadilishe *mindset* yetu, twende kutafuta watu tutakaosaidiana nao kufanya miradi hii ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme, pamoja tunaenda kutengeneza umeme mwingi sana mimi nakubali jambo kubwa, lakini tufanye *energy mix*, tukipata mtu mwingine akazalisha kwenye sua, akazalisha kwenye upepo, akazalisha kwenye *gemotheo*, sisi tunazalisha kwenye maji maana tutakuwa na umeme mwingi kama Taifa labda *megawatts*

5,000/10,000 ambao tutaanza ku-export na mwingine tutatumia ndani, lakini bado tutakuwa tume-achieve kama nchi, lakini tukitafuta kitu kimoja tu mimi nasema ningeomba sana umefika wakati tujandiliane suala la kutumia *private sector*. Lakini *private sector* ije Tanzania cha kwanza lazima sheria zetu ziwe *predictable*, pesa zetu za kodi ziwe *predictable* kila kiwe kinaaminika, lakini kama tunabadilisha magoli kila siku ni kweli baadhi ya *investors* hawawezi kuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hawana hakika kesho tutafanya nini? Kwa hiyo mimi nina amini nchi yetu ina *resorce* nyingi sana, Mungu ametubarikia kila tu, naombeni sana imefika wakati tutumie *private sector*ili tuweze kwenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la kilimo tunakiongea sana hapa ndani, lakini mimi nasema kilimo tulichoongea miaka yote jambo moja Serikali naona hatufanyi kwa nini nimesoma humu ndani, hatuongelei *commercial farming*, bila *commercial farming* matatizo ya kilimo hayatakwisha, matatizo yote ya kilimo yatatatuliwa na mashamba makubwa, sisemi tunyang'anywe mashamba. Mungu katupa ardhi bado ardhi hii watu watakuja wenye uwezo mkubwa. Mtu mwenye shamba lake kwa mfano hili jambo la korosho hivi kwa mfano mtu ambaye ana hekari 10,000; amelima korosho zake hawezi kumtafutie soko ninyi, hata ombo pembejeo, kwa hiyo nasema tufike sehemu haya mawazo kila mtu anaweza akalima, haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema tumeanza ku-*push command economy* hata hili la korosho, naomba mimi mwenzangu silielewi sana, Serikali ituache *demand and supply* ifanye kazi. Serikali kuingia ku-*detect terms* sio sawa, ndiyo matokeo yake wataingia watu katikati, watatuvuruga. Bei kuanguka za mazao imekuwepo hivyo duniani, kote kwa sababu inategemea soko la dunia. Lakini tuongelee zao moja, watu wa mahindi hali ni mbaya, mtama hali ni mbaya, kahawa hali ni mbaya, chai hali ni mbaya, *why?*

Kwa hiyo, mimi nasema ningeiomba Serikali jambo hili tuache *market force* ndizo ziamue bei, ikitokea bei safari hii imekuwa mbaya mwaka kesho mnatafuta namna kutoa *incentive* ili kuwainua wakulima, lakini tunaanza kuangaika wote just because kuna eneo moja mazao yameanguka haiwezekani? Kwa sababu bajeti ya kununua tunaitoa wapi? Tukiamua kununua sisi tunatowa wapi bajeti? Bajeti tumeipitisha hapa ndani kwahiyio, mimi ningeiomba Serikali tuache *market force* *zi-determine* biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Serikali, tuache biashara tupo kwenye soko huria, kurudi kwenye *command economy* maana yake itabidi tuanze kuleta tume ya bei, tukileta tume ya bei, tukileta tume ya bei tutarudi kule kule, wako watu wanasema *tu-own* sisi unajuwa maana on lazima uweke mtaji, ukipata hasara lazima uweke mtaji mwingine, kitakachotokea tutashindwa kufanya yale makubwa ambayo ni ya Kiserikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la watu wa *TRA, task force* nilishalisema huko nyuma, jamani naombeni biashara zinafungwa, niwaombeni biashara ni mahusiano. Mwaka 1987 Mahathir aliulizwa na Rais Mwinyi kwanini Malaysia inafanya vizuri, jibu lake ilikuwa nini? Wakiwa kwenye *Commonwealth* ya Zimbabwe akasema mimi ninafanya vizuri kwa sababu kuna asilimia 30 ya kila anayefanya biashara kwenye Malaysia yangu.

Kwa hiyo ninachosubiri ni asilimia 30 kazi yangu ni kuweka mambo mazuri ili tupate asilimia. Juzi ameingia at 94 anaulizwa anasema shughuli yangu mimi ni kulinda 24 percent kwamba wafanyabiashara anawawekea mazingira mazuri wao ndiyo *partners* wangu na sisi *partners* wetu ni wafanyabiashara, tunalo jukumu la kuwalinda, tunalo jukumu la kuweka mazingira mazuri ili wakifanya vizuri tutapata faida asilimia kubwa itaongezeka nchi itaenda mbele.

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Lathifah Chande dakika tano atafuatiwa na Mheshimiwa Innocent Bashugwa, nadhani kutakuwa kumebaki nafasi ya mtu mmoja Mheshimiwa Mohamed Shabiby, sijui kama kaenda msikitini ama.

MHE. LATHIFAH H. CHANDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kitu kinachoonyesha Serikali hii kwa kupanga tuu inajua kupanga, lakini kwenye kutekeleza, ipo shida, mipango ipo mingi lakini utekelezaji ni shida sana sana. (*Makofii*)

Kwanza ningeanza kuongelea suala la nishati. Tulikuwa na mradi wa nishati kwa kutumia gesi, mradi huo ambaao bahadhi ya ndugu zetu ndugu zangu wa Kusini (Mtwara na Lindi) waliandamana na hata tulipoteza baadhi ya ndugu zetu na wengine walifunguliwa kesi, wengine wallikimbia nchi kwa ajili ya huo mradi. Mradi huu ultumila takribani hata zaidi ya trillion 1.2; lakini pia wananchi walilazimika kuacha makazi yao, mashamba yao na kushindwa kuendelea na kazi kwa ajili ya kujinua kiuchumi na mpaka leo hii baadhi yao hawajalipwa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunaona Serikali ya Awamu ya Tano inaenda kuua ule mradi wa gesi, imekuja na mradi mpya wa *Stieger's Gorge*. Mradi huu ambaao kwanza kwa taarifa tuliyopewa utaenda kugharimu pesa nyingi zaidi kuliko ule mradi wa gesi, tumeambiwa mpaka kumalizika huo mradi inaweza ikatumika takribani trillions saba na hadi sasa zimetengwa, bilioni 700 kwa maana hiyo hadi kuja kumalizika itakuwa ni ndani ya miaka kumi, kwenye hatua za awali tu tayari imetumika bilioni 700.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi naijuliza, huu mradi kuna kitu gani mpaka tunalazimishia uendelee pamoja na kwamba wataalam wametuambia kuna athari nyingi zitakazoenda kujitokeza kwenye mazingira, lakini bado tunataka kuendeleza na huu mradi, tuna *option* nyingi za kuweza kwenda nazo, kwanza kuna hiyo gesi ambayo tayari tumeshatumia fedha, lakini pia vilevile kuna upepo, kwa sababu huu mradi wa *Stieger's Gorge* kama ni *megawatts*

umeme utakaowea kuzalishwa ni *megawatts* 2,100 ukiangalia mradi wa upopo unauwezo wa kuzalisha umeme wa *megawatts* mara nne na zaidi wa huu hapa wa *Stieger's Gorge* kwani kuna kitu gani hasa kwenye huu mradi wa *Stieger's Gorge* tunahitaji kujuua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakumbuka vizuri kabisa, wakati tupo kwenye kipindi cha Bunge la Bajeti, Waziri wa Mazingira, Mheshimiwa Januari Makamba, Serikali itakuja kufanya tafiti kujuua hizo athari, lakini cha kushangaza wenye hili hapa huu mpango tunachokiona hakuna pesa yoyote iliyotengwa kwa ajili ya kufanya hizo tafiti juu ya hizo athari zinazoweza kujitoneza. (*Makofii*)

Sasa na juzi tumemsikia kabisa Rais Magufuli akisema kwamba huu mradi utaendelea kufanyika na ametupilia mbali zile *information* ambazo zipo *bian stone research*. Sasa tunataka kujuua tunaendea na huu mradi kwa *research* gani ilifanyika na Serikali? Kama kuna *research* imefanyika basi tulitewa tuweze kujadili hapa ndani Bungeni. Kwa sababu sielewi kwa nini tunaendeleza kitu ambacho kwa asilimia kubwa itatuletea sisi wenyewe athari nyingi, na ukikaa ukiangalia huu mradi *there is no sustainability* kwa sababu kama ni maji, maji yatafika wakati yatakwenda kuisha, kwa sababu maji yanatumika na wanyama, mimea, binadamu wote tunategemea kutumia haya maji. Kwa hiyo ikifika sehemu maji yameisha tunafanyaje? (*Makofii*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa kengele imegonga. Mheshimiwa Innocent Bashungwa atafuatiwa na Mheshimiwa Richard Mbogo.

MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti Asante sana kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia mapendekezo ya mpango wa Maendeleo ya Taifa 2019/2020.

Mheshimwa Mwenyekiti, nianze kwa kuungana na Waheshimiwa Wabunge wengi waliochangia kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Pombe Magufuli kwa utendaji wake wa kazi mzuri, ametimiza mwaka wa tatu lakini tumeona Mheshimiwa Rais wetu akitekeleza kwa vitendo ule usemi kwamba penye nia pana njia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea kumpa moyo Rais wetu na tuombe Watanzania waendelee kumuunga mkono ili miradi mikubwa ya maendeleo ambayo Rais wetu ameonesha kwamba Watanzania tukithubutu tunaweza tuweze kuiitekeleza iweze kusaidi kizazi hiki na vizazi hii na vijavyo.

Mheshimiwa Mweyekiti, pia nitumia nafasi hii kumshukuru Waziri Mkuu hivi karibuni alitembelea Mkoa wa Kagera kuangalia mwenendo wa msimu wa kahawa. Mheshimiwa Waziri Mkuu aliweza kutatua changamoto nydingi katika ziara, lakini pia alitoa maelekezo ya namna bora ambayo Serikali inahitaji kujipanga ili msimu ujao wa kahawa wakulima wetu waweze kufaidika na kilimo cha kahawa na katika hilli niweze kushauri Serikali badala ya kusubiri msimu ukikaribia ndipo twende kwenye kukabiliana na changamoto za msimu basi *on quarterly basis* Serikali iwe inaita wadau, tunajadili namna ya kujipanga vizuri ili msimu wa kahawa na wa mazao mengine unapofika basi tujikite kwenye kutekeleza na kusimamia mazao haya ya blashara ili yaweze kuwasaidia wakulima lakini yaweze kuchangia kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimshukuru sana na nimpongeza Mheshimiwa Waziri Dkt. Mpango pamoja na shemeji yangu Dkt. Ashatu kwa mapendekezo kama rasimu, nasema kama rasimu kwa sababu ni mapendekezo bado na sisi Wabunge tuna nafasi ya kuboresha na nitumie nafasi hii kuwapongeza sana Kamati ya Bajeti hata muda wangu usipotosha, Kamati ya Bajeti wamatoa mapendekezo mazuri naunga mkono asillimia mia moja naamini Mheshimiwa Waziri kama mkiachukua yale pamoja na mapendekezo mazuri ya Waheshimiwa Wabunge basi tutakuwa na mapendekezo ya mpango mazuri sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo nianze kuchangia mapendekezo ya mpango kuhusu suala la ufungamanishaji wa uchumi na maendeleo ya watu na nita-*argue* katika sehemu tatu ambazo ili tuweze kufungamisha uchumi na maendeleo ya watu lazima tuwe na Taifa lenye afya na nguvu kazi. Na katika hili niipongeza Serikali katika sekta ya afya Serikali imefanya kazi nzuri kwenye vituo vya tiba kote nchini dawa inapatikana na Serikali tunaona ikiendelea kujenga vituona katika hili Mheshimiwa Waziri kwa vile tupo kwenye mapendelezo ya mpango basi vile vituo vya afya viwili vya Nyabioza na Kanoni katika Wilaya ya Karagwe vile kwenye mapendekezo ya mpango. (*Makofii*)

Mheshimwia Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ningependa kusisitiza na kuipongeza Serikali ni kuleta Mamlaka ya Maji Vijijini. Na katika hili Mhemimiwa Waziri tuombe sana Serikali pia ingalie kuwa kama kuna uwezekana zile shilingi 100 ambazo zinatoka kwenye mafuta zinaenda kwenye barabara kwa sababu ya umuhimu wa kuwatua akina mama ndoo nchini basi ikiwezekana iwe 75 kwa 75 halafu tukimaliza changamoto za upatikanaji wa maji safi na salama nchini turudi tena kwenye ile *ratio* ya 100kwenda kwenye mchango wa barabara na 50 kwenda kwenye mfuko wa maji hii itasaidia kutatua changamoto ya maji nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kuchangia na kusisitiza sana pamoja na jitihada nzuri ya Serikali elimu bila ada lakini bado kuna changamoto kubwa ya upungufu wa madarasa, upungufu wa matundu ya vyoo, maabara katika shule za sekondari hazikamilika na hosteli kwa ajili ya vijana wetu wasichana. Sasa nipende katika kwenye mapendekezo ya mpango hili mlione ni jambo muhimu sana kwa sababu *CDG* haziendi lakini Serikali kuititia vipaumbele tumeona hela ikienda kusaida kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo kwenye sekta nilizozitaja, lakini tukumbuke kwamba kuna miradi viporo upande wa zahanati, upande wa shule na kwenye mapendekezo haya basi tuiombe Serikali iangalie kwa uzito huo kama tulivyofanya Mheshimiwa Rais aliyosimamia zoezi la madawati nchini basi hali kadhalika twende kufanya hivyo kwenye shule za msingi,

matundu ya vyoo na maabara kwa ajili ya sekondari nchini.
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kuchangia ni haya mazao ya vipaumbele. Kuna wengine wamezungumzia takwimu ya *post harvest losses* asilimia 30 ya mazao ya wakulima yanaharibikia mashambani. Lakini ukienda viwanda Mheshimiwa Mwenyekiti viwanda vinahitaji malighafi za wakulima hawa Kamati ya Viwanda na Biashara tulivyotembea viwandani sasa hivi *robbot* ndizo zinafanya kazi zime-replace ajira za Watanzania, lazima ajira hizi tuzitengeneze kwenye sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti lakini ukiangalia *post harvest losses* asiliamia 30 mkulima anahangaika lakini zao lake 30% linaharibika shambani na huku viwandani wanahitaji hizi malighafi nitolee mfano...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA: Kengele ya kwanza au ya pilii?

MBUNGE FULANI: Ya pilii.

MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA: Eeh, naunga mkono hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Bashungwa kwa mchango wako, Mheshimiwa Richard Mbogo.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi, napenda niipongeze Serikali na Waziri pamoja na timu yake nzima kwa namna wameweza kuandaa mpango huu na niseme tu katika changamoto ambazo amezieleza kutokana na utekelezeji wa mpango amekwa wazi na sisi kama Wabunge tunahitaji kumsaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili uweze kutekeleza mpango au bajeti tunaangalia mapato na matumizi, na katika upande wa mapato ili kuweza kuongeza mapato maana yake utaongeza bei au *rate*, utaongeza ushalishaji au utaongeza vyanzo vipyta ya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nianze na masuala ya kodi, kwanza niombe Serikali au Wizara husika ule muda wa makampuni au taasisi mbalimbali kuitia malimbikizo ya madeni ya riba kwenye kodi badala ya tarehe 30 Novemba muongeze na watembelee makampuni mbalimbali ili watu waitikie na walipe malimbikizo ya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna suala la kuongeza bei kwenye maeneo mbalimbali mara nyigi mwezi Juni kwenye *Finance Bill* ndio tunaletewa maeneo ya mapendekezo. Lakini ningependeza kipindi hiki cha mpango hebu Waziri awe anatupa maeneo anayotarajia kuongeza ili tuwe na nafasi nzuri ya kuweza kushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba kwa namna ya pekee kabisa tuumie Watanzania lakini tupate huduma, naomba tuongezee shilingi 50 kwenye kila lita ya mafuta ili iende kwenye maji. Kwa sababu gani napendekeza, miradi ya maji ikishatengenezwa *maintenance* inaachiwa kwenye jumuiya ya watumia maji watabaki wana-*maintain* wenyewe, tofauti na *Road Fund* kila mwaka zinatoka fedha za ukarabati lakini mradi wa maji ikisha tengenezwa *COWOSO* ndio inakuwa na wajibu wa *ku-maintain* kwa hiyo kama Serikali tukiruhusu hii shilingi 50 tukaongeza ikaenda kwenye maji itasaidia kwenye miradi ya maji ambayo ndio changamoto kubwa ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulifanya mabadiliko sheria ya fedha *produce cess* tukashusha kutoka asilimia tano kwenda asilimia tatu, lakini kimsingi kwenye mazao ya biashara kama tumbaku hatujamnuifaisha mkulima kwa hiyo hii tumenuifaisha mnunuzi. Kwa hiyo niombe Serikali muone namna gani vya *ku-review* hii punguzo kutoka asilimia tano kwenda asilimia tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusu service levy. Halmashauri nyingi hazipati service levy kutoka kwa wa wakandarasi wanaotengeneza barabara ambao wapo chni TARURA na chini ya TANROADS kwa hiyo mapato kwenye halmashuri hayakuwa hayafikii malengo vilevile kampuni za simu ambazo zimeweka minara sehemu mbalimbali nchini bado Halmashauri zetu hazipati mapato upande ya service levy. Kwa hiyo tunaomba kama Serikali muweze kuangalia maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu hii ya tano tunapongeza sana kwamba tutakuwa na uchumi upande wa viwanda, lakini kuna viwanda hapa Tanzania kuna viwanda vinalishwa kwa 90%; 75% kutoka nje ya nchi. sasa kama Serikali nini mkakati kwa mfano kwenye ngano Bakiresa 95% anaingiza toka nje, sasa tuna mkakati upi wa kuweza kuwezesha akapata malighafi hizi toka Tanzania ambapo tutatengeneza ajira humu ndani tutakusanya mapato ya kodi mbalimbali, sasa nini kifanyike tutaomba Serikali ingalie na upande hata wa mafuta 75% tunaingiza kutoka nje. Kwa hiyo, dola ambazo tunalipa kwenda nje ni nyingi kuliko tunazozingiza kutokana na *export*, kwa hiyo *balance payment* inakuwa ni *negative*, kwa hiyo hii inatuathiri uchumi wetu.

Kwa hiyo, tunaomba pia kwenye upande wa kilimo wananchi wengi wanatumia jembe la mkono. Sasa ni lini tutawatoa hii benki yetu ambayo tumeanzisha kwa ajili ya kuendeleza kilimo inaenda kusaidia namna gani maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye upande wa Balozi zetu, nchi nyingi duniani tuna Balozi nyingi lakini ni jinsi gani kama kama Serikali tunazitumia hizi Balozi kwenye kupata wawekezaji na kuangalia fursa zilizopo kwenye nchi mbalimbali duniani. Tumeona Balozi nyingi hatujapata taarifa yake kamili lakini hatuzitumii vizuri na hata Balozi zingine zinahitaji taarifa toka huku nchi hazibivi kwa wakati miezi miwili/miezi mitatu kwa hiyo tutumie vizuri hizi Balozi tuweze kukuza uchumi wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la sekta binafsi na sekta isiyo rasmi, mwaka juzi ilipitishwa na mwaka jana wakati wa bajeti ilitoa taarifa kwamba watapewa vitambulisho watambulike na waingie kwenye kuchangia kwa maana kwamba walipe kodi, sasa changamoto Waziri ameileza kwenye kitabu chake kwamba imekuwa ni ngumu, sidhani kama sisi wanadamu au Serikali ikiamua jambo linaweza likashindikana.

Kwa hiyo, tukiweka vitambulisho na maeneo husika na hata wale wanaotembea kama vitambulisho wataweza pia kuhusishwa vyema nakuweza kulipa kodi na staiki zingine zote za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna masuala ya mashirika ya Serikali ambapo yana zaidi ya 50% na mengine chini 50%. Kuna kampuni kama *TTCL* inahitaji udhama wa *concession loan*, inahitaji Serikali iweze kusaidia kuwekeza. Mchango karibuni na Serikali dora 231,000 sasa ni lini Serikali itaoa fedha kwa Kampuni ya *TTCL* ili ingie kwenye ushindani, ipate faida na Serikali ipate gawio kama ambalo ndilo kusudio. Na *ATCL* tunashukuru shirika limefuliwa vizuri lakini *ATCL* inahitaji jicho zaidi, ipate *discount* kwenye *government bill* kwa mfano *land fees*, mambo ya *navigation* wapunguziwe kama *nation flag* ili waweze kukua zaidi na zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la utalii kama ni Tanzania tuna vivutio vingi je, ni lini mchango wa utalii utaongezeka kwa kiasi kikubwa katika kukuza pato la Taifa. Tunaona nchi za wenzetu wanapata mapato mengi kwenye utalii lakini vivutio ni chache sana. Sasa tuombe Wizara ya Maliasili ya na Utalii kwa kushirikiana kwa ujumla kama kuna msaada wa Wabunge, msaada wa maeneo mbalimbali watuneshe mkakati utalii utaenda kuongeza mapato kwa kiasi kikubwa na nchi ambazo watalii wengi wanapatikana tufanye mawasiliano...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa kengele mbili zimeshagonga. Tutamalizia na Mheshimiwa Anatropia Theonest kwa dakika tano.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru, kuna wachumi wa *IMF* waliwahi kusema, waliandika *paper* yao moja wakijibu walikuwa wanaulizwa maswali ni fedha kiasi gani nchi inahitaji kukopa; anasema *how much a debt is sustainable?* Maana tumekuwa na maeneo mengi kuwa deni letu ni himilifu ni toshelevu sasa katika hiyo *paper* yao ambayo waliandika walijibu kwamba kwa kiswahili wakisema; *they don't know* kwamba hawajui ni hela kiasi gani au ni *debt* kiasi gani ya Taifa ambayo ni *sustainable* na wakenda mballi zaidi wasema *market signals don't work as should;* kwamba zile *sign* za soko *some time* hazipo *predictable* nadhani na hiyo nimwambie Mheshimiwa Dkt. Mpango *sometimes market signal* haziko *predictable.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza kuwa tunajiamini kwamba deni letu ni himilivu, deni la Taifa linalipika hana anayebisha kwa sababu tunaona uchumi unakua kwa mujibu wa takwimu zetu kwa maana ya *GDP* bado ina *tolerate* mkopo tuliao nao, lakini swali tunajiuliza kwa nini hii mikopo inakuwa kwa haraka. Sikatai kwamba tunakopa fedha nyingi kwa ajili ya kenudesha miradi yetu mikubwa inayoendelea lakini ushauri wangu nitakao utoa sasa tuangalie hizo fedha tunazozikopa katika miradi tunayoweka, je, itaweza kutupa fedha kwa wakati mfupi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakopa kwa ajili ya kuwekeza kwenye miradi ambayo ni ya muda mrefu hatuna uhakika kama tunaweza kufuna haraka haraka hiyo hiyo naleta kwenye mradi mkubwa tunaouendesha kwenye *SGR*. Huo mradi mkubwa tunaouendesha ambao sisi humu Bungeni tumekuwa tukipiga kelele kwa ajili ya kufufua mradi mkubwa wa chuma wa Liganga na Mchuchuma nimepitia kwenye kitabu chako mmesema mnakamilisha taarifa za awali, nani

hajui kwamba kukamilika kwa mradi mkubwa chuma ndio ungesaidia pakubwa katika mradi mkubwa wa *SGR*, nani anabisha katika hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha tunazozidi kukopa kwa wahisani au wafadhili tukaiwekeza kwenye kujenga *SGR* tungeweza kuwekeza kidogo kama tungekuwa tunazalisha sisi chuma hapa nchini. Lakini kama haitoshi tungeweza kupata faida zaidi hata fedha kigeni kwa kuuza chuma lakini badala yake mradi ambaao umekuwa kipaumbele 2015/2016 leo inapewa *that half a page* ndio inazungumziwa na dhani Waziri atupe *status* leo kuna mwekezaji alijitokeza nadhani anaitwa Szechuan Onda akija na *terms* zake atuambie amefikia wapi *as far as concern* kuwekeza katika huu mradi ambaao kimsingi ndio mradi wenye kielelezo na unapaswa kuwa kipaumbe kwa nchi yetu kwa nchi yetu kama tunamaanisha tunakata uchumi ukue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninarudia tena kusema tusijamini sana kusema kama deni letu ni himilivu kama tunaenda kuwekeza katika vitu ambavyo havitawenza kupandisha *GDP* yetu haraka sana ikiwa ni pamoja na mazao ambayo tutazalisha au uchumi tutakaoweza kuu-*nature* ukaweza ku-*support export* ndio itasaidia deni letu lizidi kuwa himilivu. Hao Wakenya leo ambaao wanakaribia ku-*default* na wao walikuwa najinasibu kama tunavyoongea leo kwamba deni lao lilikuwa himilivu na kama haitoshi *GDP* ya Kenya iko juu kuliko ya kwetu, lakini nini kinatokea ni lazima tuijangalie wanasema ukitaka kuruka ni lazima uagane na nyonga, kwa hiyo sasa tungalie vipaumbele vyetu vya kiuchumi *in relation to* deni la Taifa hiyo ni ya kwanza, lakini ya pili, nina muda mchache, Serikali...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzmjii)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa. Katibu.

NDG. ASIA MINJA - KATIBU MEZANI: Bunge linarudia.

MWENYEKITI: Bunge linalrudia.

(Bunge Lilitrudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tukae.

Tumefika mwisho la wa kipindi cha asubuhi, niwatajé Waheshimiwa Wabunge wachache ambao watachangia mchana ambao wamesalia, tunae Mheshimiwa Katani Katani, Mheshimiwa Willy Qambalo, Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, Mheshimiwa Peter Lijualikali, tunae Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed, Mheshimiwa Ahmed Shabiby, Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Lollesia Bukwimba, Mheshimiwa Daniel Mtuka na Mheshimiwa Josphine Gezabuke. Tutaendelea kutaja kadri tutakavyoendelea na uchangiaji lakini nimewataja ambao tutaanza nao mchana japokuwa sio kwa mtiririko nilioutaja.

Baada na kusema hayo nasitisha shughuli mpaka saa 11.00 jioni leo.

(Saa 7.00 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilitrudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tukae, Katibu.

NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

**Mpango wa Maendeleo wa Taifa Unaokusudiwa
Kutekelezwa na Serikali pamoja na Muongozo wa
Kuandaa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa
Mwaka wa Fedha 2019/2020**

(Majadiliano Yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Katibu.

NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MIPANGO

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na uchangiaji, naona wale waliotajwa Majina kabla hatujaahirisha mchana tunao wachache, tutaanza na hao, tutaendelea kutaja wengine, tutaanza na Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, atafuatiwa na Mheshimiwa Qulwi Qambalo.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii kuchangia Mpango wa 2019/2020. Nianze kwa kuwapongeza kuwa huu mpango ni mpango mzuri sana ambao kila mmoja kwa kweli ana uangalia na inabidi ajivunie kwa sababu ni mpango mzuri. Jambo ambalo naomba kuongelea naomba nishauri kuwa miradi ambayo imeshaanzishwa hasa kwa muda mrefu naomba sana iangaliwe kwenye vizuri kwenye Mpango huu, kwa mfano huu mpango wa Mchuchuma na Liganga uweze kumalizika na kuangaliwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba kushauri kwenye maendeleo ambayo yapo maboma wananchi wengi wamejenga maboma ya shule, maboma ya zahanati, maboma ya vituo vya afya na vyenyewe naomba viangaliwe kwenye mpango huu viweze kuhusishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni umeme, umeme ndio nashukuru na ninapongeza Serikali, nampongeza Mheshimiwa Rais anafanya vizuri sana, lakini kuna vijiji pamoja na vitongoji ambavyo bado havijapata umeme kwa hiyo ningeliomba viweze kuangaliwa kwenye mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo naomba kuangaliwa kwenye Mpango huu, ni maji, maji ni muhimu sana, unakuta kweli Wizara ya Maji inafanya vizuri sana lakini kila mmoja ananikubalia kuwa licha ya kufanya

vizuri bado kuna matatizo ya maji kwenye sehemu mbalimbali, kwa hiyo naomba sana hili jambo liangaliwe hata kwenye Kata yangu ya Magadu bado tuna tatizo la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo naomba liangaliwe ni kwenye mikopo ya elimu ya juu. Naomba sana vigezo viangaliwe kusudi wanafunzi wengi waweze kupata mikopo, kwa sababu unakuta amefaulu lakini hakujaliwa kupata mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ninaloongelea ni kilimo, kilimo kinaajiri zaidi ya watu zaidi ya 65.5% na asilimia 100 ya chakula kinatoka kwenye kilimo, lakini tunafanya vizuri ndio kwenye kilimo, lakini bado hatujapata kipaumbele kabisa kwenye upande wa bajeti naomba sana, Mheshimiwa Waziri Dkt. Mpango uangalie kuwa kuna tulikubaliana kwenye Malabo kuwa ni 10% kwa hiyo tuangalie kuwa itakuwaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye upande wa utafiti hatuwezi kuendelea bila ya utafiti, kwa hiyo tutengethela za kutosha kwenye mpango huu tuone kuwa utafiti utakwendaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye upande wa pembejeo uzalishwaji wa mbegu nashauri na naomba mpango uwepo wa kuzalisha mbegu hapa nchini, yaani tuzalish sana hapa nchini kuliko kuchukua mbegu za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo naomba kuongelea kwenye kilimo, ni viwanda vya kuzalisha mbolea, ndio vimeanza lakini bado havijachukua kasi, kwa hiyo, kwenye mpango huu, licha ya kuwa na mbolea inayoingia kutoka nje, lakini naamini kuwa tukizalisha kwenye viwanda vyetu hapa Tanzania mbolea itakuwa chini na wakulima wengi wataweza kuinunua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni viwanda vya dawa za wadudu, yaani viwatilifu, nashauri kuwa tuwe na viwanda, mpaka sasa hivi tuna kiwanda kwa wastani

kimoja ambacho kiko Njombe (Mafinga) cha Pareto naomba sana.,

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana tuwe na viwanda vingi, naomba niongelee uvuvi, uvuvi bado hatujaendelea vizuri kwenye uvuvi wa bahari kuu, naomba sana tujikite kwenye mpango wetu huu kuangalia jinsi tukavyoendeleza uvuvi wa bahari kuu na yenyewe tukazie sana kwenye mpango huu ununuzi wa meli ili tuweze kuwa na meli zetu za uvuvi kwenye bahari kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, ni ujenzi wa bandari ya uvuvi, niko kwenye uvuvi, tuweze kuwa na bandari ya uvuvi, kusudi tuweze kuvua samaki ambao wanatoka kwenye bahari kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, cherezo, tukiwa na meli tuweze kuwa cherezo yetu, ambayo imejengwa hapa nchini kusudi meli zetu ambazo tutanunua kwenye mpango huu, ziweze kutengenezwa na kukarabatiwa kwenye nchi yetu badala ya kwenda Mombasa na nchi nydingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine tuwe na viwanda, mpaka sasa hatuna viwanda vy a kuchakata samaki, hasa wa bahari kuu, kwa hiyo naomba tuweze kuwa na mpango uweze kuhusisha viwanda vy a kuchakata samaki bahari Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa mifugo, mifugo tuweze kuwa na mpango ambao utahusisha kuwa na ufugaji wa kisasa, sio ufugaji wa kuhamahama na hasa tuki-focus sana kwenye malisho, uwepo mpango wa kwenye malisho pamoja na mpango wa kwenye viwanda, pamoja na mpango wa kwenye mambo ya miundombinu, nikisema miundombinu namaanisha ujenzi wa mabwawa pamoja na majosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine naongelea kwenye upande wa mazingira, mazingira yetu mpaka sasa

hivi, hayafurahishi kwa hiyo naomba sana, mpango wetu huu, uweze kuhusisha mambo ya mazingira. Kwenye mpango huu wa 2019/2020 mipango iliyopita imeonesha changamoto, naomba kwenye mpango huu ambao tunakwenda nao wa 2019/2020 tuweze kuona jinsi ya kutatua hii changamoto.

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Asante sana Mheshimiwa muda wako umekwisha.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Qulwi Qambalo, atafuatiwa na Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ajiandae.

MHE. QAMBALO W. QULWI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kusema yangu machache kwenye mpango huu wa Mheshimiwa Dkt. Mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikiliza hotuba ya Waziri anayehusika lakini pia hotuba ya Kamati ya Bajeti, lakini pia hotuba ya Kambi ya Upinzani. Hotuba zote hizi zimekiri mapungufu ya kibajeti, ndio maana katika mipango yote iliyopita hatukufikia malengo. Sasa sielewi awamu hii katika mpango huu wa nne ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Mpango anakuja na miujiza gani ili aweze kutekeleza yale yote ambayo ameyaweka kwenye mpango huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia takwimu katika mipango iliyopita hasa kile kipengele cha bajeti ya maendeleo, utekelezaji umekwenda kwa asilimia kati ya 50 na 60, mimi ninatafsiri matokeo haya kama sio yenye afya sana kwa sababu kama ni kule shulenii hiyo bado ni B wala sio B+; kwa hiyo tuko chini ya wastani. Kwa hiyo nilikuwa nataka niliseme kwamba hapa kinachotakiwa ni pesa ili

mipango hii iweze kufanikiwa kinachohitajika ni pesa, lakini pia kingine kinachohitajika ni dhamira ya dhati ya kutekeleza yale yote ambayo tumekusudia kuyafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri maeneo machache, Mheshimiwa Waziri naomba nikushauri umwezeshe Msajili wa Hazina afanye kazi yake vizuri, Msajili wa Hazina ana makampuni au mashirika yasiyopungua 250 ambayo yanapaswa kuchangia kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina, lakini mengi ya mashirika haya, yamekuwa yakitenda kwa kusuasua, mengine hayajui kabisa kutoa gawio kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali, mashirika mengine hata kama yanatoa gawio, yanatoa gawio kwa kile kiasi ambacho wao wanajisikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia yako mashirika ambayo kwa kweli yanahitaji kuondolewa kwa sababu yanachukua ruzuku Serikalini lakini mwisho wa siku hayazalishi kitu chochote, kwa hiyo nilikuwa nafikiri msaidie Msajili wa Hazina na huyu bwana ukimsaidia naye atakusaidia sana kupata pesa. Msaidie kupata watumishi, lakini pia mpatie vitendea kazi ili aweze kufanya kazi yake vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, ni ukusanyaji wa kodi. Mheshimiwa Waziri, wewe ndio mkusanyaji mkuu wa kodi nchi hii, na nchi hasa awamu hii ya tano, imedhamiria kujidesha kwa kukusanya kodi na kutumia kodi kwenye maendeleo, kwa hiyo unapokutana na wakwepaji wa kodi hawa watu naomba usiangalie sura yao, usiangalie dini yao, usiangalie na kabile yao, na usiangalie na vyeo vyao. Miezi michache iliyopita kulikuwa na lile sakata la makontena ya Makonda, ambayo yalikuwa na sura ya ukwepaji wa kodi, ulijaribu, ulijaribu kutoka hadharani na Watanzania tukakusifu na Watanzania tukasema tunaungana na wewe, sijui mwisho wa siku lile jambo limeishaje, umeshinda au ulishindwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uje utuambie baadae, jambo lile liliisha namna gani, lakini kama tumekubaliana kuendesha nchi kwa kodi basi wale wote

wanaostahiki kulipa kodi halali walipe na kusiwe na mianya ya watu kukwepa kodi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye eneo la kilimo, wengi wameongelea eneo hili na mimi naomba nipite pia huko huko. Nchi hii karibu asilimia 60/70 ya watu wake ni wakulima, na kwa hiyo kama tunahitaji mipango yetu ifanikiwe ni lazima tujielekeze kwenye namna ya kusaidia kundi hili kubwa liweze nayo kufanya kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo, chetu bado ni duni, wakulima wetu wengi wanatumia jembe la mkono wachache wanatumia majembe ya kukokotwa na mifugo, wachache sana wanatumia matrekta, tunahitaji kufanya mapinduzi makubwa kwenye kilimo chetu, ili kilimo kiwe na tija.

Sasa ninajua uko mradi wa Matrekta na mengi yameanikwa pale Kibaha, takwimu zinasema nchi hii, nchi hii ya Tanzania inazo kilometa za mraba karibu laki nne zinazofaa kwa kilimo na kwa kilometa hizo unahitaji walau kiasi cha matrekta milioni mbili ili ulime vizuri, lakini Tanzania ya leo, ina matrekta yasiyozidi 30,000 yakiwemo yale ya pale Kibaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sasa wewe utaona jinsi ambavyo kwa kweli, tunahitaji mapinduzi makubwa ili kilimo kiwe na tija, lakini pia suala mbegu, wakulima wetu wengi wanapanda zile mbegu ambazo sio zile zilizoboreshwa na matokeo yake wanavuna kiasi kidogo. Miaka ya nyuma tulikuwa na Kampuni inaitwa Tanseed iliyokuwa inazalisha mbegu ya mahindi, kampuni hii imetoweka, mbegu nyingi tunazopanda sasa hivi kwenye zao la mahindi ama zimezalishwa Kenya au Msumbiji au Malawi au Zambia zinazalishwa katika mazingira tofauti kabisa na haya ya kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini zinapokuja nyumbani zinauzwa kwa bei ghali mno, ni wakulima wachache wanaweza kupanda hizi mbegu ambazo zimaboreshwa.

Turudishe mashirika yetu ya Kitanzania yaweze kuzalisha mbegu hapa nyumbani ili wakulima wetu wapate mbegu kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye mbolea, maeneo mengi ya nchi hii kama hujaweka mbolea huvuni kitu, lakini tunayo Kampuni ya Mbolea Tanzania (*TFC*) ambayo mimi naweza kusema ni kama kampuni inayoelea kuzimuni, kampuni hii inashindwa hata kujiendesha, zamani kampuni hii ilikuwa inazalisha mbolea pale Tanga, kiwanda kimekufa, sasa hivi wanaagiza, wanasambaza na wanauza mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kampuni hii, inaonekana haina uwezo kabisa wa kufanya kazi hii, kimsingi kampuni hii ya *TFC* inakosa mtaji wa uendeshaji yaani *working capital*. Mheshimiwa Dkt. Mpango, shirikiana na Waziri mwenzako wa Kilimo na Waziri mwenzako wa Viwanda, illi kuisadia Kampuni ya *TFC* iweze kufanya kazi yake vizuri, vinginevyo nchi hii suala la mbolea tutalisahau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye eneo la Mchuchuma, Mchuchuma na Liganga imekuwa ni wimbo ambao hauna mwisho, hapa ndio nataka kusema kama kweli kama nchi tuna dhamira ya dhati hebu mradi huu ukamilike, miaka 25 ndani ya Bunge hili watu wanaongea habari ya Mchuchuma na Liganga, lakini miradi hii haikamiliki, kuna tatizo gani? Mimi nadhani kama tuna dhamira ya dhati jambo hili linawezekana, tuifanye Mchuchuma kama tulivyofanya kwenye reli, kama tulivyofanya kwenye ATC na kama tulivyofanya kwenye hiyo *Striglers Gorge*...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa muda wako umekwisha.

Waheshimiwa tunaendelea nilimtaja, Mheshimiwa Ritta Kabati, atafuatiwa na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, Mheshimiwa Vuma Augustino ajiandae.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia Mpango wa Taifa wa Serikali. Nianze kwanza kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu, nimpongeze pia Waziri Mkuu wetu, nipongeze Mawaziri wote wa Serikali ya Awamu hii ya Tano kwa kazi nzuri sana ambayo wamekuwa wakiifanya kwa kipindi cha miaka mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendele pia kumpongeza sana, kupongeza sana Wabunge wote ambao wamehamia CCM kutoka upinzani kwa kuona kazi nzuri sana inayofanywa na Mheshimiwa Rais, kwa kuona kazi nzuri sana inayofanywa na Mawaziri wetu na kuamua kuja CCM, kwa hiyo nikwambie Mheshimiwa Jenista jiandae kazi yako ni nzuri tutaendelea kuja huku kwetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Mpango, kama jina lake liliyvo kwa mpango mzuri, Naibu wake, Dkt. Kijaji, watendaji wote wa Wizara ya Fedha kwa kazi nzuri ambayo wametuletea huu mpango mzuri wa maendeleo ambao kwa kweli umepanga ukapangika, na ndio maana sasa hivi unatekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendele, mimi leo nikupongeza kwa sababu mambo mazuri yanaonekana, niendele kumpongeza Rais wetu na Serikali yetu na Chama chetu cha Mapinduzi kwa miradi ambayo sasa hivi yameanza kutekelezeka ya kielelezo ujenzi wa reli ya kat, ujenzi wa barabara wa barabara ya juu (*Mfugale fyoer*) ujenzi wa viwanja vyta ndege, uboreshaji wa shirika la ndege, mradi wa kuzalisha umeme maji - Rufiji, mradi wa ujenzi wa bomba la mafuta ghafi kutoka Uganda mpaka Tanga na miradi mingine mingi tu nikiitaja hapa muda utaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda katika ukurasa wa 32 wa kitabu cha hotuba ya Waziri Mpango, niendele kumpongeza marekebisho ya Sheria ya Madini, kwa kweli niendele kuwapongeza Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri kwa kufanya marekebisho ya Sheria za Madini zilizofanyiwa

mapitio ili kuwezesha Serikali yetu kunufaika zaidi na rasilimali za madini ambayo imewezesha ongezeko la mapato kwa kipindi cha mwaka 2017/2018 lengo ambalo ilikuwa limewekwa na Serikali kwa mrabaha na ada za mwaka za leseni ilikuwa shilingi bilioni 194; lakini imeweza kukusanya bilioni 301.2 ambayo sawasawa na asilimia 56, kwa kweli hilo ni jambo kubwa sana. Tutakumbuka kwamba jinsi sheria hii ilivyokuwa imeleta matatizo makubwa wenzetu walikuwa hawailewi lakini sasa hivi Serikali imeweza kupata mapato makubwa sana kuitia marekebisho ya sheria hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuitia sheria hii imeweza kuweka katazo la kusafirisha madini ghafi ambayo hayajawekewa thamani. Ushauri wangu kwa Serikali, Serikali iweke mazingira wezesi kwa kuondoa kodi katika mashine za ukataji wa madini ya vito. Hii itasaidia kuwa na wakataji wengi wa madini ya vito na pia itasaldia ajira kwa viljana wetu kuitia madini. Pia kuweka mazingira wezesi ya kusaidia shughuli za wachimbaji wadogo wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niombe Serikali iweze kuwasaidia kuwawekea mazingira wakina mama ili waweze kujiajiri kuitia madini kama vile kuna Chama cha TAWOMA ambacho ni chama cha wachimbaji wanawake kote nchini pia kiwezeshwe ili sisi wakina mama pia tuweze kujiajiri kuitia madini. Pia nishauri kwamba wawepo Maafisa Madini wa Mkoa kuliko walivyo wa kanda ilivyo sasa hivi ili kusaidia hii sekta ya madini waweze kukusanya pesa katika mikoa yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ukienda katika ukurasa wa 33 unaelezea kuhusu elimu. Niipongeze Serikali yetu kwa utaratibu wa kutoa elimu bila malipo katika shule zetu ambapo wameweza kutumia shilingi bilioni 20.9 kila mwezi. Ukifungamanisha uchumi na maendeleo ya watu, mpango wa kuendeleza ufaulu katika masomo ya hesabu na sayansi na kuendelea kutoa elimu inayozingatia mahitaji halisi ya soko la ajira. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunaelekeea kwenye uchumi wa viwanda, sasa naiomba Serikali iwe na mikakati

ya kuhakikisha kwamba shule zetu nchini zinaboreshewe maabara kwa sababu maabara katika shule nyigi bado hazijakamilika, lakini pia walimu bado hawatoshelezi kuwepo katika shule kufundisha hii elimu ya sayansi, lakini pia na vifaa vya maabara Serikali ijitahidi kwa sababu sasa hivi tunatakiwa tuandae wanasayansi wengi sana ili kusaidia huu uchumi wa viwanda, vijana wetu waweze kuajiriwa na tuweze sisi wenyewe kuwa na vijana amba wanatumikia viwanda vyao. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba tu nitoe mfano wa nchi ya Singapore; unaona nchi ya Singapore ilikuwa ni nchi ambayo ina uchumi duni sana, lakini kuna yule Waziri Mkuu ambaye ni kiongozi wao anaitwa Lee Kuan Yew ye ye kwakweli kwanza kabisa alivyoanza kuinua uchumi wa Singapore walimuona kama dikteta lakini sasa hivi alipofariki wamemkumbuka kwa sababu uchumi wa Singapore sasa hivi umekuwa upo juu sana na unaona ye ye aliamua kutoa elimu kwa vijana wake wa Singapore na sasa hivi vijana wameweza kujijiri, kuajiriwa na kutengeneza uchumi kwa kutumia viwanda walivyonyavyo...

(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja, asante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Sophia Mwakagenda atafuatiwa na Mheshimiwa Augustine Vuma, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba ajiandae.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi naomba niunge mkono Kambi Rasmi ya Upinzani maana na sisi tumetoa dira, mwelekeo na mpango ambao tunafikiri Serikali mnaweza mkaufuata. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwanza nataka nizungumzie kilimo. Tunapozungumzia kilimo ambayo tukimechukua asilimia takribani 75 ya Watanzania wamejikita katika kilimo, lakini katika mpango huu ambao Mheshimiwa Mpango umeuleta hatuoni nguvu ya Serikali kusaidia wakulima wa Tanzania waweze kukuza uchumi wao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ambazo tumekuwa tukipanga Wizara inatoa asilimia mbili tu ya mapato kusaidia wakulima. Tunafahamu kwamba katika kilimo usipoweka pesa wewe kama Serikali na ukitegemea wafadhili wakupatie pesa kwa ajili ya kilimo na bahati mbaya sana wafadhili wenyewe mmeanza kuwakorofisha. *EU*ilahidi kutoa hela zaidi ya bilioni 200 kwa ajili ya kusaidia kilimo tayari tumeanza kukorofishana nao sijui tutafika wapi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo kwa Nyanda za Juu Kusini niachilie mikoa mingine hakuna dalili zozote za kusaidia hasa katika tafiti ili uwe na kilimo bora kwanza kabisa lazima ufanye tafiti. Mwalimu Nyerere alijitahidi kuweka vyuo mbalimbali vya kilimo ikiwemo Chuo cha Uyole mpaka sasa zaidi ya miaka mitano hawajawahi kupata pesa za maendeleo kwa ajili ya chuo kile. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna viwanda vingi vilianzishwa ili viweze kusaidia wakulima kwa mfano ZZK walikuwa wakitengeneza zana za kilimo ikawa rahisi kuwafikia wananchi kwa ngazi ya chini, leo hii kila kitu tunatoa nje, tunatoa China kwa gharama za kigeni kuweza kuwafikia wakulima mwisho wa siku pembejeo zinakuwa ni bei kubwa sana kuwafikia wakulima. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbegu ambazo ndio zinatakiwa zizalishe chakula cha Watanzania asilimia 90 ya mbegu tunaagiza kutoka nje. Bahati mbaya sana mbegu nyininge zimekuwa sio rafiki kwa ardhi ya kitanzania ndio maana ninarudi nyuma kwamba tunahitaji kuwa na watu wanaofanya *research* ambao watajua mbegu hii inafaa kwa ardhi hii au zao hili linafaa mkoa fulani na watu hawa waweze

kusaidia wakulima waweze kupata mazao yanayostahiki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia *connectionya* Wizara tofauti ili kuweza kusaidia Wizara mama kuwa na mafanikio sisi kama watanzania tumeshindwa. Leo hii watu wanaohusika na mambo ya hali ya hewa hawawezi kufanya kazi kwa karibu sana na Wizara ya Kilimo kuweza kujua mwaka huu tunalima mazao kadhaa kwa kupata taarifa kutoka kwa wataalam, kila mtu anafanya kazi anavyoona ye ye inafaa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maji na Wizara ya Kilimo; maji na kilimo vinaenda sambamba, lakini wasipofanya kazi kwa pamoja Wizara ya Maji haina pesa, Wizara ya Kilimo haina watafiti, tunawezaje kufanikiwa katika kilimo na tunawezaje kuwa na maendeleo ya kiuchumi kama Watanzania na kuwafanya wakulima wanapata mazao kwa wakati sawasawa na ubora tunaoutaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na mashirika mbalimbali yakisaidia upatikanaji wa mbegu. Kama mnakumbuka Ukiliguru zamani walikuwa wanashughulika na mambo ya mbegu, sasa hivi watu kama wale wako wapi? CCM mlikuwa na kitu kinaitwa *SUKITA* kiko wapi? Vitu mbalimbali vilikuwepo zamani kwa ajili ya kusaidia wakulima hawapo, havipo na wala hakuna ubunifu wa kuanzisha vitu vingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie habari ya utawala bora na ukuaji wa uchumi. Usipokuwa na utawala bora na umoja na wananchi kutoka ngazi ya chini mpaka Taifa mnakosa nguvu na moyo wa watanzania kufanya kazi ili kuweza kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wengi wamezungumza mahali hapa kuhusu Katiba Mpya na hii ipo katika mpango ambao sisi tumekuwa tukiuzungumzia. Huwezi kuwa na maendeleo yoyote kama hamjajiwakeea utaratibu wa utawala. Watu walitoa pesa (kodi) tukaweka Tume,

wakazunguka nchi nzima, wakaweka utaratibu wa kuweza kuona kama Watanzania tunaishije, leo hii tumeacha na kuishia pemberi, kwa maana pesa zote zilizotengwa zimekwishakupotea ambayo ilikuwa ni kodi ya wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba utakaporudi utueleze umepanga nini na kwa nini Serikali yako inakataa kuzungumzia Katiba Mpya ili twende kwenye mustakabali wa maendeleo yetu hapo baadae. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulinzi na usalama ni kitu cha muhimu sana katika Taifa letu la Tanzania. Usipokuwa na ulinzi na usalama wawekezaji wanaondoka. Tumekuwa tukisikia mambo mengi yakitokea na sisi kama wananchi na hata kama Wabunge hatujapata taarifa ya kueleza kwa nini wawekezaji wanatekwa na wanafukuzwa na kama wamekosea je, mmeefanya njia gani mbadala mpya ya kuweza kuwatangazia utaratibu mpya wa kuwekeza ili watu wasiwe na mashaka na ulinzi wa Tanzania na usalama wao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pasipo na usalama hakuna mtu atakuwa tayari kuja kujunga na Watanzania. Tupo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, watu wanaona ni bora wahamishe bidhaa zao kwenda Kenya, Uganda na sehemu zingine kuliko kuja sehemu ambayo haina uhakika wa ulinzi wa maisha, mali na mitaji yao watakayowekeza. Tunaomba unapokuja kutueleza Mheshimiwa Mpango ueleze Watanzania pamoja na sisi Wabunge ni mkakati gani umejiwekea wa usalama wa wawekezaji; utatumia njia gani ya kuwalinda hata hao wachache waliobaki waendelee kutumika katika Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda sana kutoa ushauri, vitu vingi sana vinavyofanyika sasa ambavyo vinaharibu kabisa umoja wetu na hasa katika maandalizi ya kutetea uchumi wa Taifa letu. Mimi ninaomba usimamie *TRA* ambao ni wakusanyaji wa kodi kwa kweli wamekuwa kama ni askari, hawana umoja na wafanyabiashara na sasa hivi

imefika mahali hata wenye mitaji ya 300,000 wanahitaji kulisipu kodi, ni kweli sikatai kwamba wasilipe kodi lakini lazima zitungwe sheria ambazo zinasaidiana kuweza kuwasaidia hawa watu wajione wana wajibu wa kufanya hiyo kazi ya kukusanya kodi pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na hali ya udhalilishaji mkubwa sana kwa wafanyakishara na kumekuwa na matamko mengi hasa Wakuu wa Wilaya kufungia makoso kwa sababu za kisiasa. Wakati mwingine tuliona pale Tunduma, muda mrefu sana masoko yamefungwa, zile pesa ambazo siku ile hazikuingia Serikali ilikosa mapato sababu ya siasa. Vivyo hivyo Mbeya soko la *SIDO* lilitungwa kwa muda mrefu kwa sababu za kisiasa... (Makof)

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Muda umekwisha Mheshimiwa, kengele ya pili imegonga, asante sana. Mheshimiwa Vuma Augustine Holle atafuatia Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mheshimiwa Daniel Mtuka ajiandae.

MHE. AUGUSTINE V. HOLLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru lakini pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na kuniwezesha kufika jioni leo ambapo nachangia mpango huu wa maendeleo. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote niungane na wenzangu kuipongeza Serikali hasa Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi kubwa sana anayoifanya na wasaidizi wake. Kazi ya kuendesha Taifa na kuliletea maendeleo ni kazi kubwa sana na tumemsikia mara kadhaa Mheshimiwa Rais akisema wakati mwingine halali hata usingizi, anakesha akishughulika na shida za Watanzania. Sisi kama Watanzania na Wabunge tunamuombea kwamba Mwenyezi Mungu amtie nguvu na aendelee kuwatumikia Watanzania bila kuchoka na Mungu atamlipa. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze moja kwa moja kwa kuunga mkono huu mpango kwa sababu ya mambo mazuri yaliyomo humu ndani. Nimeupitia, ukiangalia miradi mikubwa ambayo Serikali inatekeleza ni miradi ambayo sisi kama Watanzania tunajivunia. Ukiangalia yapo mambo mengi sana, iko *SGR, Stiegler's Gorge* lakini pia kufufua Shirika la Ndege (*Air Tanzania*), haya yote na mengine mengi tumeanza kuona matunda yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano ukija kwenye haya licha kutoa ajira kwa mfano kufufua Shirika la Ndege, ilifika kipindi hapo katikati kabla ya juhudzi za Mheshimiwa Rais kufufua Shirika la Ndege ilikuwa kwa sisi ambaao mikoa yetu ipo mbali na Jiji la Dar es Salaam ilikuwa kupata tiketi ya ndege kwanza ni kazi kubwa na wakati mwingine inakuwa ni bei ambayo ni sawasawa na kutoka Tanzania kwenda Dudai. Maana mimi niliwahi kupanda ndege kutoka Dar es Salaam kwenda Kigoma kwa shilingi 900,000 *one way*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kufufua shirika hili la ndege sasa hivi bei imeshuka chini, unauhakika wa kwenda na kurudi Kigoma kwa hela chini ya shilingi 500,000. Kwa hiyo, haya ni mapinduzi na maendeleo makubwa ambayo tunapaswa kuyapongeza sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo mazuri sana yaliyopo kwenye mpango huu, napenda kushauri mambo yafuatayo ambayo naamini Serikali ikiyazingatia yatatupeleka mbele zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze na Benki ya Uwekezaji yaani *Tanzania Investment Bank (TIB)*. Benki hii tumeianzisha mwaka 1970 chini ya Sheria ya *Investment Bank Act of 1970*. Benki hii kimsingi ilisusua hapo katikati, ilipofika 2005 nadhani Serikali ilianza kui-restructure upya na hatimaye tukaweka malengo kwamba ingeweza kupewa mtaji wa shilingi bilioni 500 lakini mpaka sasa hivi benki hii imepokea shilingi bilioni 195 peke yake. Wanasesma kwa tathmini iliyofanyika kama benki hii ikiweza kupata trilioni moja kama mtaji, benki hii inaweza kukuza uchumi wa taifa kwa *double*

digit, lakini pia inaweza kupunguza umaskini wa Watanzania kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi nyingi duniani kote ukienda China, Uingereza, India, Malaysia na nchi nyingi sana wamekuwa na benki hizi za kimaendeleo, benki ambazo ndizo zinazofadhili miradi mikubwa ya kimaendeleo katika nchi husika na kama Serikali ikijikita huko na malengo yale ya kuwapelekea angalau hata bilioni 500 mimi naamini wanawenza kufanya kazi kubwa sana kwa ajili ya maslahi mapana ya watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wenzangu kwenye kilimo. Benki ya Kilimo ni benki ambayo kwanza Serikali imepeleka watu wazuri na wenyewe akili, mimi nipo kwenye Kamati ya *P/C* tunakutana nao sana hawa. Ukiangalia menejimenti yake ni watu ambaao wana *mind* ambazo zipo *sharp*, wana ubunifu na mipango mingi lakini ukiangalia mahitaji makubwa, uti wa mgongo wa nchi hii ni kilimo, kwa hiyo, lazima tulitizame kama benki ya kimkakati na tuitengee fedha za kutosha ili waweze kutimiza malengo yao na hatimaye waweze kuwafikia Watanzania wengi maana ipo mikoa ambayo ukienda ukauliza Benki ya Kilimo ni nini hata hawajui kwa sababu haipo. Kwa hiyo, tujitahidi kuipa mtaji iweze kwenda kwenye mikoa yote ikawafikia wakulima wadogo na wakubwa na kuwakopesha kwa ajili ya kunusuru kilimo cha nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nipende kushauri kitu kimoja, taifa letu tumejitabanaisha kama Taifa la viwanda, ndio sera ya nchi yetu. Sasa ningependa kushauri kwamba tuwe na malengo ya kuanzisha Benki ya Maendeleo ya Viwanda ambayo hapa shida ya kuwa mtaji unatoka wapi kwa sababu tunaenda ku-*discourage importation* ili tuweze ku-*Increase* uzalishaji wa ndani nadhani tungeweza kuangalia namna ambavyo tungeweza kuweka tozo kwenye bidhaa ambazo zinaingia kwetu Tanzania ambazo hazitaathiri sheria ambazo tumeingia na mataifa mengine ili tuweze kupata mtaji wa kutosha na hatimaye tuanzishe Benki ya Maendeleo ya Viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa sababu unajua kiwanda unavyokianzisha ni *long time investment, return* yake inakuja baada ya muda mrefu, sasa ukisema kwamba benki kama *NMB* au benki zingine ndio waweze kufadhili haya waanzilishi wa viwanda unakuta wanapata shida kwa sababu wanawekewa masharti magumu kwa sababu wanahitaji mitaji mikubwa lakini ambayo wanahitaji muda mrefu kuirejesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia maendeleo ya taifa lazima tuangalie na ustawi wa watu wa chini (wadogo wadogo) hasa kwenye sheria zetu. Lipo suala ambalo sheria zetu hizi wakati mwingine zinakuwa zina shida na hatimaye inaleteleza wananchi kupata shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijikite hasa kwenye Jimbo langu; lipo tatizo la Msitu wa Makerere Kusini yaani Kalandani. Tatizo hili najua linaenda kutatuka muda si mrefu kwa sababu Mheshimiwa Kigwangalla ameshasaini *document* ambayo inaenda kuwa sheria kamili kwamba lile eneo ambalo Mheshimiwa Rais alitupa tuanze kulitumia. Nakuomba Mheshimiwa Kigwangalla ufanye haraka ku-*gazette* hiyo *document* ili wananchi wasiendelee kupigwa Kalianganda na waweze kufaidi matunda ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. (*Makofj*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lolesia Bukwimba atafuatiwa na Mheshimiwa Daniel Mtuka na Mheshimiwa Ignas Malocha ajiandae.

MHE. LOLESTIA J. BUKWIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ili niweze kuchangia kwenye Mpango huu muhimu kabisa wa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kipekee kabisa kumpongeza Mheshimiwa Rais pamoja na Serikali kwa ujumla, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu kwa kazi kubwa ambayo wameifanya katika taifa letu kwa miaka mitatu. Ni kwa

namna ya kipekee kabisa kwa miaka mitatu lakini kazi iliyofanyika ni kazi kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli wametuonesha mfano kwa sababu kila baada ya shughuli za Bunge kwa Waziri Mkuu anatembelea kila sehemu. Lakini siyo yeye tu, hata Mawaziri wanapita huku na kule kusimamia na kuangalia utekelezaji, hakika usimamizi wa Serikali uko kwa hali ya juu sana na mimi nichukue nafasi hii kupongeza sana kwa juhudhi hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango kwa kazi kubwa, hasa kwa kutuletea mpango huu mpya wa mwaka 2019/2020. Kazi iliyofanyika kuandaa huu mpango kwa kweli ninapongeza sana kwa sababu wamegusa sehemu zote ambazo ni za muhimu kabisa kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu na kwa sababu hiyo tu mimi ntachukua fursa kuangalia vipengele vichache tu kuviongezea kuonesha vipaumbele vya muhimu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianzia na sekta ya nishati, ninaomba kwamba mwaka kesho wakati ambapo wanaandaa huu mpango kamili na bajeti, wahakikishe sekta ya nishati inawekewa bajeti ya kutosha hasa kwenye miradi ya *REA*. Nilivyokuwa nikiangalia kwenye utekelezaji ni vijiji zaidi ya 5,000 tu vimepata umeme, lakini jumla ya vijiji Tanzania nzima vinafika zaidi ya 12,000 kwa hiyo, naona kwamba kazi kubwa bado inahitajika fedha ya kutosha kuitia *REA* kuweza kuona kwamba vijiji vyetu vya Tanzania, hasa wananchi waishio vijijini wanapata umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu haiwezekani tukafikia azma yetu ya viwanda bila ya kuwa na umeme vijijini maana tunatambua kabisa uzalishaji uko katika vijiji vyetu kwa hiyo ninaomba kwamba mpango wetu, hasa kwenye bajeti ijayo ioneshe sekta ya nishati na umuhimu wake iwe na fedha za kutosha ili kuona kwamba vijiji vyetu vya Tanzania vinapatiwa umeme na wananchi waweze kunufaika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta muhimu kabisa ya madini ninapenda pia kuishauri Serikali, ninajua kwamba kwa kipindi kifupi tu cha mwaka 2017 tumebadilisha Sheria ya Madini, tumeibadilisha ile sheria iliyokuwepo ya mwaka 2010 na mabadiliko yake kwa kweli yamekuwa ni ya msaada mkubwa sana, hasa pia kwa kuunda Tume ya Madini. Niombe tu sasa katika bajeti ijayo katika mpango huu tuhakikishe hii *commission* ya madini iweze kuwezesha iweze kufanya zake vizuri ili hatimaye sasa tuweze kufikia azma ambayo tumekusudia kuweza kusimamia vizuri hii sekta muhimu ya madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukikumbuka wachimbaji wetu wadogo wa Tanzania. Tunajua vijana wengi wameajiriwa sana katika sekta hii, hasa vijana ambao ndio nguvukazi ya Taifa. Niombe kwamba katika bajeti zijazo, vijana wetu, hasa katika sekta ya madini wachimbaji wadogo waweze kutengewa fedha za kutosha ili wawe na mitaji kwa ajili ya kuweza kufanya shughuli zao vizuri ili hatimaye waweze kuendelea kuchangia zaidi katika pato la Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, katika sekta ya elimu Serikali imesema katika mpango kwamba imekusudia kujenga vyuo kumi. Niombe kipaumbele pia katika mikoa mipyä ambapo hatuna kabisa vyuo hivi vya ufundi. Kwa hiyo, ninaunga kabisa mkono kwamba katika sekta ya elimu vyuo vya ufundi ni vyuo vya muhimu sana ambavyo vitawawezesha vijana wetu kuwa na ufundi, yaani waweze kuwa na fani ambayo wataweza kufanya majukumu yao vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya maji mmekusudia kuanzisha Wakala wa Maji Vijijiini, jambo ambalo ni la msingi kabisa. Wote tunafahamu maji ni uhai na kwa sababu hiyo kila mahali tunahitaji kuwa na maji ya uhakika, kwa hiyo niombe tu kwamba katika utengaji wa fedha, katika kupitia mpango huo tuone umuhimu wa sekta ya maji ili kwamba basi tuweze kufikia azma ya Serikali kwamba mpaka kufikia mwaka 2020 angalau asilimia 85 ya wananchi waishio

vijijini na asilimia 95 mijini wawe wanapata maji safi na salama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaunga kabisa mkono juhudzi za Serikali, hasa Wizara ya Fedha na Mipango kwa kutuletea mpango huu muhimu ambao umegusa karibu kila eneo, kila sekta, ukiangalia sekta ya barabara vijijini, tunaomba sana pia bajeti ziongezwe kwa sababu barabara pia ndiyo kichocheo kikubwa cha maendeleo katika maeneo ya vijijini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya afya, ninaomba Serikali iongeze ajira kwa ajili ya wataalam. Tumeona kabisa kwamba vijiji au katika zahanati nyingi na vituo vya afya na hospitali tuna upungufu mkubwa sana wa wataalam katika sekta ya afya. Kwa hiyo, Serikali iongeze basi katika eneo hilo bajeti iwe kubwa zaidi kwa ajili ya ajira kwa ajili ya wataalam katika sekta ya afya kwa sababu tayari miundombinu imekwishaanza kutengenezwa hospitali za wilaya, vituo vya afya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninaunga mkono hoja nikiamini kwamba yale niliyoongea yataweza kuzingatiwa. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Daniel Mtuka atafuatiwa na Mheshimiwa Ignas Malocha na Mheshimiwa Peter Lijualikali kwa dakika tano ajiandae.

MHE. DANIEL E. MTUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nashukuru kwa nafasi hii. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai kukutana tena leo katika Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Rais wangu kwa kazi anayoichapa pamoja na timu nzima ya Mawaziri pamoja na watumishi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze moja kwa moja kuchangia; ukienda ukurasa wa 47 wa mpango, lakini na ukurasa wa 27 wa hotuba nataka kuzungumzia jambo la

hifadhi ya mazingira pamoja na kukabiliana na mabadiliko ya hali ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi hii tumebarikiwa sana kuwa na misitu minene ambayo ni vyanzo vya mvua, vyanzo vya hali ya hewa nzuri pamoja na maji, Mungu alitupendelea sana, naiita Tanzania kama bustani ya Edeni. Lakini dalili zinavyokwenda hii bustani ya Edeni sasa tunaeleka kuanza kuiharibu kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukichukua Tabora eneo la Sikonge, Chunya Mbeya, Mbarali, eneo la Singida, hapo katikati kuna msitu mmoja mnene wa Miyombo ambacho ni chanzo kikubwa sana, kuna mito karibu 18 iko pale inayotengeneza mto unaoitwa Mto Ruaha Mkuu ambaou unaenda moja kwa moja unakatiza kwenye Mbuga ya Selous, lakini unakwenda kuungana na Mto Rufiji. Lakini pale katikati pia kumegawanyika, kuna Mto Kilombero ambaou unakwenda mpaka kutengeneza mabwawa kama ya Mtera kwa ajili ya kufua umeme. Lakini kuna maeneo mengine iko mito mingi Mto Ugala, Mto Ruvuma, Mto Ruvu, mto bubu huu hapa ambaou tunategemea kuanza Bwawa la Farkwa kwa ajili ya kulisha watu wa Dodoma. Mito hii ina vyanzo vyake ambayo ni misitu pamoja na mito midogo midogo, lakini tumekuwa na tabia mbaya kidogo sisi binadamu wa Tanzania kuharibu mazingira ya mito. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kidogo jambo hili; tunahitaji vyanzo vya maji, ni lazima tulinde misitu yetu hii, tunahitaji hali ya hewa (oksijeni), ni lazima tulinde misitu hii pamoja na mvua. Kuna mtaalam mmoja anaitwa Dkt. Anne Marie, anasema binadamu kwa mwaka mmoja anavuta hewa ya bure kilogramu zipatazo 740 na mti mmoja una uwezo wa kutoa kwa mwaka kilogramu 200 hadi kilogramu 300.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mtu mmoja anategemea miti mitatu, kupata hewa ya bure ukiacha vyanzo vingine vya oksijeni, ujue thamani ya mti iliyo kuwa ni kubwa. Unapokata mti jishauri mara mbili/mara tatu

kuuangusha mti ule maana yake unaweka shoka kwenye shingo yako, kukosa oksijeni na kusababisha hasara katika maisha. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niombe jambo moja, tunazo sheria za misitu, tunazo sheria za hifadhi za wanyama, lakini pia tutumie kutoa elimu sana, wakuu wa mikoa kule watusaidie, Wizara inayohusika itusaidie, hebu tuelimisheni Watanzania tuachane na tabia ya kukata miti tulinde mazingira. Ningekuwa ni Mheshimiwa Rais mimi, Wakuu wa Mikoa kwa kweli moja ya vigezo kabisa vyta kuendelea na cheo cha Mkuu wa Mkoa ni kuhifadhi mazingira, kuhakikisha miti haikatwi hovyo, hasa kwenye hifadhi zetu za misitu. Tunazo hifadhi nyingi, karibu asilimia 32 ya nchi hii ni hifadhi hizi, zihifadhiwe kwa ajili ya kulinda mazingira ili tuweze kuendelea na *survival*, tunazungumzia *Stiegler's Gorge* tunajenga kule, tukiharibu mazingira maana yake ni kwamba umeme hautazalishwa, Kidatu kule umeme hautazalishwa, tutunze mazingira Watanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye utunzaji wa mazingira huo huo nzungumzie mifuko mifuko ya plastiki, miaka miwili mitatu iliyopita tuliweka utaratibu mzuri, kwamba tunaweka miezi sita, mifuko ya plastiki sasa Tanzania iwe basi. Rwanda wenzetu wakachukua mpango ule, wameutekeleza, wako vizuri, ukienda huwezi kuona plastiki Rwanda, lakini sisi tuna plastiki hapa. (*Makof*)

Naomba Wizara inayohusika mpango wa kuomdoa mifuko ya plastiki tusitumie hiyo. Tanzania ni chafu kila mahali, ng'ombe wanakufa, wanyama wanakufa, wakila ile mifuko haiyeyuki, plastiki hatuitaki. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie suala moja katika ukurasa wa 38 wa kitabu cha hotuba, umezungumzia vipaumbele ni pamoja na viwanda ambavyo tunatarajia. Umeitaja Dodoma na Manyoni kama baadhi ya maeneo ambayo tutatenga maeneo kwa ajili ya viwanda. Naitaja Manyoni kwa sababu imetajwa kwenye mpango, siitaji

Manyoni kwamba nitaje vitongoji vya Manyoni, hapana, imetajwa kwenye mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana mtusadie Manyoni, naomba sana muisaidie Dodoma. Tengeni fedha kwa makusudi, sasa Dodoma ni makao makuu kutakuwa na vyano vya ajira, tukitenga maeneo ya viwanda tunayo maeneo ya kutosha. Kwa mfano pale Manyoni nimesema tuna ekari zaidi ya 5,000, zipo tumezitenga kwa ajili ya viwanda...

(Hapa kegele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mtuka kwa mchango wako.

MHE. DANIEL E. MTUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya mpango wa Mheshimiwa Dkt. Mpango, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Ignas Malocha atafuatiwa na Mheshimiwa Peter Lijualikali kwa dakika tano na Mheshimiwa Josephine Genzabuke ajiandae.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuungana na wenzangu katika kuujadili Mpango wa Maendeleo na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango wa Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Rais, nimpongeze Waziri na msaidizi wake, Naibu Waziri na watendaji wote wa Serikali katika Wizara hii. Lakini mchango wangu utaelekea kwenye kilimo na hasa ukurasa wa 35 unaozungumzia changamoto mbalimbali ambazo Mheshimiwa Waziri amezia inisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakwenda moja kwa moja katika changamoto namba sita inayosema kukosekana kwa masoko ya mazao na bei ndogo za mazao. Lazima sis

wote tukubali, Taifa letu au nchi yetu kwa sasa, maeneo yote ya nchi hii tatizo hili ndilo kubwa kwa sasa. Kila kona ya nchi utakuta wananchi wanalamikia suala la kukosa masoko ya mazao na bei ndogo za mazao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru Mheshimiwa Dkt. Mpango umeliona, umeliainisha. Lakini ninachotaka kusema, jambo hili tusipoliwekea mpango thabiti lina athari kubwa sana ya maendeleo katika Taifa letu, tena athari kubwa sana ambayo inaweza ikasimamisha karibu shughuli nyigi ambazo tumezipanga katika Taifa hili. Kwanza uzalishaji utapungua, wananchi watakuwa maskini, wakulima watashindwa kununua mbolea, pembejeo, mbegu, madawa na vilevile hata mpango mzima wa Serikali ya viwanda hauwezi kwenda kama wananchi hawana pesa, zile *products* zinazotoka kwenye viwanda nani atanunua wananchi hawana pesa, rasillimali zitatoka wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo cha msingi lazima tukubali kwamba wataalam wetu sasa umefika wakati wakae na wafanyabiashara wakubwa kutafuta masoko ya wakulima wetu, tunaamini tuna watu wamesomea masoko, hao wana kazi gani. Mimi nadhani wapewe fursa ya kwenda katika nchi mbalimbali kutafuta masoko kwa nia ya kuwasaidia wakulima wetu. Tusipofanya hivyo, yavezekana hata mipango yote hii tunayopanga ikafika mahali ikasimama au ikachukua muda mrefu kwa sababu kama wananchi hawana fedha unategemea nini katika kuendesha Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kushauri uhifadhi wa chakula cha akiba cha taifa. Lazima tukubali, sisi hatuzungumzi na Mwenyezi Mungu, mwaka huu unaweza kuwa na mvua mwaka unaofuata usiwe na mvua au hata mvua zikija zikaja kwa wingi zikaharibu mazao ambayo wananchi wamelima. Sasa cha ajabu nimeona katika mfululizo wa miaka mitatu badala ya kuongeza kununua akiba ya chakula tunazidi kupunguza mwaka hadi mwaka sasa sijajua ni kwa sababu gani, tuna uhakika gani na Taifa likiwa na njaa Taifa hilo halitawaliki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kutoa mfano, kwa mfano 2016/2017 tulinunua tani 62,000; 2017/2018 zikapungua tukanunua tani 28,000; 2018/2019 zikaendelea kupungua, tani 27,000, sasa mimi najuliza hivi sisi tuna uhakika gani na miaka inayofuata kama tutapata mvua na tusipopata mvua lazima tuwe na mpango wa kutunza chakula cha kuhifadhi walau hata miaka miwili/mitatu kama kutakuwa na tatizo la mvua, siyo kwenda kwa kuangalia mwaka mmoja mmoja, hapana, suala hili naomba Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mpango aliangalie. Lazima mpango unaokuja uongeze kununua hifadhi ya chakula kwa maana ya akiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninalotaka kuzungumzia katika upande wa kilimo ni ujenzi wa maghala, naipongeza Serikali imeanza kujenga maghala katika maeneo mbalimbali, lakini maghala hayo yanajengwa sehemu za mjini ambazo barabara zinapitika. Ninashauri sasa tuelekeze mpango wa kujenga maghala vijiji kwenye maeneo ya uzalishaji ambayo wakati mwingine hayapitiki, tukifanya hivyo tutakuwa tumesaidia wakulima wetu kwanza kuwasaidia katika kutunza chakula wakati wanasubiri bei kwa sababu hawana mahali pa kutunza na wakati mwingine wanauza kwa ucharaka kwa kushindwa kutunza, lakini tukijenga maghala kwenye uzalishaji wananchi wataweza kuhifadhi chakula wakavuta subira ili bei zipande. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile barabara zetu siyo nzuri sana kiasi kwamba usipoweka maghala kule mazao yale yanaweza yakaoza. Lakini vilevile itasaidia kuwawezesha wananchi kutunza mazao kwa usalama zaidi. Tumeshuhudia miaka ya uzalishaji mahindi yanaoza wananchi wanashindwa kuyatunza kwa sababu hawana uwezo huo wa kuyatunza, hata namna ya kutunza kwa maana ya kuweka dawa kwa sababu hawana maghala ya kutunzia mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninashauri Serikali katika mpango unaokuja muelekeze ujenzi wa maghala kwenye uzalishaji, kwenye vijiji. Hata kama siyo Serikali unaweza kutafuta wabia wakajenga maghala kwenye

maeneo ya vijiji, wakaweka mkataba na wananchi anapohifadhi mazao wanalipia kidogo, hiyo itatusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kilimo cha umwagiliaji, nadhani miaka mitatu mfululizo kilimo hiki ni kama kimesimama, hata ile miradi ya umwagiliaji tuliyokuwa tumeianza imesimama na mingine imechakaa kabisa. Sasa lazima tutumie haya mabonde tuliyopewa na Mwenyezi Mungu kwa maana ya umwagiliaji, hii itaweza kutusadia sana hata ikitokea ukame mabonde yatatusaidia kwa kutumia umwagiliaji. Lakini naona sasa hivi ni kama miaka mitatu hii mradi huu umesimama; nataka kuona katika mpango huu unaokuja ni jinsi gani Serikali imejipanga katika kuboresha eneo hili la umwagiliaji. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara; niipongeze Serikali kwa barabara zile zinavyojengwa kuititia *TANROADS* zinajengwa kwa uhakika na tunaona Serikali inatoa fedha. Tatizo liliopo kwa sasa ni barabara ambazo zinajengwa na *TARURA*, wana uwezo lakini hawa fedha. Tena kwa hali ilivyo sasa kwa barabara zetu za vijiji ambazo ndiyo maeneo ya uzalishaji ni bora hata wakati zilipokuwa zinasimamiwa na halmashauri zilikuwa zinapata fedha. Lakini kwa sasa pesa hakuna. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Malocha kengele ya pili imeshagonga.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mashukuru, naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Peter Lijualikali atachangia kwa dakika tano, atafuatiwa na Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mheshimiwa Daimu Mpakate ajiandae.

MHE. PETER A. P. LIJUALIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza niseme nimpongeze Mheshimiwa Zungu kwa ambacho jana amekifanya kwa kuongea ukweli na Mheshimiwa Zungu alisema kuwa

wafanyabiashara wanakimbia nchini kutokana na kukosekana kwa mazingira rafiki katika masuala ya kodi na ushuru. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira ya wafanyabiashara katika nchi yetu ni mazingira magumu sana, Serikali ya Awamu ya Tano inafanya biashara katika nchi hii kuwa ni kikwazo, inashindwa kulea wafanyabiashara na nitatoa mfano wa haya mambo yalivyokuwa ni mabaya katika masuala mazima ya kodi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kule kwetu Ifakara tuna mradi wa barabara, huu mradi wa barabara wa kilometra 65 mkandarasi amesaini mkataba na Serikali kupitia Hazina mkataba ambao unamruhusu kuingiza vifaa vyaa ujenzi bila kulipia ushuru wala kodi yoyote. Mkataba huu ndivyo unavyosema hivyo, kazi imeanza vifaa vimefika mkandarasi huyu anakwenda kuchukua vifaa vyake anaambiwa anatakiwa alipe kodi, anasema mimi nimesaini mkataba bila kutoa kodi, *TRA* wanamwambia hatutambui mkataba wako na Hazina. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hatuwezi kuwa Taifa ambalo Serikali moja inafanya kazi kama siyo Serikali. Haiwezekani Taifa hili leo eti *TRA* wanasema hawatambui mkataba wa Hazina, *TRA* inafanya kazi wapi, Hazina inafanya kazi wapi hii ni halib. Serikali lazima iwe *solid*, lazima iwe inamuunganiko, haiwezekani sehemu moja inafanya uwamuzi peke yake huku unafanya uwamuzi peke yake. Na kibaya zaidi huu pia ukiwa ni mfano, leo Mheshimiwa Waziri Mkuu ametoa tamko anawaambia wanunuzi wa korosho anawapa siku nne wasiponuna korosho anafuta vibali vyao vyaa kununua korosho. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuishi kwa kutishia wafanyabiashara, hatuwezi kuleta maendeleo kama tunatishia wawekezaji nyie Serikali hamajiri huu mwaka wa tatu, mmeshindwa kuajiri ingawa mnajisema kwamba ninyi ndo mna hela nyingi sana. Lakini ninyi japokuwa mna hela/ mnasema mna hela lakini mmeshindwa kuajiri, sekta binafsi

ndiyo ambayo ingewasaidia kwenye kutoa ajira, sekta binafsi mnazidi kiumuiza. Hivi mmepima athari ni kiasi gani watu hao watakavyosema kwamba wanatoa fedha zao ambazo zimeingia kwenye nchi yetu zingefanya biashara, wanatoa fedha zao wanakwenda nje, mmepima athari. Lakini kibaya zaidi haya mambo ya korosho...

MHE. MAULID S. A. MTULIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MHE. PETER A. P. LIJUALIKALI: ...ni mambo ambayo humu tulisema na tuliwaambia hapa mtakwama, sasa matokeo...

MHE. MAULID S. A. MTULIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. PETER A. P. LIJUALIKALI: ... yake mmekwama mnaanza vitisho baada.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lijualikali kuna taarifa, Mheshimiwa Mtulia, Mheshimiwa Mtulia.

TAARIFA

MHE. MAULID S. A. MTULIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kumpa taarifa ndugu yangu na mtani wangu Lijualikali ya kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa kama msimamizi na mtendaji Mkuu wa Serikali iko makini na si kwamba tunawatishiwa au anawatishia habari aliyosema ni ya kweli, wasiponunua mazao ndani ya siku nne Serikali itafuta vibali vyao na wakulima wetu watapata kuza korosho zao kwa bei ya faida bila hasara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na katika hili alitishiwi, lengo ni kulinda haki za wananchi wetu wakulima wetu na Serikali imejipanga iko makini usiwe na wasiwasi. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lijualikali unaipokea taarifa hiyo.

MHE. PETER A. P. LIJUALIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema huyu ni mtani wangu sasa na mimi najua ametoka wapi na alifanywa nini mpaka leo yupo hapo alipo. Kwa hiyo, mimi tu nimwambie kwamba kama yeye anaogopa alichofanyiwa mwache aendelee kuogopa ila sisi tupo kazini tutafanya kazi ya wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetishia Waziri katoa vitisho, anawaambia wasiponunua anawafukuza anawanyima vibari vya kufanya kazi hiki ni kitisho na katika mazingira ya uwekezaji hakuna...

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. PETER A. P. LIJUALIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwekezaji mwenye akili ana anayeweza akaja akawekeza kwenye nchi ya hivi, haiwezekani, kwa hiyo mimi niseme....

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti,Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. PETER A. P. LIJUALIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lijualikali kuna taarifa nyiningine Mheshimiwa Getere.

MHE. PETER A. P. LIJUALIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti,linda muda tu.

TAARIFA

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa taarifa kwa rafiki yangu hapo. Sasa naomba labda nipende kujua maana

yake mimi ananipa wasiwasi hapo alipo anatetea wakulima wa korosho au wafanyabiashara wa korosho?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lijualikali naomba umalizie mchango wako.

MHE. PETER A. P. LIJUALIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati nzuri sana nchi inapokuwa ya kidemokrasia, inapoheshimu utawala bora lazima itende haki. Mimi naangalia haki ya mkulima wa korosho, naangalia haki ya mfanyabiashara wa nchi hii. Wote ni watanzania wanahitaji kupewa huduma sawasawa, hii habari ya kusema kwamba mfanyabiashara ni mtu mbaya mtu mwizi mtu ambaye atakawi ni *mentality* ya kimaskini. Huo ni umaskini, wewe kama huna uwezo wa kufanya biashara kaa chini fanya vitu vingine, baki na umaskini wako hivyo hivyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie tena kwamba Taifa letu liko *labeled* kama Taifa ambalo lina hali mbaya katika uwekezaji na katika biashara, kama tutaendelea na hizi tabia, kwa sababu mna mamlaka mnadhani mkafanya chochote, *mkatishia watu na ndiyo maana tunaamini hata haya mengine haya yanatokea haya ya watu kuwa watu wanatekwa tekwa haya mnashiriki, inawezekana kabisa. Kwa sababu kama unasema watu utawatoa.* (*Makofii*)**[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lijualikali, mjisema mnashiriki, wale kina "m", ni kina nani, unaosema "m," mnashiriki kina m wale ni kina nani ili *Hansard* ikae vizuri.

MHE. PETER A. P. LIJUALIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi ni naposema kama mtu anaona halimuhusu basi siyo la kwake, ila kama limemuhusu basi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lijualikali, hili ni Bunge, uslongee lugha za kihuni nani ambaye haimuhusu, umesema mnashiriki kina nani? Ndiyo swali uliloulizwa kama unaweza kulijibu lijibu kama huwezi futa hiyo sentensi yako *simple*.

MHE. PETER A. P. LIJUALIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba kuna mambo mengi yanayoendelea katika nchi yetu hayana majibu, kuna mambo ya wasiojulikana, kuna mambo mengi yanafanyika...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lijualikali *either* unafuta ama unasema ni kina nani ndiyo jambo uliloambiwa ni kina nani wanaoshiriki unawaambiwa mnashiriki, ni kina nani hao *either* useme hao ama ufute, ni jambo jepesi tu na hii ni nafasi ya mwisho unapewa kuhusu hilo.

MBUNGE FULANI: Futa.

MHE. PETER A. P. LIJUALIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hivi kama unataka nifute njoo uongee wewe. (*kicheko*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lijualikali umepewa fursa ya kuongea na kiti usiongee na mtu mwingine, ongea na kiti, usijibizane na mtu mwingine.

MHE. PETER A. P. LIJUALIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimefuta kama naongea na wewe, naona wamefurahia kufuta kwa sababu wanajua, wamefurahia sasa. (*Vigelegele*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lijualikali, naomba ukae. Mheshimiwa Josephine Genzabuke atafuatiwa na Mheshimiwa Daimu Mpakate, Mheshimiwa Katani Katani ajiandae.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kibali cha kusimama ndani ya Bunge hilli jioni hii ya leo.

Naomba nianze kwa kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Jemedari wetu Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri ambazo zimefanyika na nyingine zinaendelea kufanyika katika ujenzi wa reli, ujenzi wa barabara, ununuzi wa ndege nakadhalika. Lakini naomba

nimpungeze sana kaka yangu Mpango na Naibu Waziri kwa mpango wao waliouwakilisha ndani ya Bunge hili .*(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nizungumzie kuhusu kilimo. Kwanza napenda niipongeze Serikali kwa juhudzi ya kufufua mazao ya biashara ikiwemo na zao la mchikichi, pamba, korosho, kahawa, chai na kadhalika. Jambo hili ni zuri sana na linaweza likafufua viwanda na Serikali iongeze juhudzi katika jambo hili. Kwa mfano katika zao la mchikichi ili tuweze kufanya vizuri tunahitaji kutoa elimu ya ushirika wa kilimo cha mchikichi ili wananchi waweze kufanya vizuri wakiwemo na wanawake, elimu inahitajika sana ya somo la ushirika, kwa sababu wasipofanya hivyo kwa mtu mmoja mmoja hataweza kukopeshwa na benki ya kilimo, lakini kwa muungano wa vikundi mbalimbali wataweza kukopesheka na wataweza kuendeleza kilimo cha mchikichi. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo mengine yapo mazao mengine ambayo nayo wananchi walihamasishwa kwa muda mrefu na wakaitikia wito wakaweza kulima na kuzalisha kwa wingi. Kwa mfano wamezalisha mahindi. Lakini kwa mfano kule kwetu Kigoma, tumelima sana zao la muhogo, ni mwangi karibia Wilaya zote, Wilaya ya Kakonko, Wilaya ya Kibondo na Wilaya ya Kasulu. Na Mheshimiwa Waziri katika Wilaya yako ya Buhigwe kule Tarafa ya Mihami nako wamelima sana zao la muhogo. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilikuwa ninanomba kushauri Serikali kwa sababu kwa mfano mwaka jana gunia la kilo 100 la muhogo lilikuwa linauzwa kwa bei ya shilingi 60,000. Lakini kwa mwaka huu zao hilo limeanguka linauzwa gunia moja la kilo 100 kwa shilingi 10 ,000.

Nilikuwa ninaomba Serikali iweze kutusaidia kutafuta soko kwa sababu nimekuwa nikisikia kwamba China kuna Wachina wanahitaji muhogo. Kwa hiyo mimi nilikuwa nashauri Serikali iweze kutafuta soko la muhogo ili wananchi wetu katika maeneo mbalimbali waweze kupata soko la kuuza muhogo na waweze kuzalisha zaidi. Mimi nashuhudia kule

kwetu kupitia kilimo cha muhogo wananchi wamenufaika sana wamejenga majumba mazuri, wanafanya biashara, wanasomesha watoto. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naiomba Serikali yangu itusaidie watu wa Mkao wa Kigoma na Mikoa mingine ambao wanazalisha mihogo soko hilo liweze kutafutwa ili wananchi waweze kunufaika, mimi yakwangu ni hayo, nakushukuru sana, ahsante. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Daimu Mpakate, atafuatiwa na Mheshimiwa Katani Katani, Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed ajiandae.

MHE. DAIMU I. MPAKATE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuchangia mpango kwa siku ya leo. Kwanza naomba nimshukuru Mwenyewezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu na kuzungumza maneno mawili/matatu, pili napenda nishukuru Serikali yangu kwa kufanya mambo matatu yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza kuifanya Kusini sasa iwe inapitika kwa wakati wote kwa maana ya kuwa na barabara za lami kutoka Mtwara mpaka Mbanga na sasa hivi wanatengeneza barabara kilometra 70 zilizobaki kutoka Mbanga mpaka Mbambabay. Nashukuru sana kwa hili kwa sababu limeleta mwanga katika Mikoa yetu ya Kusini. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili kuingiza Mikoa ya Kusini katika mtandao wa umeme wa Gridi ya Taifa, nashukuru sasahivi Mikoa yote ya Lindi na Mtwara na Mkao wa Ruvuma umeingia kwenye Gridi ya Taifa, kwa hiyo tatizo la umeme katika Kanda ya Kusini sasa litabaki historia. Kwa hiyo, jambo hili litatusaidia kwa kiasi kikubwa kuwavutia wawekezaji ambao walikuwa wanashindwa kuja Kusini kwa ajili ya tatizo la umeme. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu naishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi kutujengea maghala 12 katika Mji

wetu wa Songea ili kuhakikisha kwamba mazao ya wakulima kwa maana ya mahindi yanahifadhiwa mahala salama ambapo baadae itasaidiwa kuza kwa maeneo mengine.

Lakini pamoja na shukrani hizo naomba nishauri jambo, tumekuwa na miradi ya kimkakati kwa maana ya kwamba Liganga na Mchuchuma, hatuwezi kuzungumzia bila kuzungumzia reli ya Kusini kutoka Mtwara mpaka Mbambabay. Kutokana na kitabu chako kwa maana ya hotuba ukurasa wa 50 umezungumzia suala la reli ya Kusini kutoka Mtwara mpaka Mbambabay kwenda kwenye *PPP*. Lakini tunavyoona jinsi umuhimu wa chuma ulivyo na namna usafirishaji wa chuma ulivyokuwa mkubwa na pamoja na makaa ya mawe yanayopatikana kule Ngaka, kuna umuhimu wa jambo la reli kuangalia kwa upande mwingine badala ya kutumia *PPP* kwa sababu *PPP* kwa maana ya kwamba hatutakuwa na *final say* katika kutoa huduma kwenye reli hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ningependa kuzungumzia suala la kilimo, hasa tukizungumzia habari ya pembejeo. Nimefurahishwa sana na namna ya mtindo wa kununua pembejeo kwa pamoja ambao umesaidia upatikanaji wa pembejeo kwa wakati mmoja. Lakini napenda nitoe ushauri miaka ya nyuma Serikali ilikuwa inatoa ruzuku kwenye pembejeo hizi. Bei ya pembejeo imekuwa ni kubwa sana ule utaratibu wa kutoa angalau kiasi ili kupunguza bei ya mkulima naomba Mheshimiwa Mpango ufanye chini juu ili kuwapunguzia makali ya bei ya pembejeo katika maeneo mengi. Tukichukulia mfano wa salfa mwaka huu wakulima wamenunua 32 kwa bei ya Serikali kama Serikali ingekuwa imetoa ruzuku wakulima wangeweza kununua chini ya hapo. Kwa hiyo, *purchasing power* ya wakulima na uzalishaji ungekuwa ni mkubwa zaidi kuliko tunavyojitegea sasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ambalo nilikuwa nataka nilizungumzie kwenye miradi ya kimkakati kwenye mashirika hasa yanayoshiriki kwenye miradi ya kimkakati kwa mfano ilivyo *TANESCO*. *TANESCO* kama

ingekuwa ni shirika la mtu binafsi sasa hivi limekufa kwa sababu ya utilii wa madeni uliokuwa nao. Ninaomba Serikali kama inawezekana kuinusuru *TANESCO* kwa kuondoa madeni yake kwa maana ya madeni waliyokuwa makubwa yachukuliwe na *TANESCO* na iwezeshe *TANESCO* kuweza kufanya kazi yake kibashara. Ipunguzieni *TANESCO* mzigo wa kulipia bomba la gesi kutoka Mtwara, bomba la gesi kutoka Songsongo ili waweze kuhudumia wananchi kwa urahisi na baadae kupunguza bei ya umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo tunazungumza suala la Mchuchuma na Liganga kwa upande wa *NDC*, tumekwama wapi. Kwa sababu ni muda mrefu sana na hawa wenzetu wameingia mkataba na kampuni ambayo inaonekana kama ni uwezo wakeni mdogo. Ni kwa nini Serikali isiweze kufanya kama ilivyofanya kwenye shirika la *ATCL* kuchukua mtaji, mimi naamini ndege moja tu thamani yake inaweza kuisadia Linganga na Mchuchuma ikaweza kufanya kazi ipasavyo. Naomba Serikali kwa namna ilivyo umuhimu wa Liganga na Mchuchuma, chuma ni mahitaji makubwa katika nchi hii, tunahitaji chuma kwa ajili ya ujenzi wa reli, tunahitaji chuma kwa ajili ya kujenga Bwawa pale *Rufiji Agro Power*. Kwa hiyo naomba sana jambo hili mliangalie kwa namna ya kipekee ili kuhakikisha kwamba *NDC* wanaondokana na kile kifungu walichofunga na wale wawekezaji ambao uwezo wao umeonekana ni mdogo kuweza kuanza kufanya uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye *TTCL*; *TTCL* ni shirika la umma, lakini ndili linalomiliki mkongo ambao ni wa Serikali kwa asilimia 100 na wanaosaidia kwa namna moja au nyingine kuweza kuhudumia lakini cha ajabu Serikali inashindwa kuisaidia *TTCL* iweze kuhudumia mkongo ule. Naomba sana Serikali inusuruni *TTCL* iwasaidieni percent ya mapato yanayotokana na mkongo ili waweze kuhudumia mkongo ule kwa ajili ya mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo niliona ni muhimu katika kuchangia ni suala la barabara ya kutoka Songea - Makambako...

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa, kengele ya pili imeshagonga. Mheshimiwa Katani Katani atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Keissy, Mheshimiwa Ahmed Shabiby ajiandae.

MHE. KATANI A. KATANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kukupongeza kwa kuniona, lakini pia nongoosee jitihada za Serikali ambazo zimefanywa na Waziri Mkuu kwenye suala la korosho, lakini mwisho na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akafika kwenye kikao kile cha wafanyabiashara na akatoa jambo ambalo kwangu binafsi nimefarijika nalo kwa sababu kulikuwa na bei elekezi ya shilingi 1,550 ambayo Mheshimiwa Rais baada ya kuzungumza na wadau wale wa korosho, wanunuizi ameliondoa jambo hilo na naamini litaendelea mwakani hatutakuwa na jambo hilo la bei elekezi kwa sababu linatupa shida sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini njaribu kuzungumzia suala hili la korosho ambalo ukisoma ukurasa wa 29 kwenye mapendekezo ya mpango Waziri wa Fedha ameleezea vizuri sana juu ya ongezeko la fedha kwenye sekta ya kilimo na tunapozungumza sekta ya kilimo tunaizungumzia korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipata kusema na nataka nirudie kusema leo tena kwenye jambo hili, leo zipo kauli za Serikali ambazo zinazungumzwa kwa ajili ya kumlinda mkulima tunayemzungumzia ikiwepo na kauli ile ya kusema Serikali ina uwezo wa kununua korosho yenewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe tu kwamba korosho tunayoizungumza kwa Mikoa ya Lindi ukienda maeneo ya Nachunyu toka mwezi wa nane wakulima wameshaweza kuokota korosho zao na kuzipeleka kwenye vyama vya msingi. Maeneo ya kwetu kuanzia mwezi wa tisa korosho hizi tayari zimeshafika maghalani. Waziri Mkuu mmesikia wakati anatoa taarifa tuna tani zaidi ya 78,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, korosho hizi zina mambo mengi; moja, upo wakati wakulima wanakopa fedha benki kwa ajili ya pembejeo. Leo tunapozungumza riba zinazidi kuongezeka tukiwa tunasubiri Serikali kununua korosho kama ilivyosema. Lakini nilipata kushauri jambo, unapomlazimisha mnunuzi kununua korosho wka shilingi 3,000 maana yake *export levy* ni 450 kutoka kwenye ile *15 percent* ya *export levy*. Serikali inahitaji fedha, nilishauri na nashauri tena; kwa nia njema ili Serikali ipate fedha badala ya kuingia kwenye mtego wa kununua mnaweza mkaamua, mkatoa shilingi 250 au shilingi 200 kwenye ile *export levy* shilingi 450 mnayoipata mkawaambia wanunuza kama mngesikiliza vizuri mnunuzi yule ambae alikuwa anazungumza na Mheshimiwa Rais alishauri jambo na pendekezo lake hamkulifanyia kazi vizuri.

MS holding wakati anazungumza na Rais alikuwa amezungumza suala la kupunguza *export levy* kutoka kwenye hiyo *15 percent* kwa mwaka huu siyo miaka yote kutegemea na hali ya soko ambayo na Serikali mnakiri kwamba soko la korosho halijatengemaa.

Jambo hili mkilifanya kwanza mtakusanya *export levy* ambayo ninyi wenyewe mnajua inatusaidia kwa kiwango kikubwa lakini pili, mtawapa fursa wanunuza kununua zile korosho badala ya hii hadithi tunayokwenda nayo ambayo mnaamini kwamba mnaweza kuzinunua korosho zile wakati ipo miradi imesimama kwa kukosa fedha. Ni ushauri wangu kwako Mheshimiwa Waziri, kuna fursa kubwa ya kukaa na Mheshimiwa Rais na Waziri Mkuu mkaangalia namna mbadala, badala ya kuwapa siku hizo mlizowapa ni jambo jema kama mtawapa siku nne halafu baada ya siku nne kama hawakununua kama milivyopendekeza kwamba kila mnunuzi atoe takwimu anahitaji kununua korosho tani ngapi basi mkaangalie *possibility* ya kununua korosho zile. Tunapozungumza hali ya Mtwara ni mbaya mno, hali ya Lindi ni mbaya mno, hali ya Pwani ni mbaya mno. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Iakini wakati huu mnazungumza suala la shilingi 3,000 mmesahau kwamba korosho zina *grade*. Korosho ya Mtwara ni tofauti na korosho

ya Pwani. Korosho ya Pwani ukienda kuibangua, *nut count* unaweza ukapata 250 mpaka 300 tofauti na ya Mtwara ambayo *nut count* unaweza ukapata 150. Kwenye *out turn* ukienda korosho ya Mtwara utapata 51, 52, 53, ya Pwani utapata 47, 45, korosho hizi bei haiwezi kuwa sawa. Inawezekana kabisa mlivyosema 3,000 mnazungumzia korosho za *grade* ya kwanza ambazo tunalima sisi watu wa Mtwara, Lindi ambazo parizi zetu tunazifanya za kutosha sana tofauti na wenzetu wa Pwani ambao hata ukienda kuangalia korosho yao ubora wake hauko sawa sawa na bei zake haziwezi kuwa sawa.

Kwa hiyo, kungekuwa na uwezekano pia wakati mnatoa matamko mseme shilingi 3,000 korosho ya daraja la kwanza, labda shilingi 2,200 au shilingi 2,100 korosho la daraja la pili ambazo Pwani ndiyo korosho zao wanazo pale, pengine wao wangeendelea kuuza korosho...

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. KATANI A. KATANI: ...nadhani hili ni jambo ambalo mnatakiwa kulifanyiakazi kwa namna ya pekee sana.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa, taarifa, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Katani naona watu wa Pwani wanataka kukupa taarifa. Mheshimiwa Naibu Waziri, Mbunge wa Mkuranga.

T A A R I F A

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namheshimu Bwana Katani, nafahamu anajua vizuri tasnia ya korosho na mimi nilikuwa nafikiri wkamba ye ye angeendelea kuishauri Serikali vizuri katika jambo zima la ununuzi na ufuatiliaji wa biashara ya

korosho. Hii kusema wkamba biashara ya korosho Pwani hawana korosho za *grade A* siyo kweli. Sisi kila mwaka tunauza korosho za *grade A* katika Wilaya ya Mkuranga, tunauza korosho za *grade A* katika Wilaya ya Kibiti, tunauza korosho za *grade A* katika Wilaya ya Rufiji na kwingineko.

Kwa hiyo yeye ajielekeze katika kutafuta suluhu ya jambo hili lakini kuzungumzia kwamba Pwani hakuna *grade A* siyo kweli. Tunayo *grade A*, tunazo pia za *grade B* na za *undergrade* zipo vilevile lakini siyo kweli kwamba hakuna kabisa ya *grade A*. Ajielekeze katika kuwatetea watu wake wa Tandahimba, watu wake wa Mtware na watu wake wa Lindi. Hii biashara ya kuzungumzia Mkoa wa Pwani haina *grade A* nadhani haina maslahi kwake kwa aina yoyote.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Katani unaipokea taarifa hiyo?

MHE. KATANI A. KATANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, niipokee taarifa ya ndugu yangu hapo kwa sababu anawatetea wakulima wake, lakini ninachokizungumza anakijua vizuri na kama alivyosema inawezekana naijua korosho mara 500 kuliko yeye na anajua mwaka jana *grade two* ambayo milioni 800 watu wanadai fedha kwenye vyama vyao kule kwa ajili ya ubora huu tunaozungumza kwahiyohata ukimuuliza hicho ninachozungumza *out turn* na *nut count* anaweza asilie kwasababu hajazama kwenye hiyo korosho tunayoisema, kwa hiyo nadhani likae vizuri hivyo. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Katani mimi nataka nikushauri kwa sababu haya mambo...

MHE. KATANI A. KATANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeelewa, nimepokea

MWENYEKITI: ...kuna jamii kule nje nadhani...

MHE. KATANI A. KATANI: ...nimepokea tuache watu wa Pwani...

MWENYEKITI: ...hata kama hauipokei lakini wewe nyoosha tu maelezo yako ili isije ikaonekana kama wewe unapanga makundi humu ndani ya nani analima korosho nzuri, nani analima mbaya.

MHE. KATANI A. KATANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kitabu hiki cha mapendekezo ya mpango nilikuwa najaribu kuangalia sana suala la miundombinu ambalo wenzangu wengi wameweza kulisifia, lakini kwangu ambako ndiyo wazalishaji wakubwa wa korosho na nilipata kusema mara kadhaa na niombe tu Dkt. Mpango unapoleta mpango wenyewe sasa tuone mkakati sasa wa barabara ile ya kutoka Mtwara ambayo mmeanza kilometra 50 ambazo kilometra mbili ndiyo zina lami mpaka sasa tuone kwamba mnaweka kwenye mpango. Kwenye kitabu cha mpango mtakacholeta Februari tuone barabara ile ambayo wazalishaji wa korosho kwa miaka yote wanaliingizia pato Taifa wanatembea kwenye vumbi na mnafanya wafanyabiashara kuitoa korosho Tandahimba kuleta Mtwara gharama iwe kubwa, yaani ukiangalia leo kusafirisha mzigo kutoka Dar es Salaam kupeleka Tandahimba na kutoa mzigo Newala kupeleka Mtwara unakuta Mtwara gharama ni kubwa kwa sababu ya barabara mbovu, lakini barabara ambayo hata zile fedha tulizokuwa tunalalaimika za *export levy* mngeamua kufumba macho tu mkasema kuweka lami, mngeweka lami na mngemaliza barabara ile na wakulima wakaona kwamba na wao mmewasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni maombi yangu kwako Dkt. Mpango kwamba utakapoleta mpango sasa tutaona barabara ile mmeipa kipaumbele bahati nzuri mnaiita barabara ya ulinzi. Ina mambo mengi; iko mpakani, mna kila sababu ya ile barabara kuiweka lami kwa ajili ya maslahi ya Taifa mapana sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Dkt. Mpango nimeona wenzetu kwenye ukurasa wa 33 umezungumzia suala la usafiri wa majini. Nimeona Ziwa Tanganyika, nimeona Ziwa Victoria, nimeona

Nyasa wenzetu wamepata fursa kubwaya kutengenezewa Mameli, ni jambo jema kabisa kabisa na mimi naunga mkono. Lakini sisi watu wa Mtwara tuna kiwanda kikubwa cha DANGOTE kiwanda kikubwa Afrika cha saruji. Leo tunatumia magari haya ya lusafirisha saruji kuleta Dar es Salaam na naeneo mengine tunaharibu na barabara hizi. Nione sasa kwamba kama kuna uwezekano na fedha zipo, basi na Mtwara pawepo meli angalau ya tani 200 tuwe tunasafirisha saruji ile kuleta Dar es Salaam ili kuzilinda na barabara zetu ziwe ziko kwenye mazingira mazuri na msiwe mnapeleka peleka fedha *TANROADS* kwa ajili ya kurekebisha barabara ile, mtakuwa mesaidia sana. Miaka ya 1987 mpaka 1997 tulikuwa na meli ya MV Maendeleo pale ilikuwa inafanyakazi vizuri sana na bahati nzuri kama mtaleta meli hizo zinaweza zikasaidia nchi za jirani za Comoro. Wanahitaji kufanya biashara na Tanzania, maeneo mazuri, bandari nzuri ni Bandari ya Mtwara, kama mtaona inafaa kwa maslahi mapana ya Taifa mkatuangalie na Mtwara pale pakawa na meli ambayo inaweza ikafanya shughuli ya usafirishaji.

Lakini Dkt. Mpango tulivyoingia hapa 2016/2017 kulikuwa na mradi wetu wa *LNG*, Lindi pale. Kila ninaposoma kitabu cha mapendekezo ya mpango kila mwaka tumeanza, story yake ni ile ile tu kwamba nfanya majadiliano na watu kadhaa, sasa majaliano haya *duration*yake ikoje? Tutamaliza tu miaka mitani mnafanya majadiliano au ndiyo jambo lile Mtwara limesahaulika tumaenzisha program nyingine ya *Stiegler's Gorge*? Ili nivyema kama halipo msiwe mnaliwekweka tukawa na matumaini, maana mnatupa matumaini hewa sasa ni bora...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa
Mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Katani kengele ya pili imegonga. Mheshimiwa Ali Keissy atafuatiwa na Mheshimiwa Ahmed Shabiby, Mheshimiwa Khadija Aboud ajiandae

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi jioni ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu kwanza utajikita namna Serikali yetu iokoe fedha za kigeni, kwanza tujitahidi sana ulimaji wa mbegu za mafuta ya kula. Mkoa wa Singida upewe kipaumbele kwa ajili ya alizeti, Mkoa wa Kigoma upewe kipaumbele kwa ajili ya michikichi. Tuokoe pesa za kigeni kwenye nchi yetu na sisi hela yetu ioate thamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, *TAZARA* tunaimaliza, tunaiua *TAZARA*. *TAZARA* kusema kweli ni ukombozi kabisa kwenye nchi kupeleka mizigo Malawi, kupaleka mizigo Zambia na DRC Congo. Leo ukienda pale Tunduma magari hayana idadi unahesabu mpaka unachoka. Yanasaidia kuharibu barabara vilevile yanasakiya kabisa kwa hali ya juu kabisa kupoteza hela ya kigeni kwa ajili ya kutumia mafuta kwa wingi. Kwa hiyo tukiifanya *TAZARA* iwe kipaumbele kwa ajili ya kusaldla mizigo kwenda Zambia, kwenda DRC Congo na Malawi tutaokoa kabisa hela za kigeni kwa ajili ya kuagiza mafuta nje. *TAZARA* inakwenda inaumia. Ukifika pale njiani kwanza ukiona Tunduma kwenye ukiangalia magari zaidi ya 700 au 800 yanalala pale Tunduma, ukifika pale Makambako au sehemu zingine mbao zimejaa kwa ajili ya kwenda Dar es Salaam hazina usafiri. *TAZARA* tunaiacha, tunaionna. Kama tunashindwa ndugu zangu tuwape Wachina. Tuwape Wachina waendeshe treni sisi tuokoe barabara zetu na tuokoe mizigo tupate masoko ya Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, Ziwa Tanganyika. Hii meli kila siku mkataba tutajengewa meli. Ziwa Tangayika tumpakana na nchi tajiri katika Afrika DRC Congo Mheshimiwa Waziri wewe mwenyewe unafahamu Congo kuna hela za ajabu kule. Kuna Mji wa Kalemii, kuna Moba, kuna Uvira na sehemu za Burundi. Ile meli inaweza kutuletea pesa za kigenikwa ajili ya kusafirisha mizigo kwenda nchi hizo, lakini tumekaa tu sisi hatujengi meli tumekaa kwenye makarasi mikataba itasainiwa lini? Tupe tarehe maalum hii itakuwa tayari na mikataba iko tayari tunataka tujue meli yetu ya Ziwa Tanganyika. Zamani meli ilikuwa inahudumia mpaka Kalemii, Uvira, Moba mpaka Mpulungu inapeleka mafuta leo hakuna kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoteza hela za kigeni tunaagiza vitu vya ajabu ajabu. Mpaka leo ukienda madukani unakuta mchele wa kihindi uko madukani wakati mchele umejaa nchi nzima hela yatu inapotea. Vitu vya anasa tunaagiza mpaka kope na kucha. Enzi ya Mwalimu Nyerere nakumbuka ilikuwa kabisa tunaagiza vitu muhimu kwa binadamu, hatuagizi vitu vya anasa kucheza hela za kigeni. Tunauza pamba, tunauza korosho kwa hela za kigeni, lakini leo tunakwenda China tunaagiza vitu vya ajabu ajabu inakuwa nchi yetu dampo, tunakosa kabisa udhibiti wa hela yetu ndiyo maana dola inaanguka thamani kila siku kwa sababu tunaagiza vitu havina thamani na vitu *reject*. Juzi nimeona pikipiki mimi pale barabarani; *helmet*mpya jamaa kaweka *helmet* juu ya pikipiki inadondoka chini inapasuka *helmet*, hela ya kigeni tunapoteza. Masimu *fake*, *radio fake*, ukipita barabara hii ya Dodoma *one way* kila kitu *fake* lakini yote ni hela za kigeni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *TANESCO*tunaomba mradi wa Gridi ya Taifa haraka sana Mkoa wa Rukwa, Katavi na Kigoma. Leo *TANESCO* tu imeshakuwa inaokoa kila mwezi dola milioni 82.3; kila mwezi inaokoa kwa ile Mikoa ambayo sasa imefungwa Gridi ya Taifa, kuokoa mafuta ghafi. Tulikuwa tunatumia mafuta kwenye mitandao kule Songea, sijui Makambako leo inaokoa *TANESCO*dola milioni 83 kwa mwezi. Sasa ndugu zangu tufanye haraka ili umeme huo uende mpaka Mikoa ya Rukwa, Katavi na Kigoma tuache majenereta tunapoteza hela za kigeni.

Ndugu zangu, wakulima wanalima hamuwasaidii mbolea, hamuwasaidii pembejeo, mkulima akilima mnafunga mipaka, mnafungua mipaka masoko ya nje yameshajaa mazao, faida yake ni nini? Kwamba mnataka mkulima ndiyo *guarantee*ya kuzalisha mazao ili kusaidia wale jamaa wavivu wasiolima haiwezekani, hii haiji kabisa kwenye akili ya binadamu, haiji. Mkulima kama unataka Serikali/Hifadhi ya Taifa inunue mazao, yale mengine haraka iwezekanavyo kabla ya nchi za Kenya, Burundi, sijui Malawi, South Sudan haijapata mahindi kutoka kwingine mnafungua

masoko wakati mahindi yameshatoka Kenya yamejaa katika nchi zingine, ndugu zangu hatuendi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkulima anabeba mzigo, leo mkulima mnasema mbolea imejaa mkulima hana uwezo wa kununua mbolea, tukubaliane ukweli kabisa. Atauza mahindi gunia ngapi anunue mfuko wa mbolea? Kwa hiyo ndugu zangu kilimo kitakenda kupungua, wakulima watakata tamaa kwa sababu uwezo wa kununua mbolea sasa hawana. Mazao yao mpaka leo ukienda kule Rukwa leo gunia shilingi 18,000, mbolea shilingi 70,000 auze magunia mngapi apate mbolea. Huyu wa shilingi 18,000 humpati na hana uwezo hata wa kutia hata dawa. Kwa hiyo, nawaomba ndugu zangu, msimu ukifika fungueni kila mtu auze. Leo mnasema mmefungua vibali lakini kupata hicho kibali chenyewe ni shida, hupati kwa haraka haraka. Mtu wa kijiji ana tumahindi twake mpaka uende Sumbawanga wakuzungushe hapo hapo wakutake na pesa haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza habari ya manununzi na Waziri wa Fedha uko hapa, manunuzi ndiyo mzizi wa kuiba hela katika nchi hii. Hawa wanunuzi wetu hawa wa hii miradi miradi hii wanaiba pesa za ajabu. Mimi nalalalmika kila siku hapa miradi ya maji wengine wananiambia mimi muongo. Juzi tu wametuma watu ule mradi wa bilioni 7.5, wataalam wamekwenda kuona ule mradi ni bilioni 4.4; billioni tatu nimeokoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kaagalie mabwawa wanayochimba kule, miradi ya maji wanakochimba kule ndugu zangu, Rukwa kule tumekuwa kama tuko Burundi wanatuibia miradi hii kiradi wanunuzi hawa ndiyo wa kuangalia sana Mheshimiwa Mpango.

Naomba kabisa wawe wanasema *certificate* zimekuja, *certificate* wakaguliwe kwa hali na macho tena uvae miwani ya macho manne. Haiwezekani *certificate* inakuja unalipa dakika moja hela, mna wizi ndani yake. Lazima kuhakiki miradi ya Serikali mara mbili, mara tatu kuna wizi wa hali ya juu. Hawa ndugu zangu wanataka kutucheka

upande wa pili wenyewe wanadandia treni kwa nyuma, wakisikia kitu tayari wameshadandia. Juzi Makonda kasema habari ya mambo ya kwenda kinyume na maumbile tayari wana-support. Nakwambia angalia sana watu kama hao, ni watu hatari. Wana-support viti vya ajabu ajabu, leo kakataa Waziri wa Mambo ya Ndani hatuungi mkono hoja, anayetaka kuleta misaada yake kama mambo ya namna hii aache kuleta misaada yake, nchi hii ina viongozi, ina kila kitu hatuwezi kukubali. Kusema kweli haiwezekani, Serikali...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Keissy muda wako umekwisha.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Keissy sisi wamama humu ndani hatujakuelewa ule mchango wako wa kucha na kope, nadhani tutatafuta muda kwasbabau sisi tunazihitaji hizo jamani. Tunaendelea na Mheshimiwa Ahmed Shabiby, Mheshimiwa Khadija Aboud ajiandae.

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi nataka kuchangia kidogo lakini nilikuwa sitaki kuchangia habari ya korosho kwa sababu silimi, lakini napata mashaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napata mashaka naona hili suala linaleta mlolongo mrefu sana hebu naomba Serikali ifanye uchunguzi. Hizi korosho mpaka leo wanazo wakulima, wanazo walanguzi? Nataka hili tu.

Je, nani anayetaka kufaidika sasa hivi kwa ununuzi wa korosho? Wanazo wakulima wenyewe walengwa au wanazo walanguzi? Hebu Serikali ifanye uchunguzi wa kina ili tufahamu hili suala halafu muwasaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu la kwanza kuanza kuchangia ni muhemko wa mipango yetu, korosho mwaka jana zimepanda bei kule Mtwara na Lindi mwishoni tumeletewa miche mpaka Dodoma, Gairo wapi, wote tupande korosho, kwa kupanda tu kwa msimu mmoja lakini tumeletewa sehemu zote. Sasa nilikuwa naomba katika mipango yetu ya Serikali tuangalie twende kwa *zone*/kwa ukanda tunajua kabisa ile miche iliyoletwa kwenye mikoa hii ya kanda ya kati pamoja na Morogoro kama mngetuletea mbegu za alizeti tungefanya vizuri zaidi kwenye alizeti kwa sababu ndio maeneo yetu kuliko mnatuletea sisi miche ya korosho mwishowe itakuwa kuni huku. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tuende kwa *zone* tuangalie Nyanda za Juu Kusini wanataka nini, tuangalie Kanda ya Ziwa leo hii kule pamba bado wenyewe wanatafuta soko leo mnaleta pamba zillimwe huku hebu tujaribu kuangalia hii mipango tusifanye vitu kwa mihemko tu kwa sababu watu wengine wanatafuta sehemu ya kula wanayohusika, wanajua hapa tunazalisha miche ya korosho basi imepanda kule 4000 kilo tayari Gairo, Dodoma korosho wakati watu hawajui hayo mazao, naomba iwe hivyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ni masuala ile sheria iliyopitishwa na Bunge ya *VAT* kwenye mitambo ya viwanda. Sheria ya Bunge ilipitisha kwamba mitambo yote ya viwanda iwe na *exemption* ya *VAT*, lakini kilichotokea kanuni zilipotungwa kule ziliwekwa kwamba mitambo hiyo lazima ianzie milioni 20 kwenda mbele ndio apewe *exemption* leo hii kuna wakulima wadogo unaposema milioni 20 kwenda mbele ina maana unawawekea wafanyabiashara wakubwa ndio wafaidike, wafanyabiashara wa chini ya milioni 20 hawawezi kuleta mtambo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano mtambo leo wa kusindika nyanya ni dola 6000 ukienda India, ukienda China kila mtu anao uani hapa hawezи kufanya huyo mkulima mdogo, mtambo wa kukobia kahawa ni dola 6000, 3000, 4000 lakini mfanyabiashara mdogo au mkulima mdogo

hawezi akanunua. Mashine ya kutengeneza misumali ni dola 5000 lakini mkulima au mfanyabiashara mdogo hawezi kufanya, kwa hiyo, tumeangalia viwanda na tunataka iwe nchi ya viwanda tunaangalia wale wa kubwa tu hawa wadogo hatuwaangalii kabisa, hebu tuangalie na leo vijana wana akili sana waliomaliza hapa vyuo vikuu lakini unaanza kumpa *exemptonakifika* milioni 20 nani atafanya biashara kama sio sisi hapa, ndio maana yake. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu kingine kupanga ni kuhagua hamuwezi mkaanzisha viwanda bila kuwa na umeme. Mimi bahati nzuri nilikuwa mmoja katika ile Kamati ya Richmond wakati ule iliyofanya mambo ya Richmond. Tatizo la umeme nchi hii ni shida sana na ile Kamati tulishakwenda mpaka Marekani mpaka kila sehemu, wenzetu kule wanafanya mpango wa aina yoyote wahakikishe Tanzania inakuwa na umeme wa bei mbaya. Umeme leo hapa ni dola senti 11 lakini sehemu nydingine ni 0.3 halafu unataka uanzishe Kiwanda hapa cha *Tiles*, Kiwanda cha *Tiles* kile mpaka leo bei yake bado mbaya kuliko bei ya kwenda kuchukua China kwa sababu ya bei ya umeme kama huu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo umeme wa maji kwa *unit* ukiweka bwawa zuri ni shilingi 36, umeme wa gesi uko shilingi 147, umeme wa mafuta uko shilingi 530 na bado Tanzania tunalipa *capacity charge* kwenye mitambo ya watu, na nini bado watu hamtaki tujenge bwawa la *Stigler's Gorge*. Tatizo ni nini kuna watu wanapewa pesa na hizi nchi zingine pasiwe na umeme tufanye vitu ambavyo vitaleta *impact* ya sasa hivi kwamba mwanchi wa Gairo anataka kuona *impact* yake kwamba umeme anaununua karibu na bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaanzisha viwanda hatuna umeme, watu tuna kazi hapa sijui kuna ndege wanatua pale wanaruka ruka, kuna chura wanakula majani lazima tujipange nasema hivi Serikali mkiwa waoga kutoa maamuzi au mkitaka matokeo yenu ya uzuri wa Serikali ya awamu fulani yaonekane kwa sasa hivi mtafeli. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yoyote makini inafanya kitu kwa ajili ya kitu cha maendelezo, ukiweka leo bwawa au mbele na kuendelea wataona umuhimu wake, tusiwe tunafanya vitu labda kumfurahisha mtu leo tu, leo mimi sina hela mfukoni unataka uuingie uanze kufurahisha. Niwapeni mfano tu Mheshimiwa Rais hapa alitangaza kwamba mtu yoyote atakayesema ana njaa afe, sasa kuna mtu kafa mbona hatuoni mtu aliyesema ana njaa hapa. Tuache hayo mambo ya kubembelezana kwenye maendeleo. Unaambiwa lima mtama wewe unalima mahindi ukipata njaa unapelekewa mahindi unatakiwa ukiambiwa lima mtama ukipata njaa upelekewe mtama ule hata kwa nguvu utakula tutajifunza kulipa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nataka niwaweke wenzangu ndugu zangu hawa tufanye vitu vya maendeleo ya baadae na tuwe makini na hilo tuache haya mambo ya sasa hivi mtu awe ametosheleza sijui unataka uone hela mfukoni sasa hivi, hapana tuangalie mambo ya mbele yana umuhimu gani na hili Taifa. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana.

Mheshimiwa Mpango nadhani na Wizara ya Kilimo ni muhimu kweli kufanya utafiti juu ya haya mazao yanayopelekwa maeneo mengine hasa kwa kuzingatia namna soko linavyoenda kama tumesikia hapo kwamba kule *West Africa* kokoa imeshuka bei sijui na korosho nako kule zimeshuka, sasa kila sehemu nchini ambako kuna hali ya hewa inayolingana wakilima mazao yanayofanana nadhani kama Taifa tutashindwa *ku-balance* maisha yetu kwa sababu wakilima hawa mahindi yakiwa bei juu korosho zitakuwa bei chini, korosho zikiwa bei juu mahindi yakishukua kama Taifa tunaweza kuenda vizuri.

Lakini wote tukilima mahindi, wote tukilima korosho, wote tukilima zabibu nadhani kusonga mbele itakuwa kidogo ngumu. Kwa hiyo wale watafiti wetu watusaidie kabla hawajapeleka taarifa kwa wakulima, wakulima wote tunaanza sasa kulima korosho sasa tukisikia habari za kina

Mheshimiwa Katani hapa kidogo zinatupa taabu huko duniani.

Kwa hiyo, wataalam wetu watusaidie na kwa sababu sasa hivi ndio mnaanda mpango kwa ajili ya 2019/2020 itasaidia kuleta huo muelekeo mzuri na mimi naamini wataalam wako wako tayari kwenye kuanda mpango wa miaka mitano mingine kwa sababu sasa hivi tuko kwenye miaka mitano na itaisha 2020, miaka mitano mingine waanze kuangalia kama nchi tunataka kuendaje kwenye eneo la kilimo, ahsante sana.

Mheshimiwa Khadija Aboud atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Ngalawa, Mheshimiwa Seif Gulamamli ajiandae. (*Makofi*)

MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa na mimi fursa ya kuchangia machache katika hotuba hii ya mpango. Kwanza na mimi napenda kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa hatua yake ya kuletea Taifa hili maendeleo kwa wananchi wa Tanzania. Lakini pia naipongeza Wizara ya Fedha Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara ya Fedha kwa kukaa na kujadili na kupitisha mpango huu na kutuletea sisi Wabunge ili tuongeze nayma kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mchango wangu napongeza vipaumbele vyote ambavyo tumeletewa, lakini naomba tu niongezee msisitizo kwenye mambo madogo yafuatayo; kwanza kwenye maji, nashauri kwenye maji mfuko wa maji uongezwe fedha ili kusaidia maji kwa wananchi ambaao wapo vijiji zaidi na kwenye maji pia nasisitiza Mheshimiwa Waziri pia tuupe kipaumbele mfumo wa uvunaji wa maji ya mvua kwa maana hapa tutahitaji miundombinu ili kuhamasisha wananchi wavune maji ya mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea nakwenda kwenye sekta ya uvuvi. Kwenye sekta ya uvuvi naishauri

Serikali itupie jicho zaidi kwenye uvuvi wa bahari kuu kwa kujenga bandari za uvuvi Bara na Zanzibar na pia kununua meli za uvuvi. Na katika kuhamasisha huu uvuvi na kuimarissha nashauri Serikali ilijengee uwezo Shirika la *TAFICO*, linakabiliwa na changamoto nyingi kwa kuwa miundombinu yake ni chakavu, gati zimeharibika, maghala pa kuhifadhi samaki na kutengeneza barafu hakuna kwa hivyo tukiwekeza hapa kwenye Shirika hili la *TAFICO* kazi hii ya uvuvi itafanyika na itaongeza pato la Taifa, litamsaidia mwananchi kupata ajira na kuongeza kipato ikiwemo pia kununua meli za uvuvi kwenye bahari ya kitaifa na bahari kuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sekta hiyo ya uvuvi pia nashauri Serikali iongeze fedha kwenye ukuzaji wa viumbe kwenye maji. Kwenye sekta ya viumbe kwenye maji si ufugaji wa samaki tu, kuna mambo mengi ambayo yanafanywa kwenye viumbe kwenye maji ikiwemo kuzalisha madini yenye fedha nyingi madini ya lulu ambayo tutaweze kuuza nje tukapata fedha za kigeni, tukaongeza ajira kwa vijana wetu, lakini pia tukaboresha maisha ya wananchi, pia tuaongeza usalama wa chakula na lishe bora kwa wananchi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa MWenyekiti, sekta hii ni sekta ambayo haitumii nguvu nyingi kama kilimo, kwa hiyo vijana na wanawake wakihamashwa, wakawekewa mazingirabora na wezeshi wataweza kujiingiza kwenye sekta hii ya ukuzaji wa viumbe kwenye maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikielekea kwenye kilimo nashauri Serikali tuwekeze pia kwenye kilimo cha umwagiliaji na kwenye kilimo cha *greenhouse*, hapa tuweke mazingira wezeshi ya kuangalia kodi na tozo mbalimbali kwenye miundombinu hii ya *green house* na umwagiliaji ili wananchi wanawake, vijana wajiiingize kwenye sekta hii ya kilimo na waweze kuipenda na kuimudu. Pamoja na hilo pia kuongeza huduma za ugani, mbegu bora na pia kuimarissha barabara za vijini ambazo zinachukua mazao ya wananchi kuyapeleka kwenye maeneo husika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali na Wizara ya Kilimo kwa sasa hivi mbolea ipo na inapatikana na wananchi watatumia kipindi hiki cha msimu wa kilimo kwa wakati. Sambamba na hilo Serikali pia ijiongeze katika kujenga viwanda vyetu vya mbolea hapa nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuimarisha vitengo vyetu vya utafiti ili tuweze kupata mbegu bora kwenye kilimo, kwenye mazao yote ya mifugo na mazao mengine ya biashara na mazao yetu mengine ya kula sisi wenywewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sekta ya maziwa naomba Serikali iangalie kodi na tozo mbalimbali ambazo zinawakumba wawekezaji wa sekta ya maziwa ili waweze kuwekeza kwenye sekta hii ya maziwa, maziwa ambayo yanadumu kwa muda mrefu ili na sisi tuweze kusafirisha nje ya nchi kuingizia Taifa fedha za kigeni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye upande wa mazingira ni vyema sasa tukajiwekeza zaidi kwenye uhifadhi wa mazingira na ulinzi wa mazingira. Ulinzi wa mazingira pia unategemea matumizi bora ya ardhi ambayo yatazingatia uhifadhi wa mazingira, kwa mfano, tunapohamasishana kwenda kulima tunapojingiza kwenye ukulima wa mbogamboga, vijana au wakulima wa mbogamboga wanakata miti, wanaondoa uoto wa asili, lakini tunalima mbogamboga. Kwa hiyo, hili ni jambo la kulizingatia na kulipangia mipango madhubuti ni ipi ardhi ya kilimo, ipi ardhi ya ufugaji, ipi ardhi ya kuhifadhi maziringira yetu uoto wa asili, ipi ardhi ya ujenzi na ipi ardhi ya viwanda tukijipanga hivyo tutaweza kuokoa miti yetu isikatwe hapa ni vitu vya kulizingatia kwa umakini zaidi, kwa sababu wakulima wanapohamasishwa kulima wanakata miti na wanaondoa uoto wa asili pia hili linachangia pia uharibifu wa mazingira. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine naendelea kuishauri Serikali kuweka mazingira wezeshi kwa wawekezaji wetu wa ndani na wa nje...

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa kengele ya pili imeshagonga ahsante sana. Mheshimiwa Deo Ngalawa atafutatiwa na Mheshimiwa Seif Gulamali, Mheshimiwa Venance Mwamoto ajiandae.

MHE. DEOGRATIUS F. NGALAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuchangia mpango wa maendeleo ambao umewasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mpango. Kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja na pia nipende kuishukuru Serika kwa kutuletea huu mpango ambao unaonyesha kabisa unadhamira njema kwa Taifa letu. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wa kati, ambapo kwa sasa sera yetu inatupelekea kwenye uchumi wa viwanda, viwanda hivi haviwezi kusimama vyenyewe, lazima tuwe na *link* ili tuweze kwenda kwenye uchumi wa viwanda kwanza ni lazima tuwe na nishati ya uhakika. Kwa hiyo Serikali inapozungumza suala la *Stigler's Gorge* maana yake ina *i-link* na viwanda, kwa hiyo wazo la *Stigler's Gorge* limekuja kwa wakati na ninaamini kwamba ili tuweze kuwa na mfumo wa vidanda vingi ni lazima tuwe na nishati ya uhakika. Kwa hiyo, mimi nipende kuishukuru Serikali katika suala hilo ni lazima liwekewe kipaumbele cha kutosha. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia lazima tuwepo na miundombinu tumeona barabara nyingi zikijengwa nchi nzima kwenye maeneo ambayo ni ya kilimo ambako ndiko ambapo uchumi wetu mkubwa uko maeneo hayo, tumeona mawasiliano ya simu nchi nzima na hilo pia linapelekea kwamba kwenye *connection za market hatutakuwa na tatizo kubwa*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la viwanda haliwezi kuwa mbali na kilimo ni lazima tuweke miundombinu mizuri kwenye maeneo yetu ya kilimo ambako ndipo malighafi zitakapotoka kwa ajili ya kwenda ku-service viwanda vyetu.

Kwa hiyo ni lazima Serikali ijpange vizuri kwenye eneo hili la kilimo kwenye maeneo ambayo yana kilimo kikubwa ili tuwe na kilimo cha uhakika, tuwe na kilimo cha umwagiliaji ili malighafi ambazo zitatumika kwenye viwanda ambavyo tunakusudia kuvijenga zitoke ndani ya nchi na tuweze kupungu za malighafi ambazozinaweza zikatoka nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumza bajeti au tunapozungumza mpango, tunazungumzia mapato na matumizi, niongelee kwenye eneo la mapato. Mapato yetu yote karibu yanatokana na kodi sasa mimi napenda kujiuliza elimu ya kodi wanaielewa kwa kiasi gani kwa sababu ya historia ya kodi huko nyuma enzi za ukoloni watu wanaiona kodi ni kama kitu ambacho hawasatahili kukilipa. Kwa hiyo, nipendekeze kwa Serikali sasa kodi iwe ni *mainstream* kuanzia *primary school*, sekondari mpaka kwenye vyuo vikuu kwa sababu ile elimu ya kodi hiyo inafahamika mtu ajue kwamba kodi kulipa iwe ni *prestige* na wala isiwe kwamba ni analazimishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iweke utaratibu wa kutoa elimu ya kutosha kwenye kodi na ikiwezekana iwekwe kwenye *syllabus* za shule zetu. Tunayo miradi kielelezo miradi ya Liganga na Mchuchuma nimeiona dhamira ya Serikali juu ya miradi hii ya Liganga na Mchuchuma kwa kuweka kwamba wanataka kuanza sasa kujenga Kiwanda cha Kufua Chuma cha Liganga, chuma hicho ambacho kitasaidia sasa kutengeneza taaluma nyangi kwa ajili ya *standard gauge* ambazo zitatumika kutengeneza reli zetu hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili ninaweza kulithibitisha kwa sababu ya zile barabara ambazo zinaenda kwenye migodi hiyo ya Mchuchuma na Liganga tumeona upembeuzi yakinifu na usanifu wa kina umekamilika tarehe 13 oktoba mwaka huu kwa barabara ya kutoka Madaba kuelekea Mkyu kuititia Liganga na pia tumeona barabara ya kutoka Mchuchuma kwenda kule Liganga zote upembuzi yakinifu umeshakamilika na tayari Serikali imelipa bilioni 1.79, huu ni mwelekeo mzuri kwa nchi kwa sababu hii tumeshaiita

ni miradi kielelezo na miradi kielelezo ni lazima kweli iwe ni kielelezo kizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado haya mazungumzo ambayo yanazungumzwa na mwekezaji ni lazima yawe na *time frame*. Tumekuwa na muda mrefu na mkubwa sana kwa kuzungumza na huyu mwekezaji mpaka sasa kiasi ambacho naona kwamba imechukua muda mrefu. Mimi niiombe Serikali mazungumzo haya yaharakishwe na mwisho wa siku kwamba hii miradi sasa ianze. Kwa hiyo mimi naiona dhamira nzuri na dhamira kubwa ya Serikali yetu katika miradi hii ya Mchuchuma na Liganga kama ambavyo mmeiweka kwenye mpango 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nizungumzie suala la maeneo ya uzalishaji hasa *gape* ambalo lipo nchini tunalo *gape* la mafuta ya kula, tunalo *gape* la sukari, tunalo *gape* la uzalishaji wa mbolea, tunalo *gape*, tunalo *gape* hata la ngano, haya yote kwa kiasi kikubwa tunayachukua nchi za nje, mimi nadhani sasa Serikali iweke mpango mkakati kwenye maeneo maalum ya uzalishaji wa hivyo vitu, ili tuliondoe hili *gape*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuondoa hilo *gape* maana yake Serikali itakuwa imetengeneza *balance of trade* nzuri na kuondoa ile *imbalance* ambayo sasa hivi inaonekana ipo kwa sababu vitu hivi vina uwezekano mkubwa wa kufanyika hapa nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono hoja na asante kwa kunipa fursa. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Seif Gulamali atafuatiwa na Mheshimiwa Sebastian Kapufi, Mheshimiwa Timotheo Mnzava ajiandae.

MHE. SEIF K. S. GULAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi leo niweze kuchangia mpango wa maendeleo wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nipeende kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na uwepo wangu wa siku ya leo, lakini kingine niweze kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mpango kwa kutuletea Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa ajili ya kuweza kulijenga Taifa letu liweze kuwa imara zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina mambo matatu ambayo ningependa kushauri ama kuchangia kwenye mada ambazo Mheshimiwa Mpango ameweza kuwasilisha kwenye mpango wake wa maendeleo. Ukiangalia katika ule ukurasa wa 27 ambao amezungumzia masuala ya kuboresha shirika la ndege la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha hili shirika letu la ndege nina mambo makubwa matatu ambayo ningependa Mheshimiwa Mpango aweze kuyachukua haya mambo makubwa matatu ambayo ningependa kuyawasilisha kwa siku ya leo, ni ushauri kwangu. Katika ukurasa huu tunaona kwamba Mheshimiwa Mpango anatuonesha kwamba shirika letu la ndege sasa litaanza safari zake kutoka Tanzania kwenda Guangzhou, China, lakini pia litaenda nchini India ni pongezi kubwa sana na ni hatua kubwa sana ya maendeleo katika Taifa letu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunapokwenda kwenye anga za kimataifa maana yake shirika letu linafanya biashara na katika biashara maana yake ni lazima tutengeneze mazingira ya kuingia kwenye soko la ushindani katika mashirika makubwa ambayo yanafanya biashara duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, achilia mbali shirika letu kuna mashirika jirani ambayo yanafanya kazi kama za kwetu ambazo tunataka kuzifanya. Kwa mfano, ukichukulia Shirika la Ndege ya *Kenya Airways*, *Rwanda Airways*, *Ethiopia Airways*, haya ni mashirika ambayo tunashindana nayo kwa ndani katika Afrika, lakini yako mashirika makubwa ambayo tunakwenda kushindana nayo, haya ni kama vile Emirates, tutaenda kushindana na mashirika kama Etihad, tunaenda

kushindana na mashirika makubwa kama *KLM* katika ushindani wa anga za kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nini ushauri wangu? Serikali hapa inatakiwa iliangalie vizuri hili shirika, kwanza katika kuli-*support running cost* linapoanza mwanzoni. Safari hizi mwanzoni tutakuwa na hasara hatutakuwa na faida kwa hiyo, lazima Serikali ibebe gharama za kuhakikisha kwamba shirika letu la ndege linakuwa na uhakika wa kusafiri kutoka hapa kwenda China kwa uhakika wa siku zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko siku ambazo shirika litakosa abiria, linaweza kuamua kuiahirisha safari zake, likahirisha maana yake linavunja uaminifu kwa wateja wake, lakini ni lazima Serikali ihakikishe uaminifu wa shirika letu unaendelea kuwepo na ili uweze kuendelea kuwepo ni lazima Serikali iwekeze fedha kuhakikisha kwamba, shirika hili la ndege linaendelea kufanya safari zake hata kama ni kwa hasara lakini lazima Serikali iweke fedha hata kama ni kwa mwaka mzima likiendelea kuligharamikia kwa sababu kufanya hivyo itasababisha wateja waliamini shirika hili na kuweza ku-*maintain* soko la kidunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ambalo ningependa Mheshimiwa Mpango mlichukue, lazima katika hili shirika kuwepo na *visa on arrival* katika nchi ambazo tunapeleka ndege zetu hizi. Kwa mfano, tunachukua ndege yetu tunapelaka China, ili mtu wa China atoke China aje Tanzania tunaenda Guangzhou, mtu atoke Guangzhou aende Beijing kutafuta *visa*, ni jambo ambalo kwa mchima na watu wengine wa mataifa yale inakuwa inawawia vigumu sana kwa hiyo, ni lazima tutengeneze utaratibu wa watu wanaotoka Guangzhou wakipanda ndege yetu kuja Tanzania wapate *visa on arrival* wakati wakifika Dar es Salaam. Kwa hiyo, lazima tutengeneze mazingora rafiki ambayo yataweza kusababisha ndege yetu iweze ku-*maintain* kupata wateja katika mataifa haya itakayokwenda kwa mfano China pamoja na India kwa hiyo, lazima tuweke *visa on arrival*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuweka *visa on arrival* maana yake lazima *immigration* ifanye kazi kwa ukaribu zaidi na hawa watu wanaofanya kazi hizi za ndege ili kuondoa usumbufu kwa wateja. Lazima wateja waliamini shirika letu kwa sababu tunaenda duniani, tunakutana na mashirika makubwa kama haya. Na hii itakuwa ni *unique service* kwa mashirika mengine kwa mfano mtu atakuwa yuko China anakuwa ana-optkupanda *Air Tanzania* badala ya kupanda Emirates na *Ethiopian Airline* kwa sababu akipanda *Air Tanzania* anakuwa na *visa on arrival*. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mpango chukua hili jambo na muingize katika programu yetu ambayo itasaidia kuhakikisha kwamba, ndege yetu, shirika letu hili linaweza ku-*maintain* soko la kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine, shirika letu lina madeni. Lazima Mheshimiwa Mpango uhakishe kwamba, shirika hili katika kuliendesha haya madeni yaliyokuwepo siku za nyuma, shirika hili lilikuwepo ukiangalia historia, lilikuwepo mwaka 1977 ilivunjwa ile *East Africa* tukawa na ATC, ATC kaja tukavunja 2002 tukawa na ATCL. ATCL ikaanzia pale ikaingia ubia na *South Africa Air*, lakini pamoja na hayo ilikuwa na madeni makubwa ambayo yako, haya huwezi kuyatenga haya madeni, lazima haya madeni tuyabebe kama Serikali tuchukue jukumu la kulipa, tukiliachia shirika, shirika hili litakufa kabla ya wakati.

Kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Mpango madeni yaliyoko ndani ya shirika Serikali iyabebe ihakishe kwamba, inahakikisha kwamba, inapunguza uzito wa kuendesha shirika letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kingine tukisimamia shirika letu itasababisha ukuaji wa utalii katika nchi yetu, itasababisha ukuaji wa biashara katika Taifa letu, kilimo na masuala mengineyo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mpango katika suala zima la kuendesha shirika la ndege lazima utengeneze mzingira rafiki ambayo yatasaidia shirika letu liweze ku-*survive* katika anga za kimataifa, lakini pia, katika anga ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchangiaji huohuo uende sambamba na huduma bora katika viwanja vyetu vya ndege. Tunashuhudia tunapoenda pale *airport* wakati mwingine unasafiri umebeba zako ntalali, unabeba nswalu, umebeba asali, umebeba vitu kama vile samaki, umebeba vitu vidogovidogo ambavyo unabeba sio vikubwa sana unatokanavyo nje ya nchi, ukifika pale wanakwambia lazima uende *TFDA*, sijui uende wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania sisi tukienda kwenye mataifa ya nje ndio haya tutakayoyabeba, tukienda nje ya nchi tutabeba simu tutakujanazo, kwa hiyo, vipo vingine vya kuangaliwa kupelekwa kwenye *TFDA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kingine ukienda kule mitaani...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Muda umekwisha Mheshimiwa.

MHE. SEIF K. S. GULAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuunga mkono hoja, lakini naomba sana waangalie hili suala zima la ndege za usafirishaji. Ahsante sana, naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Sebastian Kapufi atafuatiwa na Mheshimiwa Timotheo Mnzava, Mheshimiwa Juma Nkamia ajiandae.

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi nianze kwa kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na suala la kufungamanisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu ukurasa wa 47 wa hotuba ya Waziri nilikuwa na mimi nakubaliana na maeneo yafuatayo kwa maana ya kupeleka kipaumbele katika eneo la elimu na ujuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakapoendelea kuwasomesha watu wetu tija inakuja katika sura ifuatayo, mbali ya kwamba wasomi hawa, wajuzi hawa watakuja kufanya kazi nyumbani, lakini tukiwa na mpango mzuri wa kuwapa elimu watu wetu watu hawa wanaweza wakaenda nje ya nchi wakapata ajira huko na baadae kitakachofanyika ni wao kutuletea fedha nyumbani, hili linafanyika maeneo mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano wenzetu wa Misri maeneo yao ya mapato yanapatikana katika maeneo yafuatayo kwa kupitia kilimo, kwa kupitia utalii, kwa kupitia gesi asilia, lakini kwa kupitia mapato yanayotokana na Mfereji wa Suez na mwisho kabisa ni watu ambaeo wamepata kazi nje ya nchi na wanarudisha fedha nyumbani kwao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hilo, nilichokuwa naomba mipango yetu na katika hili mara ya mwisho niliwahi kuzungumza hapa Tanzania tuna bahati moja kwa kupitia kiswahili, kiswahili ambapo sisi tunaonekana ni Waziri katika eneo hilo. Hilo ni eneo lingine tukijikita vizuri huko nje ya nchi tukawa na mpango mahususi kwamba Watanzania hawa wakapate ajira nje ya nchi ambako kiswahili linahitajika kwa Kiwango kikubwa, narudi kwenye *point* yangu hiyo kwamba kwa kupitia watu hawa ambaeo wamepewa ujuzi watarudisha fedha nyumbani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoke hapo niende katika eneo lingine, kuna suala la idadi ya watu na mabadiliko ya maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi hapa nilikuwa naomba nipaweke vizuri, sipingani na suala la idadi ya watu, lakini ninachohitaji kusema tunaweza kuwekeza kwa kupitia idadi ya watu na hapa nilikuwa naomba niliweke vizuri zaidi, Watanzania ambaeo sasa hivi tunakwenda takribani milioni 55 mipango yetu isipoangalia idadi ya watu maana yake suala la idadi ya watu sio kitu kibaya, lakini idadi ya watu inaongezeka zaidi ya rasilimali, ndio tatizo langu linakuja hapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii kwa maana ya idadi ya watu kama mipango yetu haitaliangalia tuna zaidi ya 59% ambao ni vijana na mara ya mwisho kwenye kongamano lililofanyika Astana, Kazakstan linasema hivi mwakani na miaka mingine inayokuja kutakuwepo na ongezeko kubwa hasa la vijana kwa Bara la Afrika. Kwa hiyo, Tanzania hatuwezi tukajiweka kama kisiwa ni lazima mipango yetu iendelee kuangalia huko tunafanyaje na idadi hii ya watu, hasa vojana? Je, tuna mipango ya kuwekeza kwa vijana? Hilo nilikuwa naliomba sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba nitoke hapo na katika hilo pia, nilikuwa nasema mipango yetu tusiwaache *diaspora* ni watu muhimu sana kwenye kusababisha uchumi wa nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba nizungumzie suala jingine linalogusa madini na katika hili kanuni zinatuelekeza kama una maslahi yanayogusana na fedha utamke hapa, ni kweli mimi ni mchimbaji wa madini na ninapata fedha kwa kupitia eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na ushauri ufuatao, tumepitisha sheria nzuri sana ya masuala ya madini, lakini nilikuwa naomba mipango yetu katika eneo la madini hatuwezi tukawaacha wachimbaji wadogo peke yao bila kuwawezesha na kwa taarifa wachimbaji hawa wadogo wakiwezeshwa uwezekano mkubwa wa kuchangia pato la nchi hii ni mkubwa, lakini nilikuwa naomba niende mbali zaidi pamoja na kupitisha ile sheria mimi nilikuwa naomba tunayo *GST*, tusichukulie nchi yote ina namna moja ya mwamba, wataalam waendelee kutusaidia katika eneo la madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwamba wa eneo la Katavi unaweza ukawa ni tofauti na mwamba wa Shinyanga, ni tofauti na mwamba wa Mwanza, ni tofauti na mwamba wa Tanga. Kwa hiyo, wote wakiwekwa kwenye kapu moja wataalam wanakuwa hawajatusaidia na kwa maana hiyo maana yake hata tutakapozungumzia kiwanda cha uchenjuaji, namna utakavyoweza kuchenjua Tanga ni tofauti

na utakavyoweza kuchenjua Katavi kwa sababu miamba inatofautiana. Kwa mfano Katavi unaweza ukakuta katika mwamba kuna madini ya shaba, kuna madini ya fedha, kuna madini ya dhahabu, sasa hawa wote unapowaweka kwenye kapu moja mimi nasema hapo kwa maana yampango yetu tunakuwa hatujakaa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba niendelee kuzungumzia suala la uvuvi. Nimejaribu kupitia nchi mbalimbali ambazo zimefanya vizuri, moja ya eneo ambalo watu wamefanya vizuri ni eneo hili la uvuvi. Kwa mfano Seychelles ambao wao ni wa pili kwa maana ya utajiri Afrika sehemu kubwa ya uchumi wao ni kwenye uvuvi na ni uvuvi wa huyu samaki anaitwa jodari. Mimi nilikuwa nasema na sisi kama Watanzania mipango hii tuelekeze huko kuna ukanda mkubwa wa bahari, tunayo maziwa, tunayo mito, ni eneo kubwa ambalo tunaweza tukapata fedha za kigeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa naiona taabu, hebu angalia nimejaribu kupitia nchi zote zinazoonekana uchumi wao ni mzuri, wanafanya vizuri katika zile nchi 10 tajiri, sehemu kubwa utakuta ni utalii, utakuta ni uvuvi, utakuta ni madini ambayo na sisi kama Watanzania vitu hivyo tunavyo, tatizo liko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni suala la mipango. Kwa hiyo, nilikuwa nakuomba sana Waziri wangu wa Fedha tukirudi kwenye mipango; kwa mfano wenzetu wa Misri kwa kupitia Mfereji wa Suez wanapata mapato, sisi kwetu Bandari ya Dar es Salaam, bandari nyinezo katika Ziwa Tanganyika inaweza ikawa ni sawa na Mfereji wa Suez ikawa ni chanzo kikubwa cha mapato. Na Watanzania siku zote nikipata nafasi ya kuchangia hapa nasema tumebarikiwa, eneo la utalii peke yake, kwa mfano leo *South Africa* ambayo nayo inazungumzwa wanakwenda vizuri kwa maana ya uchumi sehemu kubwa ya uchumi wao ni kwa kupitia utalii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kuziangalia nchi zote hizi. Ukizungumzia Misri mbali ya kukwambia kilimo, ukiangalia utalii, *natural gas*, lakini ukija mtu wa Botswana

na yeye pia anakwambia ni eneo la madini, vyote hivi tunavyo kwa hiyo, taabu iko wapi? Labda naweza nikazungumzia ni suala la kupanga na vipaumbele kwamba tunakusudia tuanze na nini? Wapi iwe ni sehemu yetu ya kipaumbele?

Mheshimiwa Mwenyekiti, madini...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kapufi kengele ya pili ilishagonga. Nilitaka umalizie mfano wako mzuri wa Afrika Kusini. Ahsante sana.

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Timotheo Mnzava atafuatiwa na Mheshimiwa Mattar kwa dakika tano na Mheshimiwa Neema Mgaya ajiandae.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia na kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama kwenye Bunge hili kuchangia, naomba uniruhusu nitumie nafasi hii kwanza kabisa kumshukuru Mungu kwa mambo makubwa aliyonitendea, ikiwemo uhai, lakini pia kunipa nafasi ya kuweza kuwepo kwenye jengo hili siku hii ya leo, lakini pia nikishukuru sana chama changu chini ya Mwenyekiti wetu, Rais wetu John Pombe Magufuli kwa kunipa nafasi ya kuwa mgombea wake na hatimaye kuja wawakilisha watu wa Korogwe Vijijiini kwenye jengo hili. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii pia kumpongeza sana kwa dhati Mheshimiwa Rais na Serikali nzima kwa kazi kubwa wanayoifanya. Serikali ya Awamu ya Tano inafanya kazi kubwa sana na sisi sote ni mashahidi, kila mwenye macho anaona hilo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri, lakini pia kwa mpango huu mzuri ambao ameuwasilisha kwetu. Mimi nilipotazama mpango huu na kuusoma vizuri nimeona una mambo makubwa mawili; jambo la kwanza mpango huu unaonesha kabisa nia ya dhati ya Serikali kuwahudumia watu wake kwa maana ya kufungamanisha uchumi na maendeleo ya watu, lakini jambo la pili mpango huu unatoa, unakoleza ile nia yetu kama Taifa ya kwenda kwenye uchumi wa kati, uchumi wa viwanda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapotaka kwenda kwenye uchumi wa kati, uchumi wa viwanda, lazima uangalie vitu vikubwa viwili, lazima kwanza uangalie namna ya kuboresha miundombinu wezeshi, lakini pia uangalie namna ya kuboresha miundombinu saidizi. Ukiangalia vizuri mpango huu ambao umewasilishwa kwetu umejikita vizuri sana kwenye kuzungumzia namna ya kuwezesha na kuboresha miundombinu wezeshi. Tunapozungumzia ujenzi wa reli, tunapozungumzia mradi mkubwa huu wa umeme, yote hii ni miundombinu wezeshi kwa ajili ya kuwezesha Serikali yetu na nchi yetu kwenda kwenye uchumi wa kati, uchumi wa viwanda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niitie tu moyo Serikali kwamba kwenye jambo hili msisikilize sana haya maneno. Hizi kelele zipo na zitakuwa nyingi sana, lakini kuna watu ambao hawatamani kuona tukifanikiwa kwenye mambo ya namna hii. Tuendelee kuchapa kazi, Watanzania huko nje tulikotoka mimi nimetoka huko nje, inawezekana huku ndani wengine walikaa muda mrefu hawakusikia wananchi wanachokisema huko nje, huko *site* watu wanachotaka ni maendeleo, huko *site* hatusikii Katiba, huko *site* hatusikii kitu gani, watu wanataka maendeleo, wanataka kuona nchi inakwenda mbele, Serikali iendeleee. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze kidogo kwenye upande wa kilimo. Karibu asilimia 90 mpaka 95 ya malighafi ya viwanda inategemea kilimo, kilimo ni kitu muhimu sana, lakini pia tunao vijana karibu 60% ambao wanahitaji ajira.

Wanaweza kujajiri vizuri sana kwenye kilimo, lakini pia tukifanya vizuri kwenye kilimo Wananchi wakulima wakipata kipato tunatengeneza pia soko kwa ajili ya bidhaa za viwanda yetu sisi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kwenye mpango uliowasilishwa na Serikali kwenye ukurasa wa 39 unazungumzia kuimarisha, kujenga na kuboresha miundombinu ya umwagiliaji. Ni lazima tukubaliane sote kwamba, ni kweli hatuwezi tukalima kwa kutumia mvua peke yake, miundombinu ya umwagiliaji ni kitu muhimu sana na ninafurahi kuona imewekwa kwenye mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba nitoe angalizo. Tumekuwa na miradi ya umwagiliaji kwenye baadhi ya maeneo ambayo imejengwa chini ya kiwango, mingine haikufanya vizuri sana, lakini pia ili tuweze kufanikiwa kama Taifa kwenye hii miradi ya umwagiliaji lazima pia tuangalie aina ya miradi na ukubwa wa watu wanaofaidika na miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakupa mfano kwenye Wilaya yetu ya Korogwe, tunao mradi wa Bonde la Mto Mkomazi ambao ungetekelezwa ungeweza kusaidia karibu kata 10 mpaka 12. Ni mradi mkubwa sana ulibuniwa tangu enzi za akina Marehemu Shekilango, lakini mpaka leo ule mradi haujatekelezwa. Naomba sana Serikali, kwenye kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji, tuangalie miradi mikuwa namna hii inaweza kunufaisha watu wengi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye jambo hili la kilimo pia na sisi sasa tuangalie sana kwenye namna ya kupata mbegu bora. Tunao Wakala wa Mbegu wanafanya kazi nzuri sana kwenye zile mbegu ambazo wanazalisha, na mbegu zao ni nafuu. Naomba Serikali iangalie namna ya kuendelea kuijengea uwezo Wakala wa Mbegu ili waendelee kuzalisha mbegu nzuri kwa ajili ya Wakulima wetu na wale wakulima wa hali ya chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo hiki tunachokisema hakiwezi kwenda bila miundombingu mizuri. Nimeona kwenye mpango wa Serikali kwenye ukurasa wa 45 wa mapendekezo ya mpango, tunazungumzia namna ya kutengeneza miundombinu ikiwemo barabara kwa ajili ya kufungua fursa za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ningeomba nishauri hapa, tusiangalie kutengeneza barabara kwenye kufungua fursa ya kiuchumi kwenye maeneo mapya tu. Tunayo maeneo ya uwekezaji maeneo ya uzalisha ya miaka mingi ambayo pia miundombinu yake inahitaji kutazamwa sana. Kwa mfano ukienda Korogwe kwenye Tarafa ya Bungu, kuna Kilimo Kikubwa sana cha chai, lakini barabara imekuwa ni shida, inafika mahali mvua ikinyesha hata trekta tu kwenye kukusanya chai inashindwa kwa sababu ya ubovu wa barabara. Ningeomba Serikali iangalie sana kwenye maeneo ya namna hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongee jambo lingine kwenye eneo ya mifugo. Wakati napitia mapendekezo ya mpango kwenye mapitio ya utekelezajiwa awamu iliyopita, nimeona Mheshimiwa Waziri amezungumzia kuboreshwa kwa Kituo cha Taifa cha Uhilimishaji (*NA/C*) kwenye ukurasa ule wa 18. Mimi nimewahi kufanya kazi Arumeru, ni kweli *NA/Cinafanya* kazi nzuri sana na naipongeza Serikali kwa hilo. Lakini kwenye mpango wa miradi ya kipaumbele tumeenda kuzungumza kwamba Serikali inasema tutaboresha Vituo vya Uhilimishaji vya Taifa na Kikanda. Lakini viro vituo vingine vya uhilimishaji vidogo kwenye maeneo mengine na kuna maeneo vimejengwa bado havijaanza kutumika mpaka leo na hela ya Serikali imetumika. Ningeomba kwenye mpango tuangalie tuisiishie tu kwenye Kituo cha Kitaifa na vituo cha Kanda, tuangalie na vituo vingine vya uhilimishaji ambavyo vinaweza kuwafikia wananchi wakaviflikia kwa ukaribu na kwa urahisi zaidi ili vibororeshwe viweze kuwasaidia watu wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine naomba kushuri kwenye mpango huu ni kwenye upande wa viwanda.

Nimeona kwenye ukurasa wa 38 tunazungumzia kuhusu kujenga viwanda, lakini tunakubaliana wote kwamba Serikali ilifanya kazi kubwa ya kuchukua viwanda kwa baadhi ya wawekezaji ambao walishindwa kuviendeleza. Ningeomba kwenye mpango tuweke utaratibu mahususi kabisa wa namna gani viwanda ambavyo Serikali imevichukua kutoka kwa wawekezaji walioshindwa kuviendeleza wanaweza kuvifufua na kuvitafutia wawekezaji sio kujenga tu viwanda vipyta peke yake. Mfano mzuri ni kiwanda cha *Tembo Cheap Board* kilichopo kwenye Wilaya ya Korogwe eneo la Mkumbara, kiwanda kipo kwa mwekezaji ameshindwa kukiendeleza, Serikali imekichukua, ningefurahi sana kuona mpango mahususi wa Serikali namna ya kutafuta tena wawekezaji au namna ya kufanya viwanda vile vianze kufanya kazi vizuri ili viweze kuwasaidia watu wetu kwenye maeneo yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba nizungumze kidogo kuhusu baadhi ya mazao. Juzi nilisikia mchangiaji mmoja alichangia vizuri sana kuhusu zao la chai. Kuna maeneo mengi sana tunalima chai kwenye nchi yetu na chai ni zao muhimu. Lakini kumekuwa na changamoto kidogo kwenye zao la chai hasa kwa upande wa pembejeo. Wakulima wetu kwenye baadhi ya maeneo wamekuwa wakitegemea kukopeshwa na viwanda vinavyonunua chai ili kuweza kupata pembejeo kwa ajili ya kilimo cha chai na hii inawanyima hata kwenye kuja kuuza kwenye bei, hapa natoa mfano kwa wakulima wa kule Korogwe, eneo la Bungu wamekuwa wakitegemea kukopeshwa na kiwanda kinachonunua chai ili wapate pembejeo kwa ajili ya kuviendeleza zao la chai. Ningeomba Serikali tuwe na mpango mahususi wa kusaidia upatikanaji bora wa mbegu, lakini pia pembejeo kwa ajili ya kuboresha zao la chai kwenye maeneo yetu ili kuweza kuwakomboa na kuwainua wakulima hawa kwenye maeneo haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba nimalizie kwa kusema Mwalimu Nyerere kwenye kitabu chake cha Tujisahihishe kwenye ukurasa wa sita alisema; "Kosa letu kubwa ni kufanya mawazo yetu na matakwa yetu kuwa

matakwa ya raia" wako baadhi ya viongozi wenzetu ambao wakijua kwamba jambo wanadoliletu kwa wenzao halitakubaliwa wanakimbilia kusema ni mawazo wananchi au ni mawazo ya raia na mara nyingi watu hawa wanakuwa hawajazungumza wala kukubaliana na hao raia ambao wanawazungumza hapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Serikali yangu, kuna watu ambao wanakuja kusema wananchi huku wanataka hiki, wanataka hiki, wananchi wetu wanachotaka ni maendeleo, wananchi wetu wanachotaka ni huduma za elimu, wanataka huduma za afya, wanataka huduma za miundombinu, wanataka huduma za umeme, hawataki kingine, na hicho ndicho wanachojiandaa kutuhukumu nacho sisi wanasiwa wote mwaka 2020. Nawaomba sana Wanasiwa wenzangu tuache kuwasingizia wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja nakushukuru sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mbunge mgeni kabisa huyu mara yake ya kwanza kuchangia naona Mheshimiwa Mpango ameandika yote aliyoyasema, hongera sana Timotheo.

Mheshimiwa Mattar dakika tano, tutamalizia na Mheshimiwa Neema Mgaya. (*Makofii*)

MHE. MATTAR ALI SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii, lakini nichukue nafasi hii kumpungeza sana Dkt. Mpango kwa kazi nzuri anayoifanya. Mheshimiwa Dkt. Mpango, ni kweli kama Mbunge aliyepita amesema Watanzania shida yao ni maendeleo. Lakini Mheshimiwa Mpango nikushauri kidogo ili uweze kunisikiliza, lazima Serikali tuanzishe ukusanyaji wa mapato, tuweze kudhibiti mapato yetu na tuanzishe vyanzo vipyta vya ukusanyaji wa mapato ili tuweze kufika mahali wananchi wanapopataka. Lakini mimi nichukue nafasi hii kukupungeza sana kwa kazi ambayo umeifanya Dar es Salaam katika kudhibiti yale makontena.

MWENYEKITI: Waheshimiwa upande wangu wa kushoto hebu muachenii Mbunge mgeni amemaliza kuchangia, huko ndiko alikopangia kitii.

MBUNGE FULANI: Tumefanyaje?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hawa huja fanya chochote, niliowaona wanafanya hivyo ndio ninaowaambia, kama unataka niwataje naweza pia kuwataja nimewapa heshima, ndio maana nimesema upande wangu huu muachenii Mbunge amechangia alivyoona yeeye inafaa. Mheshimiwa Mattar.

MHE. MATTAR ALI SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba dakika zangu unilindie.

Mheshimiwa Dkt. Mpango, nchi yetu bado inahitajika udhibiti wa ukusanyaji wa mapato, lakini vile vile na bado kunahitajika ongezeko la vyanzo vya ukusanyaji wa mapato, kwa mfano Mheshimiwa Mpango nitaitaja kwa ufupi kwa sababu muda wangu ni mchache. Mheshimiwa Mpango kuna shilingi 50 kwenye *petrol* na *diesel* ambayo inatakiwa kwenda kwenye miradi ya maji, kusema ukweli Mheshimiwa Mpango hii fedha inahitajika. Na ukija katika mpango wako tukuombe sana tumekuwa tukikushauri sana, basi hii fedha shilingi 50 kwa maslahi ya Watanzania ili kuokoa Watanzania wengi wapate maji safi ili shilingi 50 hii iweze kupatikana. Hilo la kwanza. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, kuhusu fedha zinazokwenda Zanzibar za kujenga *airport terminal three*. Mheshimiwa Mpango, *airporthii* imekwama kwa muda mrefu na nafikiri umeshafanya mazungumzo na Waziri wa Fedha wa Zanzibar, mmeshakubaliana. Taarifa iliyokuwepo ilikuwa Julai uweze kupeleka zile fedha au umalize yale mambo ambayo ile *airport* iweze kutengenezwa, lakini umesema mpaka leo utaratibu uko kwa Mwanasheria Mkuu. Tunakuomba sana Mheshimiwa Dkt. Mpango hili suala la *airport* la Zanzibar ndio kitega uchumi ambacho kinatakiwa na kinategemewa na Wazanzibar na Watanzania wote

wanaoishi Zanzibar. Nikuombe sana hili suala tufike wakati uweze kulimaliza ili *airport* hii *terminal three* iweze kufanya kazl, bado imekwama na imekwama kwa sababu yako wewe na kila kitu kiko hapo mezani kwako Mheshimiwa Mpango. Kwa hiyo nikuombe sana ili kuwasaidia watu wanaoishi Zanzibar, fedha hizi ziweze kwenda na mradi huu uweze kutekelezwa.

Lakini la pili, Mheshimiwa Mpango tuna tatizo la ujenzi wa bandari ambayo Bandari ya Mpiga Duri. Hii kila siku watu wanapewa ahadi, hii ahadi imeshatosha. Wananchi wetu wanasubiri bandari ambayo inaweza kukuza uchumi wa Wazanzibar, lakini mpaka leo fedha yake na mpaka leo kinachoendelea bado hatujakijua. Lakini kule kunakwenda ahadi ambazo ahadi hazitekelezeki.

Mheshimiwa Mpango, tunayo bandari yetu ya Zanzibar ambayo ni ndogo leo ikija Meli moja kutoka nje, ikija ya pili basi isubiri zaidi ya wiki mbili ndio mzigo wa meli ya pili iweze kupewa gati. Sasa Mheshimiwa Mpango unategemea uchumi wa wazanzibar ambao unategemewa na unafahamu na uchumi wa Zanzibar unategemewa katika biashara ikiwa Meli ya pili inakaa kwa zaidi ya wiki mbili ndio ijje nyiningine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nikuombe sana, hili suala la kupeleka fedha au la kusaini la kumaliza suala la hizi fedha za bandari lifanyike haraka ili Wazanzibar waweze kupata maendeleo.

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mattar muda wako umekwisha. Mheshimiwa Neema Mgaya.

MBUNGE FULANI: Unga mkono.

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri aliyoifanya ndani ya miaka mitatu, lakini vilevile napongeza mapendekezo ya mpango ni mazuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazungumzaji wengi wamezungumzia suala la kilimo na wamejaribu kuishauri Serikali kwa namna mbalimbali nzuri ya kuweza kufanya kilimo chetu kiweze kuwa na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitaishauri Serikali katika sekta ya kilimo, lakini nitajikita katika suala zima la kuhakikisha kwamba tunaongeza thamani kwa mazao yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuongeza thamani kwa mazao yetu ni lazima tuweze kuanzisha viwanda vidogo vidogo kwa wingi, na niseme kwamba ni wakati sasa kwa Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Kilimo, wakae kwa pamoja ili waweze kuangalia ni namna gani bora ya kuweza kuanzisha viwanda vidogo vidogo ili viweze kusaidia mazao yetu yaweze kupata thamani kubwa na kuleta tija katika kilimo chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema tuanzishe viwanda vidogo vidogo, tukianzisha viwanda vidogo vidogo itatupelekea pia ku-*create* ajira nydingi. Kwa hiyo, vilevile pia tutakuwa tumeweza kutatua tatizo la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile huwezi ukazungumzia viwanda vidogo vidogo bila kuwa na uhakika wa vifungashio na ningependa kuishauri Serikali, kwa kuwa nia yetu ni njema ya kuhakikisha kwamba tunatengeneza ajira nydingi ndani ya nchi na viwanda vingi ndani ya nchi yetu, ni wakati sasa kuhakikisha kwamba tunazi-*support* zile taasisi kama *SIDO*, *TIRDO*, *TEMDO* na *CARMATEC* ili ziweze kutengewa pesa kuweza kuzalisha *tools*, zana za kilimo, vifungashio ili viweze ku-*support* vile viwanda vidogo vidogo na viwanda vyaa kati katika uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la Vijana wetu wanaokwenda Jeshini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi linachukua zaidi ya vijana 10,000 kwenye kila *operation*, lakini katika vijana 10,000 ni vijana chini ya 5,000 ndio ambao wanapata ajira katika vyombo vyetu vya ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wetu wanapokuwa kule Jeshini wanapata stadi za kazi mbalimbali, wanafundishwa masuala jinsi ya kufuga samaki, jinsi ya kufuga kuku, kufuga wanyama mbalimbali, jinsi ya kulima na mambo mengi mengi ya uchumi. Vijana hawa ambao wanakosa ajira kwenye vyombo vya ulinzi, inabidi warudi mitaani na wakirudi kule mitaani, wanakuwa tishio kubwa la usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi nilikuwa napenda kuishauri Serikali, kwa kupitia Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, lakini vilevile na Wizara ya Ulinzi waweze kufanya kazi kwa pamoja kuhakikisha kwamba vijana hawa wanaporudi nyumbani kwa sababu wana ujuzi mbalimbali waweze kuwaunganisha na Baraza la Uwezeshaji wa wananchi kiuchumi na kuwatengenezea mfumo maalum vijana hawa waweze kupata fursa ya kuweza kujajiri badala ya kutegemea ajira ambazo wanakuwa tayari wameshazikosa na wakaacha kuchanganyikiwa na kuijingiza kwenye masuala mabaya ya uhalifu na kusababisha kutokuwa na usalama kwenye maeneo hayo wanayotoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nilitaka pia Serikali iangalie umuhimu wa kuhakikisha kwamba katika vile viwanda vidogo vidogo ambavyo wanavyoenda kutengeneza, tuangalie kwamba kuwe na mpango maalum wa kuweza kuwashushia kodi wale ambao wameamua kuanzisha viwanda vidogo vidogo na ikiwezekana tuwape *grace period* ya kuanza kulipa kodi labda baada ya mwaka au mwaka mmoja na nusu, kwa kufanya hivyo itawasaidia wao kujijenga vizuri katika biashara zao na kuweza kuja kuwa waaminifu wakubwa katika kulipa kodi, kwa sababu watakuwa tayari wamesha tengemaa kwenye biashara zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NDG. ASIA MINJA - KATIBU MEZANI:

(Bunge Lilitrudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa tukae.

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo hapa mnatangaziwa wote Waheshimiwa Wabunge kuwa Fomu za Maadili ambazo huwa zinajazwa kabla ya tarehe 31 Desemba, kila mwaka zipo tayari. Hivyo Wabunge wote mnatakiwa kufika Ofisi ya Mheshimiwa Spika na kuchukua fomu hizo na kuzijaza kwa wakati. Kwa hiyo, mnakumbushwa Waheshimiwa kujaza hizo fomu.

Lakini nichukue fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushiriki wenu siku nzima ya leo kwa mawazo yenu yote, ambayo naami Mheshimiwa Mpango pamoja na timu yake yote na wataalam wako hapa wamewasikia. Naamini yako mengine ambayo ni ya mpango huu na yapo ya muda mrefu, wengine walikuwa wakichangia bajeti, kwa hiyo naamini utayachukua utayaweka kwenye bajeti ijayo.

Kwa hiyo nadhani kila eneo yamewekwa kwa hiyo wewe utayachukua yale yanayofaa na kuna wengine wamechangia ya miaka mitano ijayo, ile mingine. Kwa hiyo, kwa kuwa wataalam wako hapa sisi wanasiwa tunaweza kupungua pungua humu ndani zile asilimia 70, lakini wataalam wapo na naamini watafanya jambo zuri kwa sababu mawazo haya yametoka mapema.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo naahirisha shughuli za Bunge mpaka siku ya Jumatatu, tarehe 12 Novemba, 2018 saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.40 Usiku Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Jumatatu,
Tarehe 12 Novemba, 2018 Saa Tatu Asubuhi)*